# Nipashe

Jumatano Machi 18, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580182

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Lema ashtuka polisi kudaiwa kumsaka kwa mitutu hotelini

UKURASA 4



Wanawake mmejipanga au mnasubiri kuteuliwa?

Ukurasa 15

Wasichana vyuo vikuu wapata mbinu kupenya uchaguzi mkuu

Ukurasa 14

siasa

JUMATANO MACHI 18, 2020

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

Ukurasa 17

Mke wa Makamu Rais awa Waziri wa Ulinzi Sudan Kusini

FUNZO LA CORONA

Afrika ianze kujisimamia kiuchumi, isiiachie China kuifanyia kila kitu

Na Gaudensia Mngumi

INAENDELEA UK.16

Ukurasa 18

Uchaguzi Marekani kuweka historia ya rais kikongwe ?

Profesa Wangwe akitoa muhadhara wa masuala ya kiuchumi. PICHA: MTANDAO.

Mfumo ACT-Wazalendo kitendawili cha kikatiba, uchaguzi mkuu Ukurasa 19

UKURASA 13

TISHIO CORONA

# Serikali yachukua uamuzi mgumu

**SHULE** zote zafungwa kwa siku 30, mikutano, michezo yapigwa 'stop', bei za 'sanitizer', 'mask' zapaa na kuadimika... *Endelea Uk. 2, 3, 4 na 23*



Mussa Mbarouk, akinunua dawa ya kuoshea mikono (sanitizer), ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona, katika duka la dawa, eneo la Darajani, mjini Zanzibar jana. Galoni hilo, lenye ujazo wa lita tano, alilinunua kwa bei ya 75,000/-, wakati jijini Dar es Salaam liliuzwa kwa 120,000/- huku maski ikipanda kutoka 500/- hadi 5,000/- kwa moja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**



## BAA LA CORONA

BEI ya vifaa vinavyosaidia kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona imepaa, huku serikali ikiwaonya wafanyabiashara kwa kupandisha bei ya vifaa hivyo.

* **Epuka mikusanyiko ya watu**
* **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
* **Epuka kusalimiana na kushika mikono na kukumbatiana**
* **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## KIZIMBANI MADAI YA WIZI WA MABILIONI

UKURASA 4

# Mgonjwa wa kwanza nchini azungumza

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play

Download on the App Store



MICHEZO NDAYIRAGIJE AFURAHIA STARS KUJINOA KWA GPS UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

TISHIO CORONA

# Shule zote zafungwa

Na Mary Geofrey

SERIKALI imechukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na ugonjwa wa corona ambao umetangazwa kuwa janga la dunia.

Katika kuchukua hatua hizo, serikali kupitia Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, imetangaza kuzifunga shule zote kuanzia awali hadi kidato cha sita kwa siku 30 kuanzia jana.

Sambamba na kuzifunga kwa kipindi hicho, Majaliwa alisema serikali inafanya marekebisho ya ratiba ya mitihani ya kidato cha sita ambayo inatarajiwa kufanyika kuanzia Mei 4, mwaka huu.

Akizungumza na vyombo vya habari ofisini kwake, Magogoni jijini Dar es Salaam, Majaliwa pia alitangaza kuzuia mikusanyiko ya ndani na nje isiyo ya lazima kama semina, mikutano, makongamano, shughuli za kisiasa na mikusanyiko isiyo ya lazima ili kujikinga na ugonjwa huo.

Majaliwa alisema kama ambavyo serikali imeshazuia mbio za Mwenge za mwaka huu, Sh. bilioni moja ambazo zilizopangwa kutumika kwa shughuli hiyo, tayari Sh. milioni 500 zimeshapelekwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ajili ya kujikinga na maambukizi ya corona.

Kadhalika alisema serikali imesitisha michezo yote ikiwamo ya Ligi Kuu, Ligi Daraja la Kwanza na la Pili na michezo yote inayohusisha makusanyiko ya watu nchi kwa siku 30.

Alisema Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, itawaandikia barua wahusika wote juu ya kusitisha michezo hiyo kwa muda huo wa mwezi mmoja.

Kuhusu hatua zingine alisema: "Tunaendelea kuimarisha na kudhibiti wasafiri wote wanaingia nchini kwa kuwapima ili kubaini kama wana maambukizi. Watanzania wenye safari zisizo za lazima kwenye nchi zenye maambukizi makubwa, wanashauriwa wasitishe safari hizo."

Ili kuhakikisha udhibiti unafanyika kwa uhakika, Waziri Mkuu aliwataka wakuu wa mikoa na wilaya zote nchini katika maeneo yao, kufanya uchunguzi wa mara kwa mara kwa Watanzania wataoonekana kuwa na dalili za ugonjwa huo ili kuchukua hatua za haraka.

Akielezea hatua zilizochukuliwa baada ya mgonjwa wa kwanza kubainika kuwapo nchini Tanzania, Waziri Mkuu alisema serikali imechukua hatua kwa kumchukua mgonjwa huyo na kumhifadhi kwenye eneo maalum kwa ajili ya kumpatia huduma (isolation).

"Pia, serikali imefanya ufuatiliaji wa watu waliokutana na mgonjwa huyu tangu aingie nchini na kuwaweka kwenye karantini ya siku 14, na pia kuchukua sampuli kwa lengo la kubaini kama wameambukizwa virusi hivi," alisema.

Ugonjwa huo umeingia nchini baada ya Mtanzania mwenye miaka 46 aliyesafiri kwenda Ubelgiji, Sweden na Denmark hivi karibuni, kupimwa na kuthibitika kuwa na virusi vya Corona (COVID-19).

Majaliwa alsiema katika kukabiliana na ugonjwa huo, serikali inaendelea kuwajengea uwezo (mafunzo) watumishi wa sekta ya afya katika kukabiliana na magonjwa ya mlipuko ikiwamo jinsi ya kutoa tiba, kuchukua sampuli, uelimishaji na kuzingatia kanuni za afya.

"Serikali imetenga hospitali maalum za Mloganzila (DSM), Kituo cha Buswelu (Mwanza) na Hospitali ya Mawenzi (Kilimanjaro), Mnazi Mmoja (Zanzibar) na Chake-Chake (Pemba) kwa ajili ya kutoa huduma kwa waathirika," alisisitiza.

Aliiagiza Wizara ya Afya ihakikishe vifaa vya kinga ikiwamo vimiminika vya kudhibiti maambukizi (hand sanitizer) vinapatikana katika maduka yote husika na kwa bei ya kawaida na kuongeza kwamba serikali itachukua hatua kwa wafanyabiashara watakaobainika kufanya ulanguzi wa vifaa hivyo.

Aliwaomba viongozi wa dini waendelee kushirikiana na serikali katika kuwaelimisha waumini wao wote kuzingatia tahadhari za ugonjwa huu.

Pia alivitaka vyombo vyote vya habari vishirikiane na serikali katika utoaji wa elimu kwa umma kuhusu kujikinga na corona bila kufanya upotoshaji wala kuipa jamii hofu.

Amewataka wananchi watoe taarifa kuhusu uwepo wa mgonjwa au kupata ufafanuzi kuhusu ugonjwa huu kupitia namba za bure za 0800110124, 0800110125 na 0800110037.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Somanda 'B', wakinawa mikono kwa maji yaliyowekwa dawa ya Caroline, kabla ya kuingia madarasani shuleni hapo, mjini Bariadi mkoani Simiyu jana, ili kujikinga na homa ya virusi vya corona. **PICHA: HAPPY SEVERINE**

# Mgonjwa wa kwanza azungumza

Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA

MGONJWA wa kwanza kutangazwa kuugua corona nchini, Isabella Mwampamba (46), aliyelazwa kwenye Hospitali ya Mkoa Mount Meru jijini Arusha, amezungumza na Nipashe na anaendelea vizuri kiafya.

"Naendelea vizuri, waambieni watu kwenye 'groups' (makundi) ya Whatsapp waondoe wasiwasi kwani naoga mwenyewe na kupaka mafuta, kweli naendelea vizuri," alisema.

Juzi, Tanzania kupitia kwa Waziri wake mwenye dhamana ya Afya, Ummy Mwalimu, ilthibitisha kuwapo kwa mgonjwa wa kwanza wa corona huku serikali ikiwataka wananchi kuchukua tahadhari kuhusu mlipuko wa virusi hivyo.

Waziri huyo alisema mgonjwa huyo aliingia nchini Jumapili kupitia Uwanja wa Ndege Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) akitokea Ubelgiji.

"Machi 15 (Jumapili), tulipokea msafiri Mtanzania mwanamke (46), ambaye aliwasili nchini na ndege ya Rwanda Air akitokea Ubelgiji. Msafiri huyu aliondoka nchini Machi 3 mwaka huu na kati ya Machi 5 na 13, alitembelea nchi za Sweden na Denmark na kurudi tena nchini humo na baada ya hapo kurejea Tanzania," alisema.

"Msafiri huyu alipita KIA akafanyiwa ukaguzi na kuonekana kutokuwa na homa. Baadaye alianza kujisikia vibaya akiwa hotelini na kwenda Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mt. Meru ambako alichukuliwa sampuli na kupelekwa Maabara ya Taifa ya Afya iliyoko jijini Dar es Salaam kwa ajili ya uchunguzi.

"Vipimo vya maabara vimethibitisha kuwa mtu huyu ana maambukizo ya ugonjwa wa corona (COVID-19) na anaendelea vizuri," alisema.

Waziri huyo aliwatoa hofu wananchi kwamba tayari serikali inaendelea kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha ugonjwa huo unadhibitiwa usisambae nchini na wanashirikiana na Shirika la Afya Duniani (WHO) na wadau wengine katika kuendelea kutekeleza mikakati ya kukabiliana nao.

Alisema tayari amepigiwa simu na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, ambaye amemwambia kwa kuanzia watapewa Sh. milioni 500 ili kusaidia kukabiliana na ugonjwa huo.

Alisema tayari wametenga maeneo kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa watakaobainika kuwa na maambukizo ya ugonjwa huo.

Mwalimu alisema Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitarajiwa kukutana kwenye kikao cha dharura na mawaziri 12 ili kutafuta njia mbalimbali za kukabiliana na ugonjwa huo na jana, Mtendaji Mkuu huyo wa shughuli za serikali alitangaza hatua zilizochukuliwa.

# Maharusi misikitini kutoshikana mikono

Na Waandishi Wetu

SHEKHE wa Wilaya ya Kahama, Omary Damka, amesema kutokana na kulipuka kwa ugonjwa wa corona kuanzia sasa ndoa zitafungwa, lakini wahusika hawataruhusiwa kushikana mikono.

Akizungumza jana baada ya uchaguzi wa viongozi wa Jumuiya ya Waislam Tanzania (Istiqaamah) katika Msikiti wa Sangilwa Halmashauri ya Mji wa Kahama, mkoani Shinyanga, Shekhe Damka alisema wamelazimika kufanya hivyo kama tahadhari ya kukumbwa na ugonjwa huo.

Aidha, aliwaasa viongozi wa dini ya kiislamu nchini kuhakikisha kuwa wanafuata maelekezo ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na kuchukua tahadhari ya kushikana mikono.

**UFUNGUZI MASHINDANO YA SAYANSI WAFUTWA**

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imeahirisha ufunguzi wa mashindano ya kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (Makisatu), kwa mwaka 2020, kutokana na tishio la corona.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. James Mdoe, alisema wamezuia mikusanyiko kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa wa corona hata hivyo, maonesho yataendelea kwa kuwa hakutakuwa na wingi wa watu.

"Kuna hasara ndani yake, lakini hakuna namna ni lazima mikusanyiko izuiwe, " alisema Prof. Mdoe

**KONGAMANO LA VIJANA LASITISHWA**

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, amesitisha kongamano la vijana katika kilimo lililopangwa lifanyike jana, jijini Dar es Salaam, kuepukana na mikusanyiko kama tahadhari dhdi ya kusambaa kwa corona.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari jana, walikuwa wamepangwa kushiriki kongamano hilo kujadili fursa za kilimo, mifugo na uvuvi kwa kanda ya Dar es Salaam inayohusisha mikoa ya Pwani, Morogoro, Lindi na Mtwara.

"Rais John Magufuli ametoa rai kwa Watanzania kuchukua tahadhari dhidi ya vihatarishi vinavyoweza kusababisha maambukizi ya corona, kwa kuepuka mikusanyiko ya watu wengi isiyo ya lazima," alisema.

**Imeandikwa na Mohab Dominick (KAHAMA) na Renatha Msungu (DODOMA)**

## TISHIO CORONA

# Bunge lachukua hatua nzito

**Na Mwandishi Wetu**

KUTOKANA na kuwapo kwa tishio la ugonjwa wa corona, Bunge limechukua hatua nzito ikiwamo kusitisha kwa muda wageni, yakiwamo makundi ya wanafunzi au wananchi wanaotembelea kwa lengo la kuona au kujifunza shughuli zake.

Watakaoruhusiwa ni wenye kazi au shida mahususi, na shughuli za vikao vya Mkutano wa 19 wa Bunge zitaendelea kama kawaida kuanzia Machi 31, mwaka huu.

Kwa mujibu wa waraka wa Spika, Job Ndugai, namba 2 wa mwaka huu, uliotolewa jana na ofisi yake, kuanzia sasa kutakuwa na matumizi ya vifaa vya kupimia joto la mwili na vya kuoshea mikono katika maeneo ya Bunge.

"Tumefanya utaratibu wa kupima joto la mwili kwa wote wanaoingia kwenye eneo la Bunge kwa kuweka vifaa vya kupima joto la mwili, pia kuna vifaa vya kuoshea mikono katika maeneo ya getini, milangoni na kwenye mashine za alama za vidole. Kila mmoja avitumie kwa ufanisi na kila wakati," alisema Spika Ndugai.

Kuhusu ziara za kikazi za kamati ndani ya nchi, waraka unaeleza kuwa zitaendelea hadi itakapoamuliwa vinginevyo, na kwamba kamati zilitahadharishwa kuhusu kutembelea maeneo yenye msongamano.

Waraka huo ulisema vikao vya kamati vitafanyika kwenye kumbi zilizopo maeneo ya Bunge na vitahusisha wadau wachache.

Aidha, Bunge limesitisha safari za kikazi nje ya nchi, ikiwamo ushiriki wa vikao na mikutano ya kibunge, na kwamba kama wabunge wana safari binafsi, wachukue tahadhari.

"Safari za matibabu nje ya nchi kwa wanaogharamiwa na Bunge hasa kwa nchi zenye ugonjwa huo zitasitishwa kwa muda, na vibali vya safari hizo havitatolewa hadi serikali itakaposhauri vinginevyo," alifafanua.

Kwa mujibu wa waraka huo, semina na mafunzo kwa wabunge zitafanyika maeneo ya kumbi za Bunge.

Spika Ndugai alisema wabunge au watumishi wa bunge waliotoka safari za nje ya nchi watatakiwa kupitia zahanati ya Bunge kujiridhisha kama wapo salama kabla ya kuendelea na majukumu yao.

Ndugai aliwataka wananchi kuchukua tahadhari muhimu za kiafya, ili kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo.



Wafanyakazi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), wakinawa mikono wakati wa kuingia ofisini jijini Dar es Salaam jana, ili kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona. Kushoto ni Meneja wa Huduma kwa Wateja, Doreen Kiwango, Ofisa Habari, Joseph Mkonyi (katikati) na Meneja wa Stoo, Demitridah Sospeter. **PICHA: FRANK MONYO**

# Maji tiba, 'mask' zapanda bei, zaadimika kila mahali

**Na Waandishi Wetu**

BEI ya maji tiba (sanitizer) na 'mask' zimepanda bei maradufu na kuwafanya wengi kushindwa kumudu, huku wananchi wakiiomba serikali kuchukua hatua dhidi ya ulanguzi huo.

Nipashe ilipita katika maduka ya dawa muhimu maeneo ya Kimara wilayani Ubungo na kukuta 'mask' moja ikiuzwa kwa Sh. 5,000 kutoka Sh. 500 huku maji-tiba yakiwa yameadimika madukani.

Mmoja wa watoa huduma kwenye duka la dawa Kimara Baruti (jina linahifadhiwa), alisema 'mask' hizo zimeadimika dukani kwa sababu wafanyabiashara kutoka China hawajaleta nchini.

"Kweli gharama imepanda sana kwa sababu kabla hazijaadimika tulikuwa tunauza moja kwa Sh. 500, lakini sasa hivi tunauziwa boksi zima kwa Sh. 80,000 badala ya Sh. 5,000 na ndani zimekwa 50," alisema mtoa huduma huyo.

Grace Kadesha, mfanyabiashara wa duka la dawa Kimara Mwisho alisema wananunua 'mask' kutoka kwa watu binafsi ambao wanawauzia kuanzia 60,000 hadi 100,000 kwa boksi moja.

Kuhusu maji-tiba, alisema bidhaa hiyo imeadimika madukani kote, hivyo gharama zake nazo zitakuwa zimeongezeka kwa wauzaji ambao watakuwa nazo.

Alisema awali walikuwa wanauza maji-tiba yenye ujazo wa milimita 25 kwa Sh. 250 lakini kwa sasa yanauzwa kwa Sh. 5,000.

Kutokana na kuadimika kwa majitiba ya kujikinga na virusi vya corona, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, aliwataka wafamasia wote nchini kuchangamkia fursa ya kutengeneza vifaa vya kujikinga kama maji-tiba na maski za kuziba pua na mdomo ili kuvisambaza maeneo yote nchini.

Ummy alitoa agizo hilo juzi, wakati akifungua Kongamano la Kisayansi la Chama cha Wafamasia (PST) na kusema mbali na maji-tiba pia vifaa vya kuziba pua na mdomo vimeanza kuadimika hivyo wanajitahidi kuzalisha kwa wingi.

"Kutokana na tishio la ugonjwa wa corona, nawasihi wafamasia kuchangamkia fursa ya kutengeneza Clorine (maji-tiba) ya kusaidia kujikinga na ugonjwa huu. Kwa sasa mahitaji ni makubwa kwa sababu bidhaa hizo zimeanza kuadimika," alisema Ummy.

Mkoani Kagera, wananchi wamlalamikia kukosa vifaa hivyo kwenye maduka mbalimbali mkoani humo.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wakazi wanaongia kwenye maduka ya dawa za binadamu kutafuta vifaa kinga walisema wanapitia changamoto nyingi katika kuvitafuta.

Ivan Longino, mkazi wa mtaa wa Mafumbo alisema maduka yameishiwa vifaa hivyo hulazimika kutumia sabuni za mche kwenye familia zao.

Alisema licha ya kutokupatika vifaa hivyo bado vilikuwa havitumiwa sana na watu baada ya kutangaza janga la ugonjwa watu wameingia hofu na kununua lakini bado hatuelewi namna ya kutumia.

Jamali Abdul alisema kuna baadhi ya wakazi ambao wamechukua kinga hizo bado kuna uhitaji na kwamba serikali itafute namna ya upatikanaji kwani katika maduka ya sawa hakuna vifaa hivyo.

Muuzaji wa vifaa hivyo, Shakira Hussein, alisema kwa kipindi hiki dawa haipatikani na watu wamejitokeza kununua kwa wingi.

Alisema hivi sasa sabuni ya kuonyesha mikono yenye ujazo wa mil. 6 iliuzwa kati ya Sh. 2,000-3,500 ikiwa hapo awali iliuzwa Sh. 15,000 kutokana na uhitaji.

Aliongeza kwa upande wa vifaa vingine kama maski ni shilingi 1,000 kwa kila moja na grovu ni Sh. 2000 katika vifaa hivyo havijapanda bei sawa na sabuni.

***Mary Geofrey (Dar) na Restuta Damian (BUKOBA). Habari zaidi uk. 23***

# Waziri asema chanjo corona haijapatikana

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, amewatahadharisha wananchi kuacha kujidanganya na taarifa za mitandao ya kijamii kwamba chanjo ya corona imepatikana, kwa kuwa kupatikana kwake kunaweza kuchukua mwaka mmoja.

Akihojiwa na ITV katika kipindi cha mahojiano maalum, alisema ni vema wananchi wakaweka nguvu zaidi katika kuendelea kujikinga na kuchukua tahadhari ya ugonjwa huo kwa kuwa upatikanaji wa chanjo yake unaweza kuchukua muda mrefu.

"Kwenye mitandao ya kijamii kuna watu wanapotosha sana, kusema kwamba kuna sehemu fulani chanjo imepatikana. Bahati nzuri mimi ni daktari bingwa katika magonjwa haya ambukizi, kwa mfano kwa ugonjwa huu ambao tumeubaini wa corona, kuupatia chanjo yake inaweza kutuchukua si chini mwaka mmoja," alisema.

AONYA VYOMBO VYA HABARI

Amevionya vyombo vya habari kuacha kuwahoji watu wasio na utaalamu na kutumia taarifa zao ambazo zitawachanganya wananchi.

Alikanusha uvumi kuwapo mgonjwa mwingine katika Hospitali ya Mt. Meru.

"Tunaendelea kufanya ufuatiliaji wa watu wengine ambao walikutana na yule mgonjwa, hatuna mgonjwa mwingine wa corona ndani ya nchi, tupuuzie hayo mengine ya wapotoshaji ambao wanasema kuna wagonjwa wanane, hakuna hao wagonjwa, huu ugonjwa huwezi ukaufìcha," alisema.

**HALI YA MGONJWA**

Mgonjwa huyo anaendelea vizuri na anazungumza kama kawaida na waliokutana naye wamepatikana na kuchukua hatua ikiwamo kuchukua sampuli zao.

**GHARAMA ZA MATIBABU**

Fedha zilizotengwa kwenye mbio za Mwenge zitasaidia kununua vifaa vitakavyotumika kuwahudumia wagonjwa watakaogundulika kuwa na virusi hivyo kwa sababu inaporipotiwa kesi ya mgonjwa mmoja lazima atengwe kwa siku 14.

"Mgonjwa inabidi ale, kuna vifaa ambavyo vitatumika kwa wale wote wanaomhudumia, kuna suti, lakini kuna wale ambao aliokutana nao, ambao inabidi tukiwabaini, tuwaweke na tuwatunze, kwa hiyo mnyororo kwa mtu mmoja unaweza kutugharimu hata Sh. milioni 20 au 30."

**MAJI TIBA**

Alisema serikali imepata malalamiko ya kupanda kwa gharama za maji tiba (sanitizer) na 'mask' na kwamba serikali haitakubali watu watumie janga hilo kufanya ulanguzi.

"Nitoe rai kwa jamii wasiwe na taharuki, maji tiba siyo suluhu pekee, mtu unaweza kunawa kwa kutumia sabuni na maji yanayotiririka mara kwa mara, kuepuka msongamano na mikusanyiko isiyo ya lazima," alisema na kuongeza;

"Lakini nitoe rai kwa wafanyabiashara ambao wanataka kupata faida kubwa kutokana na janga kama hili, tutakaa na kutoa tamko kama serikali kuhakikisha watu hawafanyi ulanguzi kutokana na janga hili."

# Lema ashtuka polisi kudaiwa kumsaka kwa mitutu hotelini

**Na Romana Mallya**

MBUNGE wa Arusha Mjini, Godbless Lema, ameshangazwa na taarifa za kuwapo kwa askari polisi wenye silaha wanaomtafuta hotelini.

Amesema taarifa hizo zimemshtusha kwa kuwa yeye si jambazi na namba zake za simu ziko wazi kama anahitajika kwa jeshi hilo.

Katika ukurasa wake wa Twitter jana, Lema aliandika: "Sijui natafutiwa nini? Natafutwa kama jambazi, namba zangu za simu ziko wazi, hivyo kulikuwa hakuna sababu ya kuja na polisi zaidi ya 15 wakiwa na silaha kunitafuta hotelini."

Kabla Lema hajaandika ujumbe huo, jana asubuhi, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kupitia kwa Mkuu wake wa Kitengo cha Mawasiliano, Tumaini Makene, kilidai askari polisi wamezingira hoteli aliyofikia mbunge huyo iliyoko Mikocheni jijini Dar es Salaam.

Taarifa hiyo ya Chadema ilidai kuwa Lema ambaye ni Waziri Kivuli wa Mambo ya Ndani ya Nchi, anatafuta na polisi kwa sababu zisizojulikana.

"Lema alikuwa azungumze na vyombo vya habari leo (jana) Dar es Salaam kumjibu DPP (Mkurugenzi wa Mashtaka nchini)," ilisema taarifa hiyo ikiwa ni muda mfupi baada ya Makene kutuma taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu kuahirishwa kwa mkutano huo wa Lema na wanahabari.

Makene alisema mkutano huo umeahirishwa kwa sababu Lema amelazimika kuanza safari kwenda Singida kwa kupitia Arusha kwa dharura.

"Polisi hao wenye silaha, wasiokuwa na sare za polisi, wako ndani ya gari na wengine mapokezi ya hoteli... (alitaja jina la hoteli). Wamelazimisha uongozi wa hoteli ufungue chumba cha Lema, walivyojibiwa ni kinyume cha taratibu, wamewaonya wafanyakazi iwapo hawatampata mbunge huyo," ilidai taarifa hiyo ya Chadema.

Nipashe ilipomtafuta Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni, ili kuzungumzia suala hilo alidai kuwa na kikao.

Machi 12, DPP, Biswalo Mganga, alimtaka Lema ajitokeze na kueleza lini amekwenda kutoa taarifa kituo chochote cha polisi kuhusu matukio ya watu 14 waliouawa na hatua kutochukuliwa.

Februari 29, mwaka huu, Lema akiwa katika mazishi ya Katibu Mkuu wa Chadema Jimbo la Manyoni, Alex Joas, alitaja orodha ya watu 14 waliouawa kwa kuchinjwa na kuchomwa moto wilayani humo.



Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela na Mkurugenzi wa Mawasiliano wa benki hiyo, Tully Mwambapa, walipotembelea ofisini kwake jijini Dar es Salaam jana, kuzungumza namna ya kuboresha mahusiano kati ya CRDB na Jeshi hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kizimbani tuhuma za wizi mabilioni kampuni ya ulinzi

**Na Beatrice Shayo**

WATU saba wakiwamo wafanyakazi wa Kampuni ya Ulinzi ya G4s Secure Solution Tanzania Limited, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam wakikabiliwa na mashtaka ya utakatishaji fedha Sh. bilioni 2.2.

Washtakiwa hao ni pamoja na Christopher Rugemalila (34), mlinzi na mkazi wa Chanika, Ramadhani Athumani (40), mlinzi na mkazi wa Kijichi, na Ibrahim Maunga (49), mfanyabiashara na mkazi wa Kiluvya jijini.

Wengine ni Salim Mtandika (45), mlinzi na mkazi wa Mbagala Kizuiani, Dismas Mgongolwa (45), mkazi wa Kibamba, Godfrey Saimon (33), mkazi wa Manzese na Ladislaus Macha (44), mkazi wa Ukonga Kipunguni jijini.

Washtakiwa hao walifikishwa mahakamani jana na kusomewa mashtaka dhidi yao na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Mkunde Mshanga, mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Augustina Mbando.

Wakili Mshanga alidai katika shtaka la kwanza, washtakiwa wote wanadaiwa kuwa kati ya Februari Mosi mwaka huu na Februari 7 mwaka huu, ndani ya Jiji la Dar es Salaam, kwa pamoja waliungana na kuunda genge la uhalifu kisha kuiba kiasi cha Sh. bilioni 2.2.

Mshanga alidai mahakamani kuwa katika shtaka la pili, Februari 7 mwaka huu, eneo la Chang'ombe, Temeke jijini, washtakiwa hao kwa pamoja waliiba Sh. bilioni 1.2, Dola za Marekani 402,000, sawa na Sh. milioni 924.6 na na Euro 22,700, sawa Sh. milioni 59, hivyo kuiba jumla ya Sh. bilioni 2.2, mali ya Kampuni ya G4s Secure Solution Tanzania Limited.

Katika shtaka la tatu, linalomkabili Christopher, Ramadhani na Ibrahim, inadaiwa kuwa Februari 7 mwaka huu, maeneo ya Chang'ombe, Temeke jijini, washtakiwa hao kwa pamoja wakiwa wafanyakazi wa Kampuni ya G4s Secure Solution Tanzania Limited, waliiba fedha Sh. bilioni 1.2 na Dola za Marekani 402,000, mali ya mwajiri wao.

Mshanga alidai katika shtaka la nne, Februari 7 mwaka huu na Februari 23 mwaka huu, washtakiwa wote kwa pamoja, walijipatia kiasi cha Sh. bilioni 2.2 kutoka kwenye Kampuni ya G4s Secure Solution Tanzania limited huku wakijua fedha hizo zinatokana na mazalia ya uhalifu na kosa la wizi.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, washtakiwa hao hawakuruhusiwa kujibu chochote, Upande wa Mashtaka ukidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika.

Washtakiwa hao walipeleka rumande kwa kuwa kesi hiyo haina dhamana na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu haina uwezo wa kusikiliza kesi za uhujumu uchumi.

Februari 25 mwaka huu, Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam lilitangaza kuwashikilia watu wanne, wakiwamo wafanyakazi hao wa Kampuni ya Ulinzi ya G4S kwa tuhuma za wizi wa fedha walizokuwa wakizipeleka makao makuu ya Benki ya NBC kutoka katika matawi ya benki hiyo.

000000

# Corona yazua taharuki Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

WANANCHI na wagonjwa katika Hospitali ya Global mjini hapa wamepatwa na taharuki baada ya kuwapo taarifa za wagonjwa wawili raia wa kigeni wanaoshukiwa kuwa na dalili ya mambukizi ya ugonjwa wa corona.

Wagonjwa waliolazwa hospitalini hapo walilazimika kutolewa nje ili kuruhusu wafanyakazi wa hospitali hiyo kuchukua hatua za awali za kinga ikiwamo kupuliza dawa.

Ofisa mmoja wa hospitali hiyo ambaye hakutaka kutaja jina lake, alisema wamepokea raia wawili wa kigeni waliofikishwa hospitalini hapo na kuchukuliwa vipimo vya ugonjwa huo.

Alisema vipimo vya watu hao vimepelekwa Tanzania Bara kwa ajili ya uchunguzi zaidi ili kupata majibu sahihi.

"Ni kweli wapo raia wawili wa kigeni wamefikishwa hapa kwa ajili ya vipimo vya corona na vimepelekwa Tanzania Bara kwa ajili ya majibu," alisema.

Uongozi wa Hospitali ya Al-rahma, umekiri kupokea mgonjwa ambaye amechunguzwa vipimo kwa ajili ya ugonjwa wa corona.

"Ni kweli yupo mtu tunamchunguza kuhusu ugonjwa wa corona na madaktari kutoka Wizara ya Afya walifika hapa kuchukua vipimo vyake na kupelekwa Tanzania Bara lakini sisi sio wasemaji," alisema daktari mmoja.

Waziri wa Afya, Hamad Rashid Mohamed alikutana na Kamati ya Baraza la Wawakilishi la Ustawi wa Jamii na kukanusha kuwapo mgonjwa aliyethibitishwa kuugua ugonjwa wa corona hadi sasa.

Alisema zipo zaidi ya kesi tisa za watu waliochunguzwa ugonjwa huo, lakini hakuna aliyethibitishwa kuambukizwa corona.

**"Ni kweli wapo raia wawili wa kigeni wamefikishwa hapa kwa ajili ya vipimo vya corona na vimepelekwa Tanzania Bara kwa ajili ya majibu," alisema.**

HABARI KITAIFA



Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Prof. Zacharia Mganilwa, akiangalia moja ya mtambo wa ukaguzi wa magari katika kampasi kuu ya chuo hicho Mabibo jijini Dar es Salaam. Kituo hicho cha ukaguzi wa magari kina uwezo wa kukagua magari 1,000 kwa siku. **PICHA: PROSPER MAKENE**

# Zitto aanza utetezi kesi mauaji watu 20 Kigoma

**Na Beatrice Shayo**

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, ameanza kujitetea katika kesi ya uchochezi inayomkabili kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam kuhusu taarifa za mauaji kwenye Kijiji cha Mpeta mkoani Kigoma.

Akiongozwa na Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala, jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, Zitto alidai, taarifa za mauaji hayo alizipata kupitia njia mbalimbali, wakiwamo wananchi wa eneo hilo.

Alidai njia nyingine ni vyombo vya habari na Husna Mwilima, Mbunge wa Kigoma Kusini (CCM), aliyesema ndani ya Bunge kuwa wananchi wake zaidi ya 20 wameuawa na kutaka uchunguzi ufanywe.

Alidai mahakamani kuwa maudhui yaliyoko kwenye kielelezo namba tatu ambayo ni taarifa aliyosoma kwa waandishi wa habari, yalikuwa na lengo la kulitaka Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina kuhusu masuala yaliyotokea Kijiji cha Mpeta Wilaya ya Uvinza.

Zitto, ambaye ni Mbunge wa Kigoma Mjini, alidai lengo lake ni kutaka baada ya uchunguzi, hatua za kisheria zichukuliwe kwa wote watakaobainika kutekeleza mauaji dhidi ya wananchi.

Alidai hakuna shahidi wa upande wa mashtaka aliyewasilisha nyaraka kuonyesha kuwa uchunguzi umefanyika na hakuna mtu aliyefariki dunia.

Zitto alinukuu mahakamani hapo taarifa aliyoitoa kwenye vyombo vya habari Oktoba 28, 2018 akitamka: "Wiki iliyopita, yalitokea mauaji ya askari polisi. Chama chetu kinatoa pole kwa IGP na kinalaani mauaji hayo na tunataka upelelezi ufanyike.

"Taarifa tunazipata zinaogofya mno, tumeambiwa raia zaidi ya 100 wameuawa na Jeshi la Polisi, haiwezekani tukio kubwa kama hilo serikali imekaa kimya. ACT kinafanya nini? Tunaitaka serikali kufanya uchunguzi na kutoa taarifa juu ya matukio haya."

Katika kesi ya msingi, Zitto anashtakiwa kwa makosa matatu likiwamo la kutoa maneno ya uchochezi katika mkutano wake na waandishi wa habari Oktoba 28, 2018 jijini Dar es Salaam.

# Mwandishi jela mwaka mmoja au faini mil. 5/-

**Na Beatrice Shayo**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam imewahukumu mwandishi wa habari, Shafii Dauda, na mtaalamu wa Tehama, Benedict Kadeghe, kulipa faini ya jumla Sh. milioni 10 au kwenda jela mwaka mmoja baada ya kukiri kosa la kuchapisha maudhui mtandaoni bila kuwa na leseni ya Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA).

Hukumu hiyo ilisomwa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi, Godfrey Isaya, alisema kutokana na utetezi uliyotolewa mahakamani hapo na akizingatia kuwa washtakiwa ni wakosaji wa mara ya kwanza, vijana na waandishi wa habari wanaotegemewa, kila mmoja atalipa faini Sh. milioni tano au kwenda jela miezi 12.

Alisema kwa kuzingatia maelezo ya upande wa utetezi na kwa mujibu wa sheria, kila mmoja atalipa faini hiyo na ushahidi wa kompyuta yao utataifishwa kuwa mali ya serikali.

Awali, Wakili wa Serikali Faraji Nguka alidai mbele ya Hakimu Mfawidhi, Godfrey Issaya, kuwa kesi hiyo imekuja kwa ajili ya kuwasomea maelezo ya awali.

Akiwasomea maelezo hayo, Wakili Nguka alidai kati ya Juni 14 na Septemba, 2018, kwa kutumia televisheni ya mtandao inayojulikana kwa jina la Shafii Dauda, kinyume cha sheria, walitoa maudhui katika mtandao huo bila leseni ya TCRA.

Baada ya kuwasomea maelezo hayo, Wakili Nguka aliwasilisha mahakamani hapo kompyuta mpakato aina ya MacBook na kuiomba mahakama kuipokea kama kielelezo.

Wakili wa Utetezi, Oscar Mgongolwa, aliiomba mahakama wakati wa kutoa adhabu, izingatie kuwa washtakiwa hao ni wakosaji wa mara ya kwanza na Upande wa Jamuhuri hauna rekodi ya makosa yao.

Alidai kitendo cha kukiri makosa kimeipunguzia mahakama muda mrefu wa kuendesha kesi hiyo na kuiomba izingatie utetezi na kutoa adhabu ndogo itakayofaa.


Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU**
*(Barua zote za kiofisi zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)*

**Mkoa wa Arusha**
Telegram: Meru
Simu: (+ 255) 027 254-1112
Faksi: (+ 255) 027 254-1112
Barua pepe:ded@merudc.go.tz
website:www.merudc.go.tz

HALMASHAURI YA WILAYA MERU DISTRICT COUNCIL

Ofisi ya mkurugenzi mtendaji,
**S. L. P 462,**
**USA RIVER**
**ARUSHA**

**26/11/2018**

**TANGAZO KWA UMMA**

**UUZAJI WA VIWANJA KATIKA MRADI WA NGURUDOTO ESTATE**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru kwa kushirikiana na Kampuni ya **ZULFIROZ ESTATE LTD** wanawatangazia wananchi wote kuwa zoezi la upimaji wa viwanja katika eneo la Ngurdoto limekamilika.

Eneo lipo karibu na Hoteli ya Ngurudoto na Shule ya St. Jude takribani Km 1.25 kutoka Barabara ya Rami iendayo Arusha National Park na Km 3.5 kutoka barabara kuu ya Moshi- Arusha. Kuna viwanja kwa ajili ya **makazi, makazi na biashara, biashara pamoja na viwanja vya matumizi ya Ibada.**

Bei ya kiwanja ni Tsh. 19,000/= kwa mita moja ya mraba. Kiwanja kinalipiwa ndani ya muda wa mwezi mmoja. Utaandaliwa hati baada ya kukamilisha malipo ya kiwanja.

Kwa yeyote anayehitaji kiwanja afike ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru kuchukua fomu na kuchagua kiwanja kuanzia tarehe ya tangazo hili.

Wananchi wote mnakaribishwa

IMETOLEWA NA:

Grace A. Mbilinyi
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU**

MKURUGEZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU
S.L.P. 462 USA RIVER
MERU - ARUSHA

215669602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maji ya Ziwa Victoria yawe fursa kwa wakazi wa Mkoa wa Tabora

MIKOA kadhaa nchini hususani ya kanda za magharibi, ziwa na kati imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa majisafi na salama.

Kutokana na hali hiyo, wakati wa uongozi wa serikali ya awamu ya tatu chini ya Rais Benjamin Mkapa ulianzisha na kutekeleza mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria kwa ajili ya kuchukua maji kutoka ziwa hilo na kupelekwa kwenye mikoa ambayo ilikuwa inakabiliwa na tatizo la maji.

Mbali na changamoto zilizokuwapo wakati wa kuanza utekelezaji, lakini Mkoa wa Shinyanga kwa mikoa ya Kanda ya Ziwa ambao ulikuwa unakabiliwa na changamoto hiyo, uliweza kufikiwa na maji ya mradi huo na wakazi wake wakaanza kunufaika kwa kuondokana na kero hiyo.

Wilaya ya Kahama iliyoko mkoani humo baadaye nayo ilifikiwa na mradi huo na kuwa mkombozi kwa wakazi wake ambao awali walikuwa wakipata ufumbufu mkubwa wa maji.

Sasa habari za kufurahisha ni kwamba sasa mradi huo umeingia katika Mkoa wa Tabora katika wilaya za Igunga na Nzega, na serikali inasema tayari wakazi wake wameshaanza kunufaika na huduma hiyo.

Mradi huo unagharimu Sh. bilioni 600 na utanufanisha wakazi milioni 1.8 katika vijiji zaidi ya 90 katika maeneo yote ya mradi kuanzia kanda ya ziwa hadi Tabora Mjini, Igunga na Nzega.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, alisema mwishoni mwa wiki kuwa mradi huo unapita zaidi ya kilometa 300.

Dk. Abbas ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, alisema kazi inayofanyika kwa sasa ni kupeleka maji hayo kwenye vijiji hivyo.

Hii bila shaka ni fursa muhimu kwa wakazi wa maeneo husika kwa kufanya shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi kwa lengo la kujiongezea kipato. Sasa wakazi wake wanaweza kufuga, kulima na shughuli nyingine ambazo zinategemea maji.

Kutokuwapo kwa uhakika wa maji kulikuwa kikwazo kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii, hivyo tunaamini kuwa wakazi wa maeneo husika wataichangamkia fursa hiyo kwa ajili ya maendeleo yao.

Tunasema hivyo kwa kuwa maendeleo yameshuhudiwa katika maeneo kadhaa ya Mkoa wa Shinyanga ambayo kabla ya kufikiwa na mradi huo yalikuwa yakikabiliwa na vikwazo vingi.

Kufikiwa na fursa hiyo hakunabudi kuwaamsha wananchi kuchangamka kwa kuanza kuomba kuunganishiwa huduma ya maji kwa kuwa wameshafikiwa kwenye maeneo yao.

Mradi huo kwa kufika mkoani Tabora ni ishara kuwa mikoa mingine hususan ya Kanda ya Kati ya Singida na Dodoma, wenye changamoto hiyo inaweza kufikiwa na kunufaika.


Utekelezaji wa mradi huo inatia matumaini kuwa nchi yetu inaweza kunufaika kwa rasilimali zilizopo yakiwamo maji, ikiwa kutakuwa na ubunifu katika kuzitumia kwa maendeleo ya taifa na wananchi wake.

Ziwa Victoria liwe mfano kwamba rasilimali nyingine za maji zilizoko zitumike vizuri kuiendeleza nchi yetu. Kwa mfano Tanzania ina maziwa mengine na mito mikubwa, ambayo inapaswa kutumika kupeleka maji katika maeneo ambayo yanakabiliwa na uhaba wa maji.

Kwa kuzitumia rasilimali hizi kupitia utekelezaji wa miradi mikubwa, bila shaka Watanzania wengi watafikiwa na huduma za maji ya uhakika, huku lengo la serikali likiwa ni kuwa hadi kufikia mwishoni mwa mwaka huu, tutakuwa tumefikia azma ya kufikia lengo la asilimia 85 vijijini na mijini asilimia 95.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Maridhiano ya kisiasa yapewe nafasi kabla ya mikutano

MSINGI wa demokrasia unatajwa kwamba ni ushirika wa maridhiano, ambao unaweza kuunganisha pande mbili zinazotofautiana na hatimaye kurejesha umoja na mshikamano wa kitaifa.

Kutokana na hilo, hata wanasiasa wanapotofautiana katika mtazamo au jambo ambalo wanadhani linatakiwa kupatiwa ufumbuzi, hawana budi kutafuta maridhiano pale wanapoona mambo hayaendi sawa.

Nimeanza kwa kuelezea hayo kidogo, kufuatia kile ambacho kimetangazwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kwamba kinatarajia kuanza mikutano ya hadhara nchi nzima kuanzia mwezi ujao.

Lengo la mikutano hiyo ni kudai tume huru ya uchaguzi kwa mujibu wa sheria, hasa wakati huu ambao nchi inaelekea kwenye maandalizi ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 2020.

Mwenyekiti wa Chadema Taifa, Freeman Mbowe, ndiye aliyekaririwa na vyombo vya habari akisema hayo kwenye makao makuu ya chama hicho jijini Dar es Salaam hivi karibuni, lakini akagusia umuhimu wa suala la maridhiano.

Mbowe anasema kwamba kabla ya chama chake kuanza mikutano ya hadhara nchi nzima, anaona bado kuna nafasi ya kuchukuliwa kwa hatua za kutafuta maridhiano ya kisiasa.

Yapo mengi ambayo kiongozi huyo ameyaongea, lakini hili la maridhiano lingepewa uzito zaidi ili wadau wote wa siasa wakutane na kuweka mambo sawa kuliko kulazimisha kuwapo kwa mikutano.

Lakini, nikirejea kwenye hoja ni kwamba kutafuta maridhiano ni moja ya hatua za ukomavu wa kisiasa ambao unatakiwa kuendelezwa na zinaweza kusaidia kumaliza sintofahamu hiyo wanayolalamika.

Pamoja na hayo, wanasiasa wanatakiwa kutambua kuwa umoja wa kitaifa ni muhimu kuliko vyama vya siasa, hivyo ulindwe ili usije kuwatenganisha Watanzania kwa itikadi za vyama vya siasa.

Ni muhimu kutambua kuwa maridhiano ndiyo njia pekee ya kumaliza mkwamo wowote ambao unaweza kujitokeza badala ya kutumia njia ambayo wakati mwingine inaweza isizae matunda mazuri.

> **Ni muhimu kutambua kuwa maridhiano ndiyo njia pekee ya kumaliza mkwamo wowote ambao unaweza kujitokeza badala ya kutumia njia ambayo wakati mwingine inaweza isizae matunda mazuri.**

Umuhimu wa maridhiano ni kwamba yanaepusha malumbano ambayo kwa kawaida huwa hayajengi, hivyo msuguano wa kisiasa uwe wa nguvu ya hoja siyo hoja za nguvu.

Vyama vya siasa vimekuja na vitapita, lakini Tanzania itaendelea kuwapo, hivyo jambo la kukazania ni kutafuta maridhiano ya kisiasa ili hatimaye sintofahamu, ambayo wanaiona imalizike.

Maridhiano au meza ya mzungumzo, mara nyingi huwa inasaidia kupata muafaka, kuliko kukaa pembeni na kulalamika au kususa ama kufanya jambo ambalo wakati mwingine halina afya kwa umma.

Hatua ya viongozi wa upinzani kutoa wito wa kuwapo maridhiano ya kisiasa mbele ya Rais John Magufuli, ninaitafsiri kuwa ni dalili za kufunguliwa kwa ukurasa mpya wa siasa za maridhiano.

Siasa hizo ndizo ambazo zinaweza kujenga umoja wa kitaifa, kwa kutanguliza maslahi ya nchi kwanza badala ya vyama, hasa kwa kutambua kuwa vyama vya siasa vinapita, lakini Tanzania itaendelea kuwapo hadi ukamilifu wa dahari.

Kwa hiyo juhudi za wadau wa siasa kutafuta namna ya kukutana kwenye meza ya mazungumzo ni za muhimu kwa ajili ya maridhiano ya kisiasa kwa manufaa ya taifa na watu wake.

Lakini pamoja na hayo, subira na uvumilivu ni mambo ya msingi na ndivyo ambavyo vinaweza kuzaa muafaka iwapo suala la meza ya mazungumzo kwa ajili ya maridhiano litapewa nafasi.

Kwa sababu Mbowe ameonyesha bado anahitaji maridhiano, basi asichoke kuyatafuta, kwani kuna msemo wa Kiswahili kwamba; Mvumilivu hula mbivu na atafutaye hachoki, hivyo yote yanahitajika.

## BARUA / MJADALA

# Serikali iingilie usafirishaji huu

**MHARIRI,**

*WAZAZI na wapenda maendeleo ya watoto watakubaliana nami kuwa msimu wa mvua unasababisha magari mengi ya shule kuharibika na kusumbua sana watoto hiyo ni kutokana aidha na ubovu wa barabara au magari yenyewe.*

*Hiki ndicho tunachokiona kwa wanafunzi wengi wanaosoma kwenye shule zenye huduma hiyo ya usafiri.*

*Nachelea kusema magari mengi ya shule ni mabovu na mara nyingi shule husika zinatumia magari ambayo yamechoka kabisa kiasi kwamba hata ukiliona lazima ujiulize mwenye shule halioni au, hivyo basi kutokana na asha hiyo, je, kuna polisi wa usalama barabarani wanaosimamia na kukagua uzima wa magari hayo ya shule?*

*Kama hakuna tunahitaji hatua zichukuliwe sasa haipendezi kuona watoto wetu wadogo wakisimama barabarani kunyeshewa mvua na hata kuchelewa kurudishwa nyumbani kisa magari ni mabovu.*

*Pia serikali iangalie suala la miundombinu ya barabara kipindi hiki cha mvua, maana ubovu wa barabara nao husababisha magari kuzidi kuharibika zaidi.*


*Tunaomba serikali iyakague sasa magari yote yenye hitilafu ili kuyazuia kubeba wanafunzi.*

***Ni Mchikirwa Karani, Dar es Salaam***

## WASILIANA NASI:

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# Corona inavyotoa somo la ujenzi wa viwanda




**Na Gaudensia Mngumi**

KATIKA kipindi hiki cha homa ya mafua ya corona umuhimu wa kujitegemea kiuchumi hasa kuzalisha kutoka kwenye viwanda vya ndani badala ya kutegemea uagizaji bidhaa nje, linaibuka kwa nguvu zote.

Huo ndiyo wakati wa nchi maskini hasa za Afrika pamoja na Tanzania kujitafakari kuwa iwapo corona au COVID 19 itaendelea kwa miezi mingi, hatima ya biashara itakuwaje?

Si suala la kupuuza tena, ni kitu cha kuishughulisha Wizara ya Viwanda kuhusu hatima ya taifa kutokana na hatari ya kuishiwa na bidhaa kwenye maduka kwa vile kiasi kikubwa kiliagizwa kutoka China au ng'ambo.

Mathalani, Tanzania licha ya kuwa na viwanda vya nguo na kuzalisha pamba kwa wingi duniani, leo 2020 taifa halijaweza kujitosheleza kwa nguo na sasa kila kitu kinaagizwa kutoka China ambayo ina corona.

Kuanzia mwaka 1970 hadi 1985 sekta ya viwanda vya nguo ilikuwa inaongoza kwa kuajiri idadi kubwa ya wafanyakazi wakifikia takribani 37,000, takwimu za mkakati wa Serikali ya Tanzania wa kuendeleza sekta ya nguo unaoitwa From Cotton to Clothes wa 2016.

Unaongeza kuwa licha ya kuajiri idadi kubwa ya wafanyakazi, sekta hiyo, iliongoza kwa kuuza bidhaa nje na ilikuwa ya tatu katika kuchangia kodi ya serikali.

Viwanda vya nguo vilivyokuwa vinatikisa zama hizo ni pamoja na vile vilivyokuwa mikoa ya Mwanza (Mwatex) , Musoma -Mutex, Arusha, Morogoro na Dar es Salaam ikisifika kwa kiwanda cha Urafiki, Sunguratex na Kilitex.

Viwanda hivyo vilikuwa na umuhimu wa kipekee kiuchumi kwa vile kazi zake, zilianzia kwa wakulima vijijini wakizalisha na kuuza pamba kwenye vyama vya ushirika navyo vilifikisha zao hilo kwenye vinu vya kuchambua pamba ambavyo vilizalisha mashudu pamoja na mafuta vyote hivyo vikitengeneza ajira kwa watu wengi.

Mlolongo ni mrefu na mwisho kabisa pamba ilisokotwa kuwa nyuzi na kutengeneza nguo za aina mbalimbali na idadi kubwa ya Watanzania walipata kazi.

Hata hivyo, licha ya mafanikio hayo ya miaka kadhaa, leo habari imebadilika kwani viwanda vya nguo vya umma, vimeshindwa kumudu ushindani wa soko huria na bidhaa karibu zote za nguo zinaagizwa kutoka China na mitumba kutoka Ulaya na Marekani.

Uchumi wa soko huria umeruhusu uingizaji mitumba na nguo za bei nafuu kutoka nje. Kadhalika kuanguka kwa uchumi wa nchi za Afrika, ubinafsishaji, kuongezeka kwa gharama za uzalishaji, uliviumiza viwanda hivyo ambavyo jitihada za kuvifufua hazikuwa na msukumu mkali mbali na kuruhusu uagiza bidhaa kutoka China.

Leo mambo yamegeuka. Madera yaliyokuwa yamejaa Kariakoo, nguo za kila aina na mashuka mepesi na mapazia yaliyokuwa yanatembezwa kila kona ya nchi hii pamoja na mitumba kutoka Ulaya na Marekani huenda isipatikane kwa urahisi kutokana na janga la corona.

Sababu mojawapo zinazotajwa na wataalamu wa viwanda vya nguo duniani ni kwamba viwanda vya nguo vya Afrika havikuendi kwa sababu ya changamoto za uhaba wa umeme, maji, ukosefu wa teknolojia ya kisasa na kutegemea mali ghafi kutoka nje.

Ni maelezo ya mtandao wa the International Textile Manufacturers Federation (ITMF), hivyo Waafrika wakaendelea kuagiza mabelo kwa mabelo ya mitumba kutoka nje na makontena kwa makontena kutoka China.

Pamoja na soko huria kuleta changamoto kuna mambo yenye tija ambayo taifa litakuja kujuta na kurudisha mikakati ya kujitegemea hasa kutokana na corona.

Hata bila corona haikufaa kukaa kimya ilitakiwa kujifunza fursa ambazo zimetokana na mabadiliko ya sekta ya viwanda vya nguo na jambo la muhimu ingekuwa ni kuhamasisha sera ya uwekezaji mpya kwenye nguo.

Haikufaa kukaa kimya kama jitihada zilihitajika kuwekeza kwenye kushona nguo za michezo ya aina zote ziwe za michezo (jezi), masweta ya wanafunzi, sare za wanafunzi na watumishi mbalimbali badala ya kukaa kimya kuangalia viwanda vikifa na mashine kuliwa na kutu.

Hata hivyo kuna viwanda vya nguo vya kisasa ndani vya Ukanda wa Uwezekaji (EPZ), vinavyoonyesha kuwa biashara ya kushona mavazi haina gharama kubwa ikilinganishwa na kujenga viwanda vya kutengeneza nguo, pia kushona mavazi ni uwekezaji mkubwa duniani.

Uzalishaji ni lazima ungefanyiwa mikakati ili kuubadilisha badala ya kuendeleza Urafiki, Mwatex, Kilitex na Sunguratex kungekuwa na haja ya kuanzisha ushonaji na utengenezaja wa mashuka na fulana, soksi, za wanafunzi, vitenge na hata vikoi ili kubadilisha na kuhuisha viwanda hivyo.

Kwa vile serikali ilibaini kuwa ujenzi wa viwanda vya nguo ni gharama kubwa zaidi kuanzia ununuzi na ufungaji wa mitambo na vifaa vya uchambuzi wa pamba, wahandisi, usokotaji nyuzi, ufumaji na uchapaji, kadhalika gharama kubwa za uendeshaji, maji, umeme na malighafi zinazohitaji kwenye uchakataji, kubadilika lilikuwa jambo lisilokwepeka.

Hata hivyo, ukilinganisha gharama hizo ni wazi kuwa uwekezaji wa kushona mavazi hauna gharama kubwa ikilinganishwa na kuendesha kiwanda, Tanzania inatakiwa kubadilika na kuelekea huko hasa zama hizi za corona ambazo zinafunga milango na China na mataifa mengine ya Asia yenye uzalishaji mkubwa.

Kama viwanda hivyo vya EPZ vinavyofanya ni somo kuwa huu ni uwekezaji unaoweza kufanywa na wafanyabiashara na wajasiriamali nchini ambao wanaamua kuingia kwenye kutengeneza mavazi.

Ni wakati wa kutafakari na kuchukua hatua.

**KABWELA** NA FADHILI MOHAMMED



# Kiwanda kuunganisha magari kuanza sasa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angella Kairuki, amekutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Scania, Lars Eklund, ambaye ameahidi kujenga kiwanda cha kuunganisha magari nchini.

Akizungumza na wanahabari jijini Dar es Salaam, Waziri Kairuki alisema kampuni ya Scania kutoka Sweden ni wazalishaji na waundaji wakubwa wa magari ya biashara hasa malori na mabasi.

"Kujengwa kwa kiwanda hicho utakuwa ni uwekezaji mkubwa wa kampuni ya Scania nchini. Kwa upande wetu tutaendelea kuboresha mazingira ya biashara ili kuvutia mitaji na uwekezaji zaidi," alisema.

Waziri Kairuki alisema mazingira mazuri ya kiuwekezaji yaliyopo kwa sasa Tanzania yamekuwa kivutio kikubwa kwa wawekezaji, hivyo kuwavutia wengi kuwekeza mitaji yao.

"Serikali imeazimia kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025. Na jukumu letu kama wizara tukishirikiana na Kituo cha Uwekezaji (TIC) ni kuendelea kuweka mazingira mazuri na kuonesha fursa na vivutio vya uwekezaji vilizopo hapa nchini," alisema Waziri Kairuki.

Aidha, Waziri Kairuki alimshukuru Eklund na kampuni yake kwa imani iliyonayo kwa Tanzania ambapo imeshachukua hatua mbalimbali ikiwamo kuondoa vikwazo vilivyokuwa vinakwamisha maendeleo na ustawi wa biashara na uwekezaji nchini.

"Tunaishukuru na kuipongeza kampuni ya Scania kwa kuleta mradi huo Tanzania kwani utatoa mchango mkubwa katika suala la ajira na pia kuchochea ukuaji wa mapato ya serikali kupitia kodi," alisema.

Kairuki na kuongeza kuwa ujenzi wa mradi huo utakapoanza serikali itatoa ushirikiano mkubwa.

Eklund alimweleza Kairuki kuwa uamuzi wa kujengwa kwa kiwanda hicho Tanzania umetokana na mazingira mazuri ya uwekezaji pamoja na upatikanaji wa gesi asilia ambayo ni rasilimali muhimu katika uendeshaji wa mabasi yanayotumia nishati ya dizeli au gesi ya CNG.

"Mbali ya mazingira mazuri ya kiuwekezaji yaliyopo Tanzania, mabasi ya Scania yanatumia gesi, hivyo kuja kuwekeza Tanzania ni kwa sababu kumekuwa na upatikanaji mkubwa wa gesi asilia, ambayo tumekuwa tukiitumia kama nishati ya kuendeshea magari yetu," alisema Eklund.

Kwa mujibu wa Eklund, kumekuwa na uhitaji mkubwa wa magari ya Scania ambayo yamekuwa yakitumika kwa usafirishaji wa abiria na mizigo na hasa katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Avemaria Semakafu (kulia), na msafara wake wakipata maelezo kuhusu kazi anazofanya roboti ajulikanaye kwa jina la Pepper kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa Vodacom Tanzania, Jaquiline Materu (kushoto), alipotembelea banda la kampuni hiyo, katika maonyesho ya mashindano ya sayansi, teknolojia na ubunifu yaliyoandaliwa na wizara hiyo, kwenye Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**


IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM AT KISUTU

CIVIL CASE NO. 73 OF 2019

HELIMAN WORLD WIDE LOGISTICS (T) LIMITED……..PLAINTIFF

VERSUS

DAVE IMPEX LIMITED…………………DEFENDANT

**SUMMONS TO APPEAR FOR JUDGMENT**

TO: THE MANAGING DIRECTOR
DAVE IMPEX LIMITED ANY WHERE YOU ARE
P.O. Box 7377
PLOT 67 R. KURASINI
DAR ES SALAAM.

**WHEREAS** the above case has arranged for judgment on 23/03/2020 at 11.00am a suit against you at Kisutu Resident Magistrate's court the facts of which may be found on request in the court file.

**AND FURTHER TAKE NOTICE** that if you default in appear the court will inter Judgment on your absence.

**Given** under my Hand and Seal of court this **10th day of FEBRUARY, 2020.**

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE
KISUTU – DAR ES SALAAM

215672202


# Kilimo cha umwagiliaji chaongezeka Mbeya

**Na Mwandishi Wetu, MBEYA**

UBORESHAJI wa miundombinu ya umwagiliaji mkoani Mbeya imeongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta 49,117 mwaka 2018 hadi kufikia hekta 71,890 mwezi Machi 2020.

Akizungumza ofisini kwake Mhandisi wa Umwagiliaji mkoani Mbeya, Elibariki Mwendo, alisema uboreshwaji wa miundombinu hiyo umefanyika katika skimu za Mbaka na Katelantaba (Busokelo), Uturo, Gwiri, Igomelo, Mwendamtitu (Mbarali) na Mshewe (Mbeya Vijiji).

Mhandisi Mwendo amesema baada ya uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji kwa sasa eneo la umwagiliaji katika skimu ya Mbaka ni hekta 500, na Katelantaba eneo la umwagiliaji ni hekta 250, wakati katika skimu ya Uturo eneo linalomwagiliwa ni hekta 900.

Alisema katika skimu ya Gwiri eneo linalomwagiliwa ni hekta 400, Igomelo ni hekta 312 wakati skimu ya Mwendamtitu ina eneo la umwagiliaji hekta 30,00l na Mshewe Wilaya ya Mbeya Vijijini ina eneo la hekta 250.

Mhandisi Mwendo alisema kutokana na uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji mkoani Mbeya, uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji umeimarisha kilimo cha umwagiliaji ambacho ndio kilimo cha uhakika, uzalishaji wa mazao ya chakula kama mpunga, mahindi na mboga umeongezeka na kuinua kipato cha familia, wilaya, mkoa na taifa.

Alisema serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha skimu za umwagiliaji ili kuhakikisha skimu hizo zinazalisha mazao ya chakula matunda na mboga kwa mwaka mzima na hivyo kuwa na usalama wa chakula nchini.

Ofisa Kilimo Mwandamizi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji mkoani Mbeya, Mnadi Taribo, amesema Tume imeendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa wakulima kama kilimo shadidi cha mpunga, ambacho hutumia maji kidogo na uzalishaji wa mpunga unakuwa mara mbili zaidi ikilinganishwa na kilimo kinachotumia maji mengi.

Akitoa mfano Taribo alisema katika skimu ya umwagiliaji ya Madibira uzalishaji wa mpunga kwa kilimo cha kawaida (maji mengi) hutoa tani 7.2 kwa hekta wakati kilimo shadidi (maji kidogo) huzalisha tani 9 .3 kwa hekta.

Skimu ya umwagiliaji ya Uturo uzalishji wa mpunga kwa kilimo cha kawaida ni tani 5.7 kwa hekta wakati kilimo shadidi huzalisha tani 13 kwa hekta.

Alisema kilimo shadidi kinatumia maji kidogo kwa chini ya asilimia 50 ikilinganishwa na kilimo cha kawaida na uzalishaji wake ni mkubwa na kuwa na matumizi bora ya rasilimali maji.

**Mhandisi Mwendo alisema kutokana na uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji mkoani Mbeya, uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji umeimarisha kilimo cha umwagiliaji ambacho ndio kilimo cha uhakika, uzalishaji wa mazao ya chakula kama mpunga, mahindi na mboga umeongezeka na kuinua kipato cha familia, wilaya, mkoa na taifa.**

HABARI KITAIFA

# Mil. 90/- zajenga machinjio ya kuku

**Na Yasmine Protace**

HALMASHAURI ya Manispaa ya Ubungo, jijini Dar es Salaam, imetumia zaidi ya shilingi milioni 90 kwa ajili ya kujenga machinjio ya kuku katika soko la Mabibo.

Hayo yalisemwa na Diwani wa Kata ya Mabibo, Kassim Lema, katika maadhimisho ya Siku ya Wanamke Duniani, ambapo Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) kwa kushirikiana na vituo vya Taarifa na Maarifa vya Wilaya ya Ubungo vilishirikiana kuandaa maadhimisho hayo.

Diwani Lema ambaye ilikuwa ni mmoja wa wageni waalikwa alitoa taarifa ya ujenzi wa sehemu ya machinjio, baada ya washiriki katika maadhimisho hayo kulalamika machinjio ya kuku katika soko la Manzese kuwa halifai kuendelea kutumika kuchinjia kutokana na kutofaa na kusababisha kuku kuchinjwa ovyo.

Amina Juma, alisema kuwa soko la machinjio ya kuku Manzese ni baya na halifai kuchinjiwa kuku, na kwamba wanaomba halmashauri kuwajenga ili kuku wachinjiwe katika maeneo yanayofaa.

Lema akijibu kero ya machinjio ya kuku, alisema kuwa Halmashauri ya Ubungo inatumia zaidi ya shilingi milioni 90, kwa ajili ya kujengea soko la machinjio ya kuku Manzese.

"Machinjio ya kuku Manzese hayaridhishi kutokana na kuku kuchinjwa katika machinjio isiyofaa, hivyo halmashauri imetoa zaidi ya shilingi milioni 90 na sasa machinjio imejengwa," alisema.

Aliongeza kuwa machinjio hayo, yatatumika muda wote kutokana na ujenzi wake kupiga hatua kubwa.

# Serikali yaombwa umakini corona mikoa ya mipakani

**Na Pendo Thomas, KIGOMA**

VIONGOZI Baraza la Makanisa ya Kipentekoste Tanzania Mkoa wa Kigoma (CPCT), wameomba serikali kuongeza umakini kwenye mikoa inayopakana na nchi zilizogundulika kuwa na wagonjwa wa corona kwa kutoa elimu ya ugonjwa huo ili kusaidiana na serikali kudhibiti njia rasmi na zisizo rasmi.

Wakitoa risala yao Jumapili iliyopita katika maombi maalumu ya kumwomba Mungu aiepushe nchi ya Tanzania na ugonjwa wa corona na kuombea Watanzania walioko nchini China, Askofu mstaafu PAGT Jimbo la Kigoma Maiko Kulwa, alisema serikali itumie njia mbalimbali kuwafikia wananchi wa maeneo ya vijiji vilivyo mipakani ili watambue namna bora ya kujikinga na kutoa taarifa endapo atabainika mtu mwenye ugonjwa huo.

"Pamoja na maombi yetu kwa Tanzania na dunia, tunatoa ushauri kwa serikali na vyombo vinavyohusika kuwe na ukaguzi makini unaohusisha wananchi kudhibiti njia rasmi na zisizo rasmi na kuhakikisha vifaa vya kusaidia kugundua maambukizi vinafika kwa wakati," alisema.

Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji, Dk. Vedastus Makota, akiongea kwa niaba ya Katibu Tawala mkoa wa Kigoma, Rashid Mchata, alisema kuna vipimo vitano vya kusaidia utambuzi wa ugonjwa huo ambavyo viwili vimewekwa katika kiwanja cha ndege na vitatu vimewekwa maeneo ya mipakani.

Makota alisema wameanza kuchukua tahadhali mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuzitaka taasisi za dini kupunguza baadhi ya taratibu za ibada zinazo walazimu kugusana pamoja na kuagiza kuwekwa maji tiririka katika maeneo yao ili waumini wanawe mikono kabla ya kuanza ibada.

Mganga Mkuu Mkoa wa Kigoma, Simon Chacha, alisema wananchi wanapaswa kufuata maelekezo wanaoyopewa na wataalamu wa afya kuchukua tahadhari kwa kuepukana tabia zote hatarishi zinazo sababisha maambukizi hayo.

"Niwatake fuateni ushauri wa wataalamu wa afya kwa sababu huko kwenye mitandao kumekuwa na upotoshaji wa ugonjwa huu wengine wanasema unaambukizwa kwa jasho, ugonjwa huu unaenea kupitia majimaji yanayotoka katika njia za hewa, makamasi, kikohozi na mate," alisema.

Aliwataka wananchi kutokueneza taarifa za uwepo wa watu wenye dalili za ugonjwa huo katika mitandao ya kijamii kwa kuwa inaweza kuleta taharuki badala yake watumie vyema namba za simu za bure zilizotolewa na serikali kwa ajili ya kutoa taarifa kama atabainika kuwapo mtu mwenye viashiria vya ugonjwa huo.



Mafundi ujenzi wakiweka saruji tayari kwa ajili ya kuweka lami katika barabara ya Sinza Shekilango, jijini Dar es Salaam juzi.
**PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wakaguzi wataka upungufu wa watumishi h/shauri kutatuliwa

**Na Restuta Damian, BUKOBA**

WAKAGUZI wa ndani wa halmashauri za wilaya mkoani Kagera wameomba serikali kutatua changamoto ya upungufu wa watumishi, usafiri na kupatiwa elimu ya utambuzi wa mfumo mpya wa ukusanyaji wa mapato kwa njia ya Tehama.

Maombi hayo yametokana na kutofanya kazi kwa ufanisi kwani maeneo yanayofikiwa katika kufanya ufuatiliaji wa usimamizi na ukaguzi wa vyanzo vya mapato ni machache.

Walitoa ombi hilo wakati wakizungumza na Nipashe katika kikao cha kuwajengea uwezo kutambua ukaguzi sehemu ambayo mifumo ya taarifa hupatikana kuanzia vijijini hadi maeneo ya miji.

Iman Mgonja, mkaguzi wa ndani katika Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi, alisema upungufu wa watumishi kwenye kitengo hicho unakwamisha kufanya kazi kwa ufanisi wakati serikali inahitaji mapato ili kuweka miundombinu imara.

Mgonja alisema, kwenye halmashauri kuna miradi mikubwa na midogo ambayo vyanzo hutofautiana katika tozo kwa halmashauri na maeneo ya kufikia kuangalia mienendo ni changamoto ya magari.

"Halmashauri yetu ya Missenyi tuna chanzo kikubwa cha mpaka wa Mtukula unaingiza na kutoa mazao, kiwanda cha sukari Kagera Sugar pamoja na nyanzo vidogo vidogo inavyopatikana vijiji na maeneo yalichangamka," alisema Mgonja.

Revocatus Manyerere, mkaguzi wa ndani Halmashauri ya Wilaya Muleba, alisema kitengo hicho hutegemea kuomba gari kutoka idara nyingi ili kufanya kazi kwa wakati.

Alisema licha ya kutokuwa na magari pia watumishi ni wachache ikilinganishwa na nyanzo vya mapato vinavyotegemewa ambavyo ni mazao ya samaki, kilimo na misitu.

Ofisa usimamizi mwandamizi wa fedha katika sekretalieti ya mkoa, Pius Ngaiza, alisema changamoto hizo inasababisha kushindwa kutambua uwezo wa vyanzo katika makusanyo, kwani linakuwa tatizo upande wa watumishi na magari.

Ngaiza alisema serikali imebadili njia ya ukusanyaji na kuweka mifumo ya Tehama ambayo inafungwa kwenye afya, elimu hali ambayo itasaidia kutambua idadi ya mapato. Alisema mkoa mzima unawatumishi 17 ambao wamegawanywa kwa kila halmashauri ikiwa uhitaji ni 31 njia zinazotumika nikusaidiana na watendaji kusimamia mapato.

Mkuu wa mkoa huo, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, alisema kupitia kikao hicho yatafanyika mabadiliko katika ukusanyaji wa mapato kwa njia rasmi.

Aliongeza kuwa kwa kipindi kirefu hapakuwapo na ubunifu wa miradi mikubwa, hali iliyosababisha kutegemea fedha za serikali kuu kwa kuona kuwa taifa lina miradi mingi ya kutafuta fedha kufanya shughuli za maendeleo.

# Shuwasa yahofia kukwama ukusanyaji mapato ya mil. 700/-

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

MAMLAKA ya Maji na Usafi wa Mazingira Shinyanga (Shuwasa), imeingiwa na hofu ya kushindwa kutekeleza agizo la Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa la ukasanyaji wa mapato ya Sh. milioni 700 kwa mwezi.

Hofu hiyo inatokana na mabomba kupasuka mara kwa mara, na kusababisha ukosefu wa huduma ya maji kwa wananchi na viwanda.

Hayo yalibainishwa juzi na Mkurugenzi wa Shuwasa, Flaviana Kifizi, wakati akizungumza na wahabari alipokwenda kukagua bomba la maji ambalo lilipasuka katika eneo la Masekelo jirani na mto Kidalu na kulifanyia matengenezo, kuwa upasukaji wa mabomba ovyo unawakosesha mapato.

Alisema Waziri Mbarawa alipokuwa mkoani Shinyanga Januari mwaka huu, wakati akivunja bodi ya zamani ya maji ya mamlaka hiyo na kuzindua mpya, alitoa maagizo kuwa kila mwezi wanapaswa kukusanya Sh. milioni 700, na kubainisha mabomba hayo yakiendelea kupasuka huenda agizo hilo likagonga mwamba.

"Tatizo la upasukaji wa mabomba haya ya maji mara kwa mara mamlaka imekuwa ikiingia hasara ya kufanya matengenezo, pamoja na kukosa mapato kwa sababu huduma za maji zinasitishwa kwa wananchi pamoja na viwanda ambavyo ndio vina matumizi makubwa ya maji," alisema Kifizi.

"Kutokana na kupasuka kwa mabomba haya na kutukosesha mapato, tumeanza kuingiwa na hofu ya kushindwa kutekeleza agizo la Waziri Mbarawa, la kukusanya mapato Sh. milioni 700 kwa mwezi, kwa sababu huduma zimekuwa za kusuasua mabomba yanapasuka" aliongeza.

Aidha, alibainisha kuwa sababu za mabomba kupasuka mara kwa mara ni wananchi kupunguza matumizi ya maji na kutumia maji ya mvua, hali ambayo inasababisha mabomba kuzidiwa kutunza maji na hatimaye kupasuka.

Alifafanua zaidi kuwa kazi ya mabomba ni kusambaza maji na siyo kuyatunza.

Mmoja wa wakazi wa Shinyanga, Estomine Henry, alieleza kusikitishwa na ukosefu wa huduma za maji mara kutokana na mabomba kupasuka, na kuiomba mamlaka hiyo ijitahidi kufanya ukaguzi wa mabomba ili yasiendelee kupasuka.

## Shule zapigwa jeki vifaa vya mil. 15/-

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE za Sekondari Kibamba, Kinzudi na Shule ya Msingi Makuburi Jeshini, zilizoko wilayani Ubungo jijini Dar es Salaam, zimepewa msaada wa vifaa mbalimbali.

Msaada huo umetolewa na kukabidhiwa na Benki ya NMB, ambao umejumuisha viti, meza na madawati vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 15.

Hafla ya kukabidhi msaada huo ilifanyika jana katika viwanja vya Shule ya Sekondari Kibamba, ambako Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Badru Idd, alimkabidhi msaada huo Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kisare Makori.

Akizungumzia mgawanyo wa misaada hiyo, Badru alisema Shule ya Sekondari Kibamba na Kinzudi kwa pamoja zimepewa viti 100 na meza 100 (sawa na viti 50 na meza 50 kwa kila moja), huku Shule ya Msingi Makuburi Jeshini, ikipewa madawati 100.

Alibainisha kuwa, benki yake imekuwa na utaratibu wa kusaidia jamii kupitia Programu ya Uwajibikaji kwa Jamii, ambayo imetumika kwa karibu miaka 10 sasa, ikitoa usaidizi wa utatuzi wa changamoto katika sekta za elimu, afya na majanga.

"Ni utamaduni tulioufanya kwa karibu miaka 10 sasa, lengo likiwa ni kurejesha kwa jamii sehemu ya faida yetu ya kila mwaka, lakini utaratibu huu unalenga kuunga mkono juhudi za serikali katika kuboresha sekta hizo na kuleta matokeo chanya," alisema Badru.

Aliwataka wanafunzi wa shule za Kibamba, Kinzudi na Makuburi Jeshini, kutunza vifaa hivyo, ili viweze kutumika kwa muda mrefu na kusaidia wanafunzi wa shule hizo watakaotumia kuepukana na adha za kusoma wakiwa sakafuni.

Akitoa neno la shukrani baada ya kupokea vifaa hivyo, DC Makori aliishukuru NMB kwa namna inavyoshikamana sekta za elimu na afya wilayani mwake na kwamba kwa niaba ya serikali, wanatambua na kuthamini mchango wa benki hiyo.

"Kwa hakika NMB ni wadau muhimu wa sekta ya elimu na afya wilayani Ubungo, mmetusaidia mara kadhaa na tunawaomba msituchoke, tena muendelee kufanya hivyo kila tutakapowakimbilia, ili kusaidia pale serikali inapoishia katika shule, zahanati na vituo vya afya," alisema Makori.

Aliwataka wadau zaidi wa elimu kujitosa kusaidia utatuzi wa changamoto za sekta hiyo wilayani mwake kama inavyofanya NMB.

Mkuu wa Sekondari ya Kibamba, Natujwa Mrinde, kwa niaba ya wakuu wa shule zilizosaidiwa, aliishukuru benki hiyo na kuiahidi kuvitunza vifaa hivyo.

Alisema Kibamba Sekondari yenye wanafunzi 1,365, ilikuwa na changamoto ya uhaba wa viti na meza na kwamba saada wa NMB unaenda kupunguza kwa kiasi fulani adha ya wanafunzi kusoma katika mazingira yasiyo rafiki.

Naye Ofisa Elimu (Sekondari) Wilaya ya Ubungo, Hilda Shalanda, alisema kinachofanywa na NMB katika wilaya yake kwenye sekta ya elimu, ni kitu cha kupongezwa na kinachopaswa kuungwa mkono na wadau wengine kwa kuzifikia shule mbalimbali zenye uhitaji.




Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Dar es Salaam na Zanzibar, Badru Idd (kushoto), akikabidhi msaada wa madawati, viti na meza 150 vyenye thamani ya Sh. milioni 15, kwa Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kisare Makori, jijini Dar es Salaam, kwa ajili kuzisaidia shule tatu za Manispaa ya Ubungo ambazo ni sekondari za Kibamba na Kinzudi na Shule ya Msingi Makuburi Jeshini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Taasisi zatakiwa kusaidia wanawake

**Na Shaban Njia, SHINYANGA**

TAASISI mbalimbali nchini zimetakiwa kuendelea kuwekeza nguvu katika kusaidia kutatua changamoto zinazowakabili wanawake na kuwakwamisha kusonga mbele kimaendeleo.

Akizungumza na waandishi wa habari katika uzinduzi wa vyoo vilivyofanyiwa maboresho, meneja wa kampuni ya kutengeneza vyoo ya Sato, Justin Mbowe, alisema wanajisikia furaha kusherehekea Siku ya Wanawake ikiwa ni miaka 25 toka azimio la Beijing, ili kuhamasisha mabadiliko chanya.

Mbowe alisema wanawake ni nguzo katika jamii na kampuni ya Sato limejizatiti kumsaidia mtoto wa kike ili awe mwanamke wa nguvu katika jamii inayomzunguka na kufanikiwa kujisimamia katika kujitafutia na kujipita maendeleo yake.

Aidha, alisema katika sherehe za mwaka huu kampuni hiyo imeamua kushiriki ujenzi wa vyoo bora kwa ajili ya wasichana wa eneo la Segerea jijini Dar es Salaam ili kutatua changamoto ya kuwa na vyoo bora katika maeneo ya umma.

Aidha, alisema uhamasishaji wa kampeni ya kitaifa ya ujenzi wa vyoo bora Sato ilitembelea mikoa yote ya kanda ya ziwa na kutoa elimu ya umuhimu wa vyoo bora na nafuu kwa wananchi wa maeneo hayo.

Naye Daktari Msaidizi wa Mkoa wa Dar es Salaam Dk. Ayubu Kibao, alilishukuru shirika hilo kwa kutoa mchango mkubwa kwa watoto wa kike na kwamba wamejipanga kusimamia kwa karibu afya na usafi wa mazingira kuhakikisha kaya zinatumia vyoo bora.

Kampuni ya utengenezaji ya vyoo ya Sato imetoa vyoo 80,000 kwa shule za msingi katika kusherehekea Siku ya Mwanamke Duniani iliyofanyika Machi 08, mwaka huu.

# TZ mwenyeji mkutano hifadhi za urithi jiolojia

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

TANZANIA inatarajiwa kuwa mwenyeji wa mkutano wa kwanza wa kimataifa wa Hifadhi za Urithi wa Jiolojia katika Bara la Afrika.

Akizungumza na waandishi wa habari Kamishna wa Uhifadhi wa Mamlaka ya Ngorongoro (NCAA), Dk. Freddy Manongi, alisema mkutano huo utafanyika jijini Arusha, Mei 18 hadi 23, mwaka huu.

"Mkutano huu utawashirikisha wataalamu kutoka nchi mbalimbali na utafanyika Arusha kwa mara ya kwanza katika Bara la Afrika, baada ya Hifadhi ya Urithi wa Jiolojia ya Ngorongoro- Lengai kuwa hifadhi ya kwanza na ya kipekee kupatikana Afrika ikiwa ni Kusini mwa Jangwa la Sahara," alisema.

Alisema mkutano huo, utagawanyika katika sehemu kuu mbili; sehemu ya kwanza ni kongamano litakaloanza Mei 18 hadi 20 mwaka huu, na litakuwa na mada za kitaalamu zitakazotolewa na viongozi wa Shirika la Elimu ya Sayansi na Utamaduni wa Umoja wa Mataifa (Unesco) Global Geopark zilizofanikiwa katika mabara yote duniani, zikiwasilisha uzoefu wa kutambua vivutio vya kijiolojia, kuvihifadhi, kuvifanya rasilimali za kiutalii pamoja na namna ya kuvitumia kwa manufaa endelevu ya jamii.

Alitaja sehemu ya pili ya mkutano huo, ni washiriki wa mkutano kutembelea hifadhi za Jiolojia ya Ngorongoro-Lengai ili kuona uhalisia wa mawasiliano na kujifunza kwa vitendo.

"Lengo la mkutano huu wa siku sita ni kutoa mafunzo, kubadilishana uzoefu pamoja na kuchochea uanzishwaji na uendeshaji wa hifadhi wa maeneo ya urithi wa jiolojia, ambayo yatakuwa ni kivutio kipya cha kuongeza idadi ya watalii hapa nchini," alisema.

Hata hivyo, alisema hadi kufikia mwanzoni mwa mwaka huu kwa dunia nzima kulikuwa na jumla ya hifadhi za kijiolojia 147, kutoka mataifa 41 na kati ya hizo ni hifadhi mbili pekee zilipatikana katika Bara la Afrika ikiwamo ya Ngorongoro-Lengai pamoja na M'goun iliyopo nchini Morocco.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, alisema utalii wa miamba utakuwa ni fursa kubwa ya Tanzania kuongeza idadi ya watalii kutoka milioni 1.5 hadi kufikia milioni 10 kama walivyoelezwa.

"Hii ni fursa ya kipekee ambayo tumeipata katika nchi yetu tunatakiwa kuitumia vizuri ili tutangaze vivutio hivi adhimu vya urithi wa jiolojia (utalii wa miamba) ili tufikie malengo tuliyojiwekea ya kuongeza idadi ya watalii kufikia milioni 10," alisema.

Alisema kipindi chote cha mkutano huo serikali itaimarisha usalama katika Mkoa wa Arusha ili washiriki wa mkutano huo wawe katika hali ya utulivu," alisema.

Mkutano huo utaandaliwa na NCAA kwa kushirikiana na Mtandao wa Hifadhi za Urithi wa Jiolojia Duniani(Global Geopark Nertwork), Unesco.

## Mzumbe waingia makubaliano kujenga sekondari

**Na Allan Isack, ARUMERU**

CHUO Kikuu cha Mzumbe, kimeingia makubaliano na wananchi wa Kijiji cha Kiseriani, Kata ya Mlangarini Halmashauri ya Arusha DC, wilayani Arumeru, kuanzisha ujenzi wa shule mpya ya sekondari Kiseriani.

Katika makubaliano hayo, Chuo Kikuu cha Mzumbe kitajenga vyumba vinne vya madarasa, ofisi za walimu na vyoo.

Wadau hao wamejitokeza kuchangia sekta ya elimu, katika Halmashauri ya Arusha DC, kwa lengo la kuboresha na kuweka mazingira rafiki ya kufundishia kwa walimu na kusomea kwa wanafunzi darasani.

Ujenzi wa shule hiyo unafuatia sera ya serikali ya kuboresha sekta ya elimu na kutoa elimu bila malipo.

Ujenzi wa miundombinu hiyo, utagharimu Sh. milioni 150.

Fedha hizo zimezotolewa na Chuo Kikuu cha Mzumbe kama fidia ya shamba lililotolewa na Kijiji cha Kiseriani kwa chuo kikuu hicho.

Ofisa Elimu Sekondari Halmashauri ya Arusha DC, Medad Lupenza, ameupongeza uongozi wa chuo hicho na Kijiji cha Kiseriani, kwa kufanya makubaliano hayo muhimu kwa ajili ya sekta ya elimu.

Alisema makubaliano hayo yameleta mapinduzi kielimu katika eneo ambalo awali halikuwahi kuwa na shule ya sekondari.

Hata hivyo, alisema watoto wa Kijiji cha Kiseriani, walikuwa wakitembea zaidi ya kilomita 10, kufuata huduma ya shule ya sekondari.

Alisema, halmashauri hiyo imeanza mchakato wa awali wa kusajili shule hiyo.

Wananchi wa kijiji hicho pia wameanza ujenzi wa maabara ya masomo ya sayansi ili kukidhi vigezo vya shule kusajiliwa.



Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU) Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Anna Mbise (kulia), akizungumza baada ya wajumbe wa chama hicho kukabidhi sabuni kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu wa Kijiji cha Irkujit Kata ya Edonyongijape, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wanawake walia mfumo dume kumiliki mali

**Na Allan Isack, BABATI**

WANAWAKE wa vijiji vinne vya Wilaya ya Babati mkoani Manyara, wamesema kuwa mila na desturi zinazokumbatiwa na wanaume ni kikwazo kwao kupata haki ya kumiliki ardhi katika jamii.

Walisema hayo wakati mafunzo ya haki ya kumiliki ardhi katika jamii yaliyoandaliwa na Shirika lisilo la kiserikali Cosita.

Walihudhuria katika mafunzo hayo kuwajengea uwezo kutoka katika vijiji vya Kiongozi, Malangi, Chemchem na Mtuka.

Mwanaidi Ramadhan, mkazi wa Kijiji cha Kiongozi, alisema baada ya kupata mafunzo hayo, yatawabadilisha na watakwenda kutoa elimu kwa wanawake wengine katika jamii.

Alisema kwa kipindi kirefu wanaume wanawaonea wanawake, lakini baada ya kupata mafunzo hayo watakwenda kutafuta mabadiliko katika jamii.

Philomena Homa kutoka kijiji cha Chemchem alisema elimu waliyoipata itawasaidia kuongeza ari ya kwenda kudai haki zao za kumiliki ardhi na mali katika jamii.

Homa alisema iwapo watapata ardhi itawasaidia kuinuka kiuchumi kwa kuwa wataitumia kufanya uzalishaji wa mali na watachangia shughuli za kimaendeleo katika jamii.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Cosita, Patrice Gwasma, alisema wanatekeleza mradi wa haki za ardhi kwa wanawake na mradi huo unafadhiliwa na Shirika la Foundation for Civil Society (FCS).

Alisema kwa mujibu wa utafti wa Kamisheni ya Umoja wa Mataifa wa mwaka 2012/15 kwa kishirikiana na Shirika la Sweden (SIDA), kwa pamoja walibaini asilimia 20 ya wanawake duniani ndiyo wanamiliki ardhi.

Alisema asilimia 80 ya wanawake duniani hawamiliki ardhi, hivyo ameitaka jamii kubadilika na kutoa elimu ili wanawake na wanaume wote wawe na haki sawa ya umiliki wa ardhi.

Alitoa elimu ili waitumie elimu hiyo kwa ajili ya kuwatetea watoto wao.

Naye Mratibu wa Mradi wa Haki za Ardhi kwa wanawake, Paulo John, alisema vyanzo vya migogoro katika jamii ni wananchi kutokufahamu Sheria za Ardhi.

Alisema mwanamke ana haki ya kumiliki ardhi kwa mujibu wa sheria namba nne na tano ya mwaka 1999, kifungu cha 3(2) na kifungu hicho kinampa haki mwanamke ya kumiliki, kutumia na kuuza au kuigawa ardhi sawa na haki aliyonayo mwanaume.



# Ujenzi maabara kisasa wakamilika kwa 80%

**Na Godfrey Mushi, SIHA**

MAABARA kubwa ya kisasa na ya kwanza kwa nchi za Afrika Mashariki ambayo inajengwa katika hospitali ya taifa ya magonjwa ambukizi ya Kibong'oto, imekamilika kwa zaidi ya asilimia 80.

Kukamilika kwa maabara hiyo kinatajwa kutalisaidia taifa kukabiliana na magonjwa ambukizi ya kifua kikuu, kifua kikuu sugu, virusi vya corona vinavyodaiwa kusababisha homa ya mafua na tishio la ugonjwa wa ebola.

Hayo yamo katika taarifa ya Kaimu Mkurugenzi wa Hospitali ya Taifa ya Magonjwa ambukizi ya Kibong'oto, Dk. Donatus Sere aliyoitoa jana kwa maofisa wa Wizara ya Afya, maofisa habari na timu ya wanahabari kutoka vyombo mbalimbali.

"Hivi sasa tuko mbioni kuanza kuitumia maabara hii ambayo imebaki kidogo kumalizika. Tumepata vifaa vya kisasa vya kuchunguza na kuja na majibu ya magonjwa yanayotokana na mfumo wa hewa. Hapa magonjwa kama kifua kikuu na kifua kikuu sugu ni tatizo kubwa ambalo linawasumbua wananchi walio wengi," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Sere, kifua kikuu kimekuwa kikiongezeka nchini kutokana na mfumo wa maisha ya watu hasa wanaoishi vijijini.

Alisema maabara hiyo ya kisasa inayojengwa kwa gharama ya shilingi bilioni nane, inatasaidia kupambana na magonjwa hayo ambukizi na tishio duniani.

Idadi kubwa ya wagonjwa wanaofikishwa hospitalini hapo ni wachimbaji wa madini katika migodi mbalimbali nchini.

Aidha, alisema mikoa inayotishiwa na idadi kubwa ya wagonjwa hao ni Dar es Salaam, Geita, Mwanza na Mara.

Kwa nyakati tofauti, baadhi ya wagonjwa waliolazwa hospitalini hapo, Thdeus Joseph na Emanuel James, wameeleza kuridhishwa kwao na huduma zinazotolewa na hospitali hiyo.

**"Hivi sasa tuko mbioni kuanza kuitumia maabara hii ambayo imebaki kidogo kumalizika. Tumepata vifaa vya kisasa vya kuchunguza na kuja na majibu ya magonjwa yanayotokana na mfumo wa hewa. Hapa magonjwa kama kifua kikuu na kifua kikuu sugu ni tatizo kubwa ambalo linawasumbua wananchi walio wengi," alisema.**

# Corona yaahirisha mkutano mabingwa utafiti saratani

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

MKUTANO wa kimataifa wa wataalamu wa utafiti na mabingwa wa magonjwa ya saratani uliokuwa ufanyike kwa siku nne katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, umeahirishwa kwa muda usiojulikana.

Jana, Mkurugenzi wa Hospitali hiyo, Dk. Gileard Masenga, alisema mkutano huo uliokuwa uanze Aprili 4 mwaka huu, sasa umesogezwa mbele hadi hapo utakapotangazwa tena.

"Ni kweli tulikuwa na mkutano wa wataalamu na mabingwa wa saratani kutoka nchi mbalimbali duniani ambao walikuwa wanakuja nchini na hasa hapa KCMC katika warsha ya siku nne, lakini imebidi tuahirishe kwa sababu ya kukabiliana na maambukizi ya ugonjwa wa corona," alisema.

Ugonjwa huo unaosababishwa na kirusi jamii ya corona (Covid 19), ambacho ni tofauti na virusi vingine vya jamii hiyo ambavyo viliwahi kusababisha milipuko ya ugonjwa unaojulikana kama 'Sars-Cov' mwaka 2003 na Mers-Cov Corona Virus mwaka 2013.

Ugonjwa huo huambukizwa kwa njia ya hewa kwa kuingiwa na majimaji yenye virusi kutoka kwa mtu mmoja kwa njia ya kukohoa au kupiga chafya au kwa kugusa majimaji au makamasi kutoka kwa mgonjwa aliyethibitishwa kuwa na dalili za ugonjwa huo.

Dalili za ugonjwa huo, huanza kuonekana kati ya siku moja hadi 14 tangu kupata maambukizo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, Prof. Gilleard Masenga (wa pili kulia), akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) mjini Moshi mkoani Kilimanjaro jana, namna walivyojipanga kukabiliana na virusi vya corona. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# KCMC sasa yaweka utaratibu mpya kuhudumia wagonjwa

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda ya KCMC, imetangaza utaratibu mpya wa kuwahudumia wagonjwa wake kuanzia sasa, ambapo ndugu mmoja peke yake ndiye atakayepewa kitambulisho maalum ili kukabiliana na kasi ya maambukizi ya virusi vya corona.

Uamuzi huo umetangazwa jana ikiwa ni siku moja tangu, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, kutangza Tanzania kupata kisa cha kwanza cha mgonjwa wa corona.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Prof. Gileard Masenga, alisema uongozi wa hospitali hiyo umeona ni vyema wagonjwa na ndugu za wagonjwa kuwa na ndugu mmoja ambaye atakuwa akimtembelea mgonjwa au kumuuguza.

Prof. Masenga alikuwa akitoa taarifa kwa umma jana kuhusu ugonjwa wa virusi vya corona.

"Kwa wakati wote atakapokuwa hospitalini, ndugu huyo atapatiwa kitambulisho maalum, kwa sababu ndugu zaidi ya mmoja hataruhusiwa kumuhudumia mgonjwa kwa kipindi hiki.

"Vile vile kwa mgonjwa ambaye hatohitaji msaada wa ndugu wa karibu, tunapendekeza kuwa atumie simu kuwasiliana na ndugu na jamaa zake kuhusu mwenendo wa afya yake pindi akiwa hospitalini hapa."

Pia mkurugenzi huyo amewaomba wagonjwa wanaokwenda kliniki katika hospitali hiyo kuanza matibabu kwenda peke yao au kwa ndugu mmoja kwa yule aliyezidiwa au kuhitaji msaada zaidi.

Ugonjwa huo unaosababishwa na kirusi jamii ya corona (Covid 19), ambacho ni tofauti na virusi vingine vya jamii hiyo ambavyo viliwahi kusababisha milipuko ya ugonjwa unaojulikana kama 'Sars-Cov' mwaka 2003 na Mers-Cov corona virus mwaka 2013.

Ugonjwa huo huambukizwa kwa njia ya hewa kwa kuingiwa na majimaji yenye virusi kutoka kwa mtu mmoja kwa njia ya kukohoa au kupiga chafya au kwa kugusa majimaji au makamasi kutoka kwa mgonjwa aliyethibitishwa kuwa na dalili za ugonjwa huo.

Dalili za ugonjwa huo, huanza kuonekana kati ya siku moja hadi 14 tangu kupata maambukizo.



Ukurasa 15

**Wasichana vyuo vikuu wapata mbinu kupenya uchaguzi mkuu**

## Wanawake mmejipanga au mnasubiri kuteuliwa?



Ukurasa 14



Ukurasa 17

**Mke wa Makamu Rais awa Waziri wa Ulinzi Sudan Kusini**


# siasa

JUMATANO MACHI 18, 2020

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe





Ukurasa 18

**Uchaguzi Marekani kuweka historia ya rais kikongwe ?**

FUNZO LA CORONA

# Afrika ianze kujisimamia kiuchumi, isiiachie China kuifanyia kila kitu

**Na Gaudensia Mngumi**

ULE msemo kuwa karne ya 21 ilikuwa ya China kwa sababu iliibuka kuwa taifa kubwa duniani lenye nguvu za kiuchumi, lililokuwa na uwezo wa kufanya biashara na karibu dunia nzima.

Aidha, pia ina akiba kubwa ya fedha kwenye hazina ya taifa, hadi Januari 2020 inatajwa kuwa na akiba ya dola trilioni 3,399.9.

Leo, huenda upepo ukabadilika ukawa hizi ni zama za Afrika. Ikimaanisha kuwa kwa kila jambo lolote baya yakiwamo maradhi ya corona inayohatarisha afya za watu, hatima ya uzalishaji wa huduma na bidhaa na kuwa kitisho cha kuangusha uchumi duniani, Afrika ikijizatiti inaweza kubadili kibao na kuandika historia mpya kwenye maendeleo yake.

Wataalamu wa uchumi wa-

**INAENDELEA UK.16**



Profesa Wangwe akitoa muhadhara wa masuala ya kiuchumi. **PICHA: MTANDAO.**

**Mfumo ACT-Wazalendo kitendawili cha kikatiba, uchaguzi mkuu** Ukurasa 19




Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wanawake Chadema Kanda ya Kaskazini. Vyombo vya wanawake vinawajibu wa kuwahamasisha kuwania ubunge majimboni badala ya kusubiri kuteuliwa. **PICHA: MTANDAO**

# Wanawake mmejipanga au mnasubiri kuteuliwa?

**Na Reubeni Lumbagala**

MWEZI huu ni wanawake na kwa kutambua umuhimu wa mwanamke duniani, Umoja wa Mataifa (UN), umepanga Machi 8, kila mwaka kuwa Siku ya Wanawake Duniani.

Ni siku muhimu ya kutambua, kuenzi na kuthamini umuhimu na mchango wa mwanawake katika juhudi za maendeleo.

Aidha, ni fursa ambayo dunia inapata darasa ili kufahamu mchango wa wanawake na namna katika nyakati tofauti tofauti wanawake wamesaidia kufikia malengo na maendeleo ya familia, jamii na taifa.

Ni waandishi wachache katika maandiko yao hasa vitabu wameonyesha mchango wa wanawake katika maendeleo ya kijamii, kiuchumi na hata kisiasa, hivyo, jamii ina uhitaji wa kuelimishwa mambo mazuri na ya kihistoria yaliyofanywa na wanawake ili kubadili mtazamo wa sasa kuhusu uwezo wa wanawake.

Moja ya matukio makubwa na muhimu katika nchi yetu kwa mwaka huu ni uwepo wa uchaguzi mkuu wa kuchagua madiwani, wabunge pamoja na rais unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba.

Ni uchaguzi ambao hufanyika mara moja katika kipindi cha miaka mitano kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

> Wakati wa uchaguzi hauko mbali ni vyema wanawake wakajipanga mapema kuanzia sasa, ili muda utakapofika waweze kushiriki kugombea.

Kwa kila nafasi hizo zipo sifa na vigezo ambavyo kwa yeyote aliyekidhi, anayo nafasi ya kuomba ridhaa kupitia chama chake cha siasa na mwishoe kwa wananchi ili aweze kutimiza malengo ya kuwatumikia wananchi. Wanawake ni kundi muhimu ambalo kama sehemu ya wanajamii, wanayo fursa ya kugombea nafasi mbalimbali ili kuweza kuwaongoza wengine na kutimiza matarajio ya wananchi kwa viongozi wao.

Makala haya ni maalum katika kuwakumbusha wanawake kuwa taifa linapoelekea kwenye uchaguzi mkuu wa mwezi Oktoba, 2020, wamejipanga vipi katika kugombea na hatimaye kushinda nafasi mbalimbali za uongozi? Je, katika vyama vya siasa kuanzia chama tawala hadi vyama vya upinzani, wanawake ambao ni "jeshi kubwa" wamejipanga kugombea au wameamua kuwa wasindikizaji tu?

Uwepo wa viti maalum nchini ni jitihada za kuwainua wanawake na kuongeza idadi ya wawakilishi katika uwanja wa siasa. Hivyo, wanawake wanapaswa kuacha kutegemea nafasi za viti maalum na zile nyingine za uteuzi zinazofanywa na Rais wa Tanzania.

Bado wanaume wameshikilia kata na majimbo mengi huku kukiwa na idadi ndogo ya wanawake katika nafasi hizo za udiwani na ubunge.

Wasichana na wanawake wamekuwa wakiathirika sana uwepo wa changamoto za kimaendeleo kama maji, afya, katika maeneo yao. Kwahiyo, njia mojawapo ya kutatua changamoto hizo ni wao wenyewe kujitokeza kuwania nafasi ili watakapokuwa viongozi waweze kuzishughulikia kero hizo kwa nguvu zao zote. Na mwanamke atakayeonyesha uwezo wa kiuongozi, wanawake wenzake wampe ushirikiano wa kutosha ili aweze kushinda nafasi anayogombea badala ya wanawake wenyewe kuwa mstari wa mbele kumbeza na kumkatisha tamaa.

Wakati wa uchaguzi hauko mbali ni vyema wanawake wakajipanga mapema kuanzia sasa, ili muda utakapofika waweze kushiriki kugombea.

Ni vyema wanawake wakafahamu kuwa nafasi za uteuzi si nafasi za kuweka uwiano sawa kati ya wanawake na wanaume, bali ni nafasi ambazo ili mtu akidhi vigezo vya kuteuliwa hutangulia sifa za msingi za uwezo wa mteuliwa wa kumudu majukumu atakayopewa na mamlaka za uteuzi.

Pia, nafasi za uteuzi zipo chache ambazo haziwezi kusawazisha uwiano na usawa wa kijinsia katika uongozi. Mwenye kukidhi vigezo vya uteuzi vilivyoainishwa ndiye huteuliwa bila kuzingatia jinsia yake. Wanawake wakigombea, wakashinda na mwishowe wakawa mfano wa kuigwa kiuongozi, wataongeza imani ya wananchi juu ya uwezo wa wanawake katika uongozi na katika masuala mengine ya kimaendeleo.

Ni matarajio yangu kuwa, wakati utakapowadia wa kuchukua fomu za kugombea nafasi mbalimbali za udiwani, ubunge na urais, wanawake watajitokeza kwa wingi kuchukua fomu hizo kwani huo ndiyo mwanzo wa kupata ridhaa ya kuchaguliwa na wananchi.

Na wakati wa kuomba kura utakapowadia, wanawake wasiombe kura za huruma kwa kutanguliza jinsia yao kama sifa ya msingi ya kuchaguliwa, bali waeleze uwezo na karama za kiuongozi walizonazo na namna watakavyoshiriki kuzitafutia ufumbuzi wa kudumu changamoto zinazowakabili wananchi.

Sambamba na hilo, ni lazima wanawake wenyewe kwa wenyewe wapendane na waone kuwa mafanikio ya mwanamke kushinda uchaguzi ni mafanikio ya wanawake wote. Hii ikijengeka miongoni mwa wanawake, itajenga ari na nguvu ya kusaidiana wanawake wenyewe kwa wenyewe ili kufikia mafanikio ya kushinda uchaguzi na kuwatumikia wananchi.

Kiu ya wananchi ni kupata viongozi wachapakazi, wazalendo, wenye ujasiri, uthubutu na hofu ya Mungu ili kuwatumikia wananchi wao. Nawatakia kila la kheri wanawake wote wenye nia ya kugombea katika uchaguzi mkuu.

Wanawake mpambane, muache kusubiri nafasi za viti maalum na uteuzi, kwani uwezo, nia, sababu za kuongoza mnazo. Wanawake mtafakari, mchukue hatua, hatimaye tuwaone kwa wingi kwenye mabaraza ya madiwani, bungeni na siku moja Ikulu.

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***

# Wasichana vyuo vikuu wapata mbinu kupenya uchaguzi mkuu

**Na Sabato Kasika**



Wasichana kutoka vyuo mbalimbali wakifuatilia hotuba ya mgeni rasmi kwenye maadhimisho hayo. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA.**

MACHI 13 mwaka huu, wasichana zaidi ya 300 toka vyuo vya jijini Dar es Salaam, wanakusanyika katika ukumbi wa mikutano wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji wakiadhimisha Siku ya Wanawake Duniani.

Mjadala mkuu siku hiyo ni ushiriki wa vijana katika uongozi kwa kuzingatia matumizi chanya ya teknolojia.

Akizungumza katika maadhimisho hayo, mbunge wa viti maalum mkoani Kagera, Halima Bulembo, anawapa mbinu mbalimbali vijana wa kike ili wapate uongozi.

Anasema, dhana ya usawa wa kijinsia ni hali ya wanawake na wanaume kuwa na fursa sawa na upatikanaji wa haki zenye kuleta tija, katika nyanja mbalimbali za maendeleo ya jamii, kati ya makundi hayo mawili.

"Lengo kuu ni kuwapo kwa usawa wa jinsia ni kuhakikisha raia wote wanapewa nafasi ya kukua na kuondolewa vikwazo mbalimbali ili waweze kuchangia na kutambuliwa kwa usawa katika maendeleo yao ya kijamii, kiutamaduni, kiuchumi na kisiasa," anasema Bulembo.

Maadhimisho hayo yakiwa yameandaliwa na Jukwaa la Wanaharakati Vijana la Young Feminist Forum (YFF) kwa kushirikiana na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), unawaleta vijana wa vyuo vikuu ambao ndiyo wasomi wanaotakiwa kuwa chachu kwenye uongozi wa kisiasa.

Aidha, Halima anawaambia kuwa hali hiyo inatokana na ukweli kwamba, hakuna nchi yoyote duniani, ambayo haijumuishi wanawake na vijana katika uongozi, hivyo vijana wanawake wasibaki nyuma kutafuta uongozi.

**MIKAKATI**

Mbunge Halima anataja mbinu zinazoweza kuwasaidia wasichana kufanikiwa katika harakati za kuwania uongozi kwamba, ni kutokata tamaa hata kama wanakutana na vikwazo kutoka ndani ya vyama.

Anasema, kuna changamoto nyingi ikiwamo maneno ya kukatisha tamaa kutoka kwa wale wasiowatakiwa mema, katika kuwania uongozi, lakini anawataka 'wakomae' tu hadi wafanikiwe.

"Viongozi wanawake wanahitajika kwa wingi, kwani tukiwa wengi tunaweza kusukuma ajenda zetu zikapita, hivyo niwatie moyo wale mnaotaka uongozi, msikate tamaa, wala kuogopa," anasema Halima.

Anasema, siri ya mafanikio ni uvumilivu na kujiamini na kwamba nafasi za uongozi zipo majimboni, wananchi wamewachoka viongozi waliopo sasa, wanataka wapya, lakini hawaoni wa kuwapa nafasi hizo.

"Kama msichana atakwenda kuwania ubunge au udiwani akashindwa, basi asikate tamaa bali arudi kujipanga ili mwaka mwingine wa uchaguzi arudi kuwania tena, asiogope kupambana," anasema mbunge huyo wa CCM.

Anawaambia kuwa kuna umuhimu wa vijana kuandaliwa mapema katika siasa ili kuja kuwa viongozi wakubwa wa baadaye katika nchi hii, hivyo vijana hawatakiwi kubaki nyuma.

> Vijana wa kike changamkieni fursa mbalimbali za uongozi, kwani hata kwenye serikali za wanafunzi vyuoni, wengi wa viongozi huwa ni wa kiume, hebu anzieni huko hadi bungeni.

"Kwa hiyo nirudie kusema kwamba, kuthubutu bila kuogopa na wala kutokata tamaa na pia uvumilivu ni mambo muhimu ambayo yatasaidia wasichana kufanikiwa kuingia katika uongozi," anasema.

**KUWA WANACHAMA**

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, anawataka vijana wa kike kujiunga na vyama vya siasa wanavyovitaja na kupewa kadi, kwa vile siyo rahisi kuwania uongozi, katika uchaguzi bila kuwa na kadi ya chama cha siasa na kulipa ada.

"Ni muhimu sana kuwa na kadi ya chama siasa, lakini vinginevyo siyo rahisi kuwania uongozi, hivyo niwahimize mkajiunge na vyama vya siasa mnavyovipenda wenyewe ili mpate kadi," anasema Liundi.

Anasema, TGNP haiwezi kuwaelekeza ni vyama gani wajiunge navyo, bali wao wenyewe ndiyo wanaojua ni wapi ambapo wanaona ni sahihi kwao ili wajiunga na kuwa wanachama halali.

"Vijana wa kike changamkieni fursa mbalimbali za uongozi, kwani hata kwenye serikali za wanafunzi vyuoni, wengi wa viongozi huwa ni wa kiume, hebu anzieni huko hadi bungeni," anasema.

Anasema, masuala ya haki na usawa wa kijinsia na ajenda nyingine zinazohusu wanawake, zinatakiwa kusimamiwa na vijana wanawake hasa wanafunzi wa vyuo kama hao, hivyo wasibaki nyuma.

"Wito wangu kwa vyama vya siasa ni kupanua wigo wa demokrasia ya usawa wa kijinsia ndani ya vyama hivyo ili kukuza ushiriki wa wanawake na vijana katika kuwania nafasi za uongozi," anasema.

Mkurugenzi mtendaji huyo anasema, wanawake wamekuwa wakikumbana na changamoto nyingi nyakati za uchaguzi hali, ambayo inachangia kuwakatisha tamaa na kuwakwamisha.




Halima Bulembo (kushoto) akizungumza kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani. Katikati ni Mkurugenzi wa TGNP, Lilian Liundi na Ofisa Programu Mwandimizi wa mtandao huo, Deogratius Temba.

Anasema, mwamko wa makundi ya wanawake na vijana katika siasa imeanza kuonekana, lakini bado muhimu kuwa wengi zaidi kwenye nafasi za uongozi na kuwa na mchango mkubwa wa kutetea wenzao.

**KUSHIRIKI SIASA**

Mmoja wa viongozi wa jukwaa hilo, Fatuma Ngamba, anawataka vijana wa kike na hasa wasomi wa vyuo vikuu, kushiriki katika harakati mbalimbali za kudai haki na usawa wa kijinsia bila woga.

"Tusione haya wala kudhani uanaharakati ni jukumu la watu fulani au kundi tofauti hasa kudhani kuwa ni watu wazima, bali hata vijana tunatakiwa kuwamo, hivyo tuungane, tuwe na mshikamano, ushirikiano na malengo ya kuwa na umoja," anashauri Fatuma.

Anawaambia wakiungana na kuwa na lengo moja, wanaweza kusaidiana hata kwenye kutafuta nafasi za uongozi na hatimaye wakawa wengi na kufanikisha ajenda zinazohusu usawa wa kijinsia.

"Kwa hiyo vijana wanawake tusibaki nyuma, katika harakati mbalimbali zenye lengo la kutufanya sisi vijana wanawake kwa ujumla kushiriki kwenye nafasi za uongozi," anasema Fatuma.

FUNZO LA CORONA

# Afrika ianze kujisimamia kiuchumi, isiiachie China kuifanyia kila kitu



Makao makuu ya Umoja wa Afrika, nchini Ethiopia yaliyojengwa na China. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**INATOKA UK.13**

naona kuwa kuibuka maradhi haya kuifanye Afrika kujitafakari kwa kuwa inategemea zaidi China kwenye uchumi wake, hivyo ni wakati wa kuanza kujitegemea kiuchumi, kuanzia kuzalisha huduma, bidhaa na kuwa muuzaji bidhaa ughaibuni badala ya kuagiza kila kitu mpaka kibiriti kutoka ng'ambo.

Maradhi hayo yapo Asia, Amerika na Ulaya na pia ni kitisho kwa Afrika lakini ni changamoto inayotakiwa kutumiwa katika kujitegemea.

**UTEGEMEZI UMEONGEZEKA**

Mchumi mbobezi na profesa wa uchumi, Samwel Wangwe, akizungumza na Nipashe kuhusu Afrika anavyoweza kuumizwa na corona kutokana na utegemezi wa kiuchumi kwa China na nchi za Asia, anakumbusha kuwa maradhi haya iwe fursa ya kuibuka na kubadilika ili kuanza kujitegemea.

Anaeleza kuwa hilo ni somo la kuanza kujielekeza kwenye mikakati ya kujitegemea na kuacha utegemezi uliokithiri kwa China, kwani Afrika badala ya kuiga na kuitumia kujitegemea imeongeza maradufu utegemezi kwa China.

Anaonya kuwa hakuna sababu ya Afrika na hata Tanzania kujiweka pembeni na kuiachia China kufanya kila kitu kwenye miradi hasa ujenzi na uwekezaji, wakati wananchi, serikali na wataalamu wakiendelea kuangalia kinachoendelea kama vile ni mashabiki wanaofurahia kandanda uwanjani.

Anatoa mfano kuwa kampuni za China zimekuwa wajenzi wakuu

> Chuma itumiwe kuzalisha skuruu, nati na bolti za magari, pikipiki, matrekta, kompyuta, mashine ...vifaa hivyo ni muhimu tena vinaweza kutumiwa na sekta nyingi si Tanzania na sehemu nyingine nyingi Afrika.



Wataalamu na wanasiasa wakiwa kwenye mgodi wa makaa ya mawe ya Kiwira, Tanzania inashauri kuanza kuchenjua makaa hayo na kuanzisha viwanda vya bidhaa za chuma. **PICHA: MTANDAO.**

wa miundombinu ya Afrika, viwanda na kufanya uwekezaji kwanini? Anasema inashangaza wanapewa zabuni zote wenyewe na makandarasi na wajenzi wanabaki kuwa watizamaji ndani ya mataifa yao.

Inakuwaje badala ya kuitumia China kuendelea kinachoendelea ni kuitumia China kubaki maskini na kuendelea kuwa wategemezi maradufu?

**CHA KUFANYA**

Profesa Wangwe anashauri kufanyakazi mathalani za ujenzi wa miundombinu au majengo ya serikali kwa kushirikiana na China na si kuwaachia kila kitu peke yao. Kwa mfano kama ni ujenzi wa barabara za juu Ubungo, Tanzania ilitakiwa kukubaliana kuwa ina ujuzi na utaalamu kiasi fulani hivyo ndiyo utakaokuwa mchango wake kwenye kandarasi hiyo.

Aidha, China nayo ingeelezwa kuwa inatakiwa kushiriki kwa kiwango gani iwe vifaa, teknolojia au utaalamu na kwamba kila upande ungeshiriki kwenye kazi na si kuiachia China yenyewe, kwani taifa linahitaji pia kufunza wahandisi na makandarasi wa kujenga madaraja ya juu ya njia za juu hata majengo ya kisasa.

Anasema si hivyo tu, hata kwenye maeneo mengine lazima sasa kuamka na kufanyakazi kwa lengo ya kupata teknolojia kwa kushirikisha makandarasi au vijana wa Tanzania na Afrika kwenye kandarasi hizo badala ya kuwaachia kila kitu kwani hata wazawa wanatakiwa kubakia na utaalamu na siyo kuachwa walivyo kwani wengi hawana ujuzi.

"Kinachohitajika ni kuunganisha nguvu na kujijengea uwezo wa kujitegemea sisi wenyewe, tusikae pembeni na kuwaachia wageni kazi zote za ukandarasi na miradi mikubwa ya kiuchumi. Tuwaambie sisi tuna hiki pengine asilimia 40 na tunataka ninyi mjazie hapa asilimia 60 zinazobakia na tunahitaji mfanye kazi na vijana na wataalamu wetu..." anasisitiza Profesa Wangwe.

**KAMPUNI ZA UMMA**

Profesa Wangwe anaeleza kuwa kampuni za China zinazojenga miundombinu na miradi mikubwa ya uchumi Afrika ni za umma kwa mfano kuna kampuni ya reli China Railways Construction Corporation Limited-CRCC. Nyingine ni China Civil Engineering and Construction Corporation CCECC zinajenga miradi Tanzania na kwingineko Afrika.

"Hizi ni kama kampuni yetu ya ujenzi ya taifa ya MECCO Mwananchi Engineering and Contracting Company Limited, ilijenga majengo makubwa kama jengo la kitega uchumi la bima-NIC soko la Kariakoo. Haikutakiwa kuachwa inatakiwa ufufuliwe ifanye kazi kama ambavyo Wachina wanatakiwa kutumia mashirika ya umma. Ni lazima tuanze kujitegemea kama wanavyofanya wenzetu," anasisitiza Profesa Wangwe.

**KUJENGA VIWANDA**

Akizungumzia jinsi utegemezi wa bidhaa na huduma kutoka ng'ambo unavyoweza kudhibitiwa ,Dk. Kamugisha Byabato, mhandisi wa nishati jadidifu (renewable energy) na mitambo kutoka Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine Tanzania (Sauti) Mwanza, anasema kuibuka kwa corona ni fursa kwa Afrika kufikiria kuanza kujitegemea sasa.

Anasema japo ni janga linaloangamiza binadamu, lakini ni fursa kwa Afrika kujipanga kuzalisha bidhaa bora kwa kutumia teknolojia rahisi kama inavyofanya China.

**FURSA INAYOIBUKA**

Dokta Byabato anasema wakati huu Afrika inapotafakari wapi pa kupata soko la kununua bidhaa kuanzia mavazi hadi mashine kutokana na kitisho cha mafua ya corona kuelekea kutishia na kukwamisha uchumi na uzalishaji huko China, ni wakati wa kuanzisha viwanda vya bidhaa za kiteknolojia na zenye ubora zinazouzwa kwa bei nafuu.

Anakumbusha kuwa China ni mnunuzi mkubwa wa malighafi kutoka Afrika ili kuzalisha vitu vya aina mbalimbali ambavyo vinarudi kwenye soko la Afrika mfano simu za mikononi, pikipiki, nguo, vifaa vya umeme na ujenzi pamoja na vyombo vya nyumbani.

Mhadhiri huyo anakumbusha kuwa China inanunua madini, bidhaa za kilimo na mifugo, mazao ya misitu na kila kitu ambacho inaona kinafaa kwa uchumi wake kutoka Afrika, ambayo imeshindwa kutumia fursa hiyo kujitegemea.

"Afrika imejaa malighafi inachokosa ni teknolojia yaani wabunifu na wataalamu wa kutosha wa kutumia mitambo na mashine kuzalisha viwandani. Ndiyo maana sasa ianze kutumia wataalamu wachache waliokuwapo kwa ajili ya kuzalisha bidhaa mbalimbali kama ambavyo China inafanya huku ikiendelea kufundisha na kuandaa wengine."

**IFANYE NINI?**

Anasema kwa mfano Tanzania ina chuma ya kutosha inayopatikana Liganga, lakini ina makaa ya mawe ya kutosha yaliyoko Mchuchuma, Ngaka na Kiwira.

"Katika mazingira hayo kuna chuma na mkaa wa mawe, ambao unatumiwa kuyeyusha chuma kupata malighafi za kuzalisha mashine, meli, reli, mitambo, magari na vifaa vingi vya ujenzi kama nondo na vyuma vikiwamo vya kuezekea.

"Pia ndiyo malighafi ya viwanda vya kutengeneza 'bolti', 'skruu' na 'nati' na vipuri vya magari, mitambo, mashine, kompyuta vinajengwa kwa kuwa kuna chuma itumike kutengeneza bidhaa hizo sasa," anashauri.

Anaongeza: "Chuma itumiwe kuzalisha skuruu, nati na bolti za magari, pikipiki, matrekta, kompyuta, mashine ...vifaa hivyo ni muhimu tena vinaweza kutumiwa na sekta nyingi si Tanzania na sehemu nyingine nyingi Afrika."

Aidha, anasema kuna wataalamu wa kutengeneza magari na miundombinu kikiwamo kiwanda cha Jeshi la Wananchi cha Nyumbu-kilichoko Kibaha mkoani Pwani.

Halikadhalika, anaeleza kuwa Tanzania ina madini mengi kuanzia dhahabu, bati, shaba, urani na magadi. Yote hayo yanaweza kutumiwa kwenye viwanda vya kiteknolojia kuzalisha mota za umeme, simu na viambato vyake, ikiwa Tanzania na Afrika inajipanga kikamilifu kukabiliana na fursa hizi zinazojitokeza kutokana na changamoto iliyotokea China.

**UMEME**

Anasema mradi wa kusambaza umeme nchini kote unategemea nyaya za umeme na transfoma. Zote kwa kiasi kikubwa zinaagizwa kutoka China, lakini zinaweza kuzalishwa nchini. Moto hizo za umeme zinategemea madini ya aina mbili ya chuma na shaba.

Transfoma nazo kwa mujibu wa maelezo yake hutegemea nyanya ambazo ni za shaba na chuma kwa ajili ya kuunda 'bodi'. Teknolojia hiyo na wataalamu wapo nchini hivyo kwa Tanzania ni kujipanga zaidi na kuzalisha zaidi.

**VIKOMBE VYA UMEME**

Dokta Byabato anasema vikombe vya kupoza umeme vinavyofungwa kwenye nyaya ni sehemu ya bidhaa ambazo zinaweza kuzalishwa nchini kwa kutumia udongo wa 'caoline' ambao unapatikana ukanda mzima wa pwani na eneo ambalo unafahamika na umeshawahi kuchimbwa ni Pugu.

Vikombe hivyo vinaweza kutumiwa na mashirika mengi ya umeme Afrika na hata nje ya Afrika iwapo vitazalishwa kwa ubora na kwa teknolojia ya kisasa.

**NGUO**

Msomi huyo anakumbusha kuwa licha ya China kuiuzia nguo Afrika inachukua pamba ambayo ni malighafi inayozalishwa na nchini na karibu Afrika nzima.

Anataka Afrika ijenge viwanda vya kutengeneza nguo za aina mbalimbali badala ya kutegemea zinazotoka China kwani leo ndilo taifa linalozalisha madera, kanga, fulana na nguo mbalimbali kwa ajili ya wateja wa aina mbalimbali.

**VIWANDA VYA VIPURI**

Dokta Byabato anasema ni wakati wa kuanza viwanda vya kuzalisha vipuri kama magurudumu, 'bearings' za magari na hata matairi yazalishwe kwa wingi kuanzia ya pikipiki, baiskeli, trekta, bajaji kwa sababu mashamba ya mpira yapo.

Anakumbusha kuwa kwenye kutengeneza matairi kinachohitajika ni teknolojia ya kuandaa tabaka (layers) za matairi kulingana na mahitaji kwa mfano tairi la ndege ni kuongeza tabaka (layer) za kuliwezesha kuhimili shinikizo la kuendesha chombo hicho.

Aidha, matairi ya pikipiki na bajaji nayo tofauti zake ni matabaka yanayohitajika kulingana na ukubwa chombo kinachohusika.

Anasema, kwa Tanzania wataalamu na wahandisi wa aina mbalimbali wapo, tena wengine walipelekwa masomoni ng'ambo miaka ya 1970, lakini hawajatumiwa au kutumikia taifa ipasavyo, hivyo serikali iwasake popote walipo na waanze kutumika saa kujenga viwanda.

> Halikadhalika, anaeleza kuwa Tanzania ina madini mengi kuanzia dhahabu, bati, shaba, urani na magadi.

## Mke wa Makamu Rais awa Waziri wa Ulinzi Sudan Kusini



Angelina Teny, Waziri wa Ulinzi pamoja na Rais Kiir. **PICHA: MTANDAO**

RAIS wa Sudan Kusini, Salva Kiir, ametangaza majina ya mawaziri wapya wanaounda Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) nchini humo.

Katika Baraza la Mawaziri wa Kiir, mke wa makamu wa Rais Riek Machar, ambaye ni hasimu wake anakuwa Waziri wa Ulinzi.

Sudan Kusini inakabiliwa na changamoto nyingi kwa kurejesha amani na usalama katika maeneo mbalimbali nchini humo.

Kwa jumla, serikali hiyo itaundwa na mawaziri 34 na manaibu waziri 10 na pia kuna wanawake walioteuliwa katika nafasi muhimu.

Wanawake wanane watashiriki katika serikali hiyo ya Sudan Kusini. Mkewe Makamu Rais Riek Machar, Angelina Teny, ambaye ameteuliwa kuwa Waziri wa Ulinzi, ni miongoni mwa wanawake hao walioteuliwa kwenye nyadhifa kubwa.

Béatrice Khamisa pia ameteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Sudan Kusini. Ni mara ya kwanza nchini Sudan Kusini wanawake kushikilia nafasi kama hizo. Pia, mwanamama mwingine ameteuliwa kuwa Waziri wa Mazingira.

Mawaziri wengine ni; Jean-Luc Jock sasa anashikilia wadhifa wa Waziri wa Mambo ya Afrika, Paul Ayom Akek, ameteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani.

Miezi 18 ilikuwa muhimu kwa Salva Kirr na Riek Machar kukubaliana juu ya masharti ya mchakato wa amani na kabla ya kuundwa kwa serikali ilichukua wiki tatu zaidi kwa mahasimu hao wawili kukubaliana juu ya nafasi muhimu katika serikali hiyo.

Hata hivyo, makubaliano kati ya wawili hao yalizaa matunda na kupelekea kushuka kwa mapigano na kuwezesha maendeleo hatua kwa hatua kuelekea suluhu ya kisiasa katika wiki za hivi karibuni.

Wakati huo, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa limeongeza muda wa mwaka moja kwa tume yake nchini Sudan Kusini, Minuss, likisema kwamba hali katika nchi hiyo "bado ni hatari kwa amani na usalama katika ukanda huo". **RFI**

# Uchaguzi Marekani kuweka historia ya rais kikongwe ?




Waonyesha nia Biden (kushoto) na Sanders wakiwa jukwaani kuchuana kuomba kuteuliwa kugombea urais kwa teketi ya Democratic. **PICHA: CNN.**

**Na Mashaka Mgeta**

UCHAGUZI Mkuu wa Rais wa Marekani unatarajiwa kufanyika Jumanne ya Novemba 3, mwaka huu, huku wagombea wanaopewa nafasi kubwa ya kuibuka washindi wanatajwa kuwa ni Donald Trump, Joe Biden na Bernard Sanders.

Wakati Trump ni Rais wa sasa kwa tiketi ya chama cha Republican, Biden na Sanders wapo katika 'fainali' ya mchujo wa kuomba kuteuliwa na chama cha Democratic kuwania kiti hicho.

Zipo hoja na mazingira kadhaa 'yanayowazunguka' wagombea hao katika historia ya uchaguzi, na zaidi kwa kiti cha urais kilicho nafasi ya juu ya utawala wa taifa hilo lenye nguvu kubwa za kiuchumi na kijeshi. Miongoni mwa hayo na linalobeba mjadala ni kuhusu umri mkubwa, ule unaowaweka katika kundi la wazee hasa kwa atakayefanikiwa kushinda kiti hicho na kuapishwa mapema 2021.

### REKODI YA UZEE

Rekodi zinaonyesha kuwa, Rais Donald Trump alizaliwa Juni 14, 1946 kwenye Hospitali ya Jamaica jijini New York. Hivyo ana takribani miaka 74 na ikiwa atashinda tena kiti hicho, ataapishwa akielekea miaka 75.

Wakati Trump ametimiza kalenda 74, Sanders aliyezaliwa Septemba 4, 1941 huko Brooklyn, New York ametimiza miaka 78. Kama atafanikiwa kuteuliwa na kushinda kiti hicho ataapishwa akielekea umri wa miaka 79.

Kwa upande wake, Biden alizaliwa Novemba 20, 1942 katika Hospitali ya St Mary huko Scranton, Pennsylvania. Hivyo kwa sasa ana miaka 77 na ikiwa atateuliwa na kushinda urais, ataapishwa akiwa katika umri wa miaka 78, yaani mwaka mmoja nyuma ya Sanders.

> Kwa mujibu wa Biden, wanawake wengine wanaoweza kushika nafasi hiyo ni aliyekuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sally Yates na maseneta wa New Hampshire, Maggie Hassan na Jeanne Shaheen.

Kwa upande wake, Trump anapewa nafasi ya kuwa 'rais mzee' ikiwa tu atafanikiwa kushinda awamu ya pili ya kuitawala Marekani, wakati Sanders na Biden watakuwa wanaingia madarakani wakiwa 'marais wazee' ikiwa watamshinda Trump. Lakini kwa namna kura za maoni zinavyopigwa katika chama cha Demoratic, Biden anapewa nafasi kubwa zaidi ya kuteuliwa kuwania kiti hicho.

### HISTORIA YA BIDEN

Ni mwanasiasa mzee akiwa na umri wa miaka 77, mzaliwa wa Scranton, Pennsylvania. Aliishi Wilmington, Delaware.

Amekuwa seneta katika awamu sita tangu alipochaguliwa kwa mara ya kwanza mwaka 1972, akitokea Delaware. Pamoja na nafasi hiyo, Biden amewahi pia kuwa Makamu wa Rais wa 47 wa Marekani.

Pia aliwahi kuomba ridhaa ya chama chake kimteue kuwania urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka 1988 na ule wa 2008.

Biden alitumika katika nafasi ya Makamu wa Rais wakati wa utawala wa Barack Obama, wakati wa kupitishwa kwa sheria ya unafuu wa huduma za afya Affordable Care Act, na hadi sasa suala la huduma bora za afya limebaki kuwa miongoni mwa vipaumbele vyake.

Ni jambo analolijadili mara kwa mara katika muktadha wa changamoto zilizowahi kuikabili familia yake. Mke wake wa kwanza na binti yake walifariki dunia kwenye ajali ya gari mwaka 1972. Na mwaka 2015, kijana wake wa kiume, alifariki kutokana na saratani ya ubongo.

Huduma bora za afya, anasema kupitia tangazo dogo linaloongekana kwenye runinga, ni jambo linalomgusa katika ubinafsi wake.

Pia akiwa mwenyekiti wa zamani wa Kamati ya Uhusiano wa Nje ya Seneti ya Marekani, Biden anaongelea kwa 'hisia kali' kuelezea na kulinda wajibu wa Marekani kwa dunia.

Akiwa na uzoefu wa kutumika kwa miongo kadhaa katika nafasi ya useneta, anaamini katika thamani ya vyama vya upinzani kushirikiana na chama tawala.

Hivyo anasema akichaguliwa kuwa Rais wa Marekani, atawasilisha hoja hiyo kwa chama kilichopo madarakani kwa sasa-Republican.

Kwa hesabu za umri wake, bila shaka Biden atakuwa Rais anayeingia madarakani (ikiwa atagombea na kumshinda Trump, lakini zaidi atakapoapishwa akiwa na umri wa miaka 78. Katika masuala ya kisiasa, Biden amefanikiwa kujijenga katika majimbo hayo.

### USHIRIKA WAKE NA OBAMA

Uhusiano wa Biden na Obama ni mkubwa sana. Wanashirikiana vizuri; na Biden amekuwa akizungumzia suala la urafiki wao huo mara kwa mara, pamoja na kazi walizofanya kwa masuala kama huduma bora za afya kwa wote na sera za nje.

Amekuwa akisifiwa sana katika kampeni zake pindi anapomtaja na kumsifu Obama. Na wapigakura wengi katika chama cha Democratic, hasa wenye asili ya Afrika, wamekuwa wakivutiwa na uhusiano huo na namna unavyowafanya wamuunge mkono Biden.

### BEN SANDERS

Seneta Bernie Sanders, aliyemshindani wa karibu wa Biden katika kuwania kuteuliwa na Democratic kuwania urais, anamzidi Biden kwa mwaka mmoja.

Lakini kama Rais wa sasa, Donald Trump atashinda tena kiti hicho, atakuwa rais mzee katika historia ya taifa hilo. Historia yake inaonyesha kuwa baada kuzaliwa Scranton, Pennsylvania, alihamia Delaware akiwa mdogo.

### CORONA YAWATENGANISHA

Wakati mdahalo wa 11 wa wanaotafuta kuwania urais kupitia chama cha Democratic ukifanyika, wagombea hao walilazimika kusimama mbali wakiachana kwa takribani futi sita kama moja ya njia za kuepuka maambukizi ya virusi vya corona.

Ulikuwa mdahalo wa watia nia wawili, Biden na Sanders waliobaki katika kinyang'anyiro hicho kupitia Democratic. Ni 'mtanange wa kisiasa' unaotarajiwa kufikia majimbo ya Arizona, Florida, Illinois na Ohio wiki hii. Licha ya tukio hilo la kuihamasisha jamii kujiepusha na maambukizi ya virusi hivyo, Biden na Sanders wanamkosoa na 'kumshambulia' Trump kwa kauli zake kuhusiana na corona.

Wakati hayo yakijiri, Sander anasisitiza umuhimu wa 'kumnyamazisha' Trump, jukumu analosema linapaswa kufanyika akiwa Rais ama hata asipochaguliwa kushirika nafasi hiyo ya juu ya utawala wa Marekani.

"Kitu cha kwanza tunachopaswa kukifanya, nikiwa nimechaguliwa kuwa Rais ama vinginevyo, ni kumnyamazisha huyu Rais kuanzia sasa," Sanders anasema.

### KUTEUA MWANAMKE

Biden anaweka wazi kwamba ikiwa atachaguliwa kuwa Rais, basi hana namna nyingine zaidi ya kumteua mwanamke kuwa Makamu wa Rais.

"Kuna wanawake wengi wenye sifa na vigezo kuwa Rais hata kesho. Nitamteua mwanamke kuwa Makamu wa Rais," anaongeza.

Kwa sasa, Biden anaongoza katika kura za maoni kwa chama chake, akipewa nafasi kubwa zaidi ya kumkabili Trump kwenye uchaguzi huo.

Amewahi kuwataja wanawake kadhaa kwamba wana sifa za kuwa Makamu wa Rais, wakiwamo Seneta wa California, Kamala Harris, Stacey Abrams, Seneta wa Minnesota, Amy Klobuchar na Seneta wa Massachusetts, Elizabeth Warren.

Kwa mujibu wa Biden, wanawake wengine wanaoweza kushika nafasi hiyo ni aliyekuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sally Yates na maseneta wa New Hampshire, Maggie Hassan na Jeanne Shaheen.

Hata hivyo, kwa upande wake, Sanders hakutoa uhakikisho wa kumteua mwanamke kuwa mgombea mwenza ili kama akishinda, awe Makamu wa Rais.

Marekani imeshakuwa na wanawake wawili tu katika historia yake, walioteuliwa kuwa wagombea wenza. Wanawake hao ni Geraldine Ferraro aliyewania kupitia kwa mgombea urais Walter Mondale katika uchaguzi wa mwaka 1984 na Sarah Palin aliyewania kupitia kwa John McCain mwaka 2008.

***Makala haya yameandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali vya kwenye mtandao. 0754691540***

# Mfumo ACT-Wazalendo kitendawili cha kikatiba, uchaguzi mkuu 2020



Zito Kabwe na Maalimu Seif (kulia) katika majukumu ya chama chao. **PICHA MTANDAO.**

**Na Ani Jozeni**

UCHAGUZI wa viongozi wa kitaifa katika chama cha ACT-Wazalendo kirefu cha Alliance for Change in Tanzania ambacho siyo rahisi kusikia kikitajwa umekamilika.

Kilichoingia katika hisia za watu au za wafuatiliaji wa habari kwa jumla ni mpangilio ulioonekana katika ngazi ya juu kabisa, na kwa upande mwingine kuwekwa picha katika kurasa za kwanza za magazeti kadhaa nchini.

Kilichojiri ni kupata kura nyingi Seif Sharif Hamad Mwenyekiti Taifa na Zitto Kabwe kiongozi mkuu, hao wakiwa katika picha na Makamu Mwenyekiti Bara, Dorothy Semu.

Ni mazingira yenye kuyakinisha mahitaji kadhaa ya kisiasa katika pande zote mbili kwanza kisiasa halafu kiutendaji, kuwa Zitto Kabwe ni mwanzilishi na kiongozi mkuu badala ya uenyekiti kama ilivyozoeleka. Na Maalim Seif anapanda ngazi moja kimfumo ukilinganisha na nafasi yake ya ukatibu mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF) ingawa alikuwa mwenyekiti halisi kwa upande wa Zanzibar. Alikuwa Katibu Mkuu wa CUF (Taifa) ila mwenyekiti hakuwa na nafasi Zanzibar.

Ina maana kuwa uenyekiti wa Maalim Seif wa chama cha siasa anachoshiriki kwa upande wa Zanzibar uko pale pale na sasa unatambuliwa rasmi, na hiyo si ajabu baadhi ya wafuasi wake na labda wengi zaidi kuendana na hali itakavyokuwa wawe tayari au wawe na hamasa kama ile ya kwanza.

> Inaelekea pia kwamba nafasi ya ukatibu mkuu ACT-Wazalendo itakuwa na mtu kama Dk. Mashinji, yaani mtendaji na siyo mfafanuzi wa mwelekeo wa chama, kwani kiongozi mkuu na mwenyekiti taifa wanatosha kwa hitaji hilo.

Itakuwa siyo rahisi kwani CUF ilianzia Zanzibar na msingi wake ulikuwa ni uanaharakati Visiwani, yaani Kamahuru, ufupisho ambao isingekuwa rahisi kuundiwa Bara. Huku kwa jumla vifupisho ni vya Kiingereza, kama NCCR na hata CUF yenyewe, siyo Kamahuru.

Inaelezea vile vile kuwa katika mahusiano yao ya kawaida kisiasa, hakuna chembe ya mabadiliko jinsi Zitto anavyohusiana na Seif, kuwa Zitto ndiyo kiongozi na Seif ni mshauri mkuu. Ilikuwa kidogo kama ilivyowahi kuwa Chadema ambako aliyekuwa mgombea urais, Edward Lowassa, alikuwa mshauri mkuu asiye rasmi, na katibu mkuu ambaye sasa amekimbia chama, Dk. Vincent Mashinji, akiwa mtendaji tu wa chama.

Wakati wa Dk. Wilibrod Slaa, katibu mkuu alikuwa pia ndiye mshauri mkuu wa Mwenyekiti Taifa, Freeman Mbowe, na akawa pia mgombea urais wa chama hicho 2010 aliyekipatia mafanikio makubwa. Hivi sasa mshauri mkuu ni Makamu Mwenyekiti Bara.

Kuna uhusiano wa karibu kati ya nafasi ya uongozi wa chama na ugombeaji nafasi ya juu zaidi, na kwa maana hiyo anayetazamiwa kugombea anaweza kuwa ndiyo mwenyekiti au ni mshauri mkuu wa mwenyekiti. Endapo ni mwanachama wa muda mrefu anakuwa pia na nafasi ya utawala, ambako inategemea hali ilivyo kwa wakati uliopo, kama ni ukatibu mkuu (unaoashiria ufafanuzi wa kina wa sera na mielekeo ya chama) au umakamu mwenyekiti.

Hapa mwonekano ni ukaribu wa kihisia kati ya mwenyekiti na huyo msaidizi mkuu, ila nafasi hiyo inaweza kutumika 'kujazia' mahitaji ya sura ya chama kitaifa, kama enzi za Profesa Abdallah Safari.

Inaelekea pia kwamba nafasi ya ukatibu mkuu ACT-Wazalendo itakuwa na mtu kama Dk. Mashinji, yaani mtendaji na siyo mfafanuzi wa mwelekeo wa chama, kwani kiongozi mkuu na mwenyekiti taifa wanatosha kwa hitaji hilo.

Chadema kuna mwelekeo unaorudi kwa kiasi fulani kwa Dk. Slaa, kwani John Mnyika licha ya kuwa havijazi 'viatu' vya Dk. Slaa, bado ni mmoja wa viongozi waandamizi na sehemu ya Chadema 'jadi,' waliokuwapo miaka yote. Ni mtu mwenye uwezo wa kutoa ushauri wa karibu kwa mwenyekiti, nje ya makamu mwenyekiti (Bara).

Ni kielelezo kuwa sura ya chama kwa mpangilio wa viongozi wake inaendana na chama hicho kinavyojisikia miongoni mwa watu, kinvyojipanga na kujitambulisha kwa watu, kudhihirisha mshikamano kwa upande mmoja na upenyo wa mamlaka kwa upande wa pili. ACT-Wazalendo siyo rahisi kuwa na katibu mkuu mwenye upenyo halisi wa madaraka au makamu mwenyekiti Bara, kwani waanzilishi wa ngazi ya juu walishaondoka huko na kwenda CCM. ACT-Wazalendo ilikuwa na hisia iliyogawnyika sehemu mbili, ile ya upinzani inayotumia itikadi ya uzalendo kama nyenzo ya upinzani, na ile ya uzalendo inayotumia upinzani kama nyenzo tu.

Waliokuwa katika hisia ya pili, ambao kwa ndani ni wazalendo kwa maana ya uanaharakati na mabadiliko, siyo upinzani kwa maana ya kuiondoa CCM madarakani kama hisia ya msingi ya ushiriki wao kisiasa, ndiyo hao waliohama na kuingia CCM. ACT-Wazalendo walikuwa ni wengi zaidi kwani chama hicho ni mchepuo wa Chadema katika mtafaruku wake na aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu Zitto Kabwe. Wako ambao hawakuungana na Zitto katika ACT-Wazalendo ambao pia waliondoka wakati awamu ya tano ilipoonyesha sura mpya ya uzalendo na hata uanaharakati wa kisiasa, ila wasingeweza kuwa wengi kama kule ACT-Wazalendo kwani Chadema imesheheni watu wanaoipinga CCM kama hisia yao ya msingi.

Kwa upande mwingine mpangilio wa uongozi katika ACT-Wazalendo sasa umekaa vizuri zaidi kutokana na kuondolewa kwa nafasi ya mwenyekiti taifa ambaye maskani yake na chimbuko lake ni Bara.

Anabaki tu kiongozi mkuu na mwenyekiti taifa anakuwa kana kwamba ni mwenyekiti Zanzibar, hivyo hakuna ushindani wa nafasi kiuongozi, sababu mojawapo ikiwa ni kuondolewa kwa wale waanzilishi ambao wangekuwa katika nafasi za juu za ushauri au utawala wa chama.

Waandamizi zaidi ni Profesa Kitila Mkumbo aliyekuwa mshauri wa ngazi ya juu Chadema (mshauri mkuu akiwa ni Profesa Mwesiga Baregu), na Anna Mghwira aliyekuwa mgombea urais wa chama hicho na mwenyekiti wa kwanza.

# Wenye vyama mnawategemea wapigakura kutoka kundi lipi?




Wapigakura wakisoma majina na kuingia kwenye sanduka la kura. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Said Nguya,** DODOMA

VYAMA vya siasa takribani 19 mwaka huu vinatarajiwa vishiriki uchaguzi mkuu wa kitaifa wa viongozi kada ya udiwani, ubunge na urais.

Ni mithili ya timu za mchezo wa mpira wa miguu zikiwa uwanjani, ingawa tofauti na kwenye uwanja wa mpira kwenye siasa viwanja haviwekwi nyasi bandia.

Aidha, wakati ushindi kwenye ushindani wa mpira wa miguu hupatikana kwa kuzingatia kauli ya 'mchezo ni dakika 90' ushindi wa kisiasa hutegemea zaidi historia.

Katika nchi ya kidemokrasia kama Tanzania, mtaji wa ushindi kisiasa ni wingi wa wapigakura, ambao wanaweza kuwa wanachama, wakereketwa, wafuasi na mashabiki wa kisiasa.

Ni wazi ushindi wa kisiasa siyo wa "dakika 90 uwanjani" kutokana na ukweli kwamba chama kupata wapigakura wengi ni mchakato wa muda mrefu.

Umahiri wa chama katika kusimamia itikadi na imani zake, ndiyo msingi imara kwa chama kuwa na wapigakura wengi.

Hata hivyo, katika siku za karibuni, siasa nchini imepoteza uhalisia huo. Hili linadhihirishwa na wimbi la wanachama kujiunga na vyama vya kisiasa kwa ushabiki na kuvutiwa na utendaji kazi wa baadhi ya viongozi na sio itikadi na imani ya vyama kama ilivyotarajiwa hapo awali.

> Kura za mazoea pia zinatajwa kukiongezea nafasi ya ushindi chama hicho, ikilinganishwa na vyama vya upinzani ambavyo havina nafasi katika makundi hayo ya wapigakura.

Wapo wanaoshuhudiwa wakihama kutoka chama kimoja kwenda kingine, kwa madai ya kuchukizwa katika vyama vyao vya awali lakini ni dhahiri zipo sababu ambazo haziwekwi wazi.

Awali, itikadi za vyama na uelewa wa kutosha wa mlengo wa kisiasa wa vyama vya siasa ndiyo ulikuwa msingi wa watu kujiunga na vyama, tofauti na sasa ambapo ufuasi wa vyama vya siasa unaongozwa na hisia, ushabiki binafsi na kuridhishwa kwa matakwa yao ya maisha.

Nyakati za uchaguzi mkuu, vyama vya siasa vimekuwa vikitumia kila mbinu kujiongezea wapiga kura.

Mwaka huu, ukiacha chama kikuu cha upinzani Chadema CCM, ACT- Wazalendo, NCCR - Mageuzi na TLP vyama vingine vipo kimya havijaweka wazi hata mikakati yake ya ushindi.

Kwa upande wa vyama vya upinzani, vikiwamo Chadema, ACT - Wazalendo na CUF vimekuwa vikitumia mbinu tofauti na zile zinazotumiwa na CCM, katika kutafuta wapigakura.

Ikumbukwe, yapo makundi matano ya wapigakura; wale wanaopiga kwa kura za huruma, wapigaji wa masuala, wapo wanaopiga kura za itikadi na imani, kura za mazoea pamoja na kura kushtukiza.

### KURA ZA UPINZANI

Vyama vya upinzani vimekuwa vikitumia zaidi mbinu ya ushawishi wahisia, ili kupata huruma kwa wananchi (Public Sympathy) kwa kigezo kwamba wanaonewa na serikali.

Kwa sasa vyama hivyo vinafanya juhudi za kutosha, katika kutumia mbinu hiyo ili kuaminisha watu kuwa vinaonewa na hakuna mazingira ya kufanya siasa wala kukosoa serikali.

Endapo watafanikiwa kutumia vizuri mbinu hii, wataelekea kwenye uchaguzi mkuu wakiwa na uhakika wa wapigakura wa kundi la kura za huruma.

Uzoefu wa kisiasa katika kugawa makundi ya wapigakura kuanzia ngazi ya familia, unaonyesha wapigakura za huruma huwa ni asilimia 16, wa masuala ni asilimia 32, kwenye itikadi na imani ni 28 na mazoea ni 14 wakati kushtukiza ni asilimia 10.

### CCM

Kwa upande wa CCM imekuwa ikitumia mbinu ya kueleza jinsi ilivyotekeleza ahadi, matakwa na matarajio ya wananchi tangu walipochaguliwa kuongoza dola, tangu awamu moja hadi nyingine ya uchaguzi. Mbinu hii ndiyo inayofahamika kama mbinu ya masuala, ambayo huwapa uhakika wa asilimia 32 ya kura zote zinazopigwa.

Licha ya uwepo wa sintofahamu katika siasa, CCM bado ina mtaji mkubwa wa wanachama wanaotambua itikadi na imani zake, hususan watu wazima na wazee. Ni kwa msingi huo, chama hicho kinapewa nafasi kubwa zaidi ya kuwa na wapigakura wengi ikilinganishwa na vyama vya upinzani.

Kwa upande wa wapiga kura za mazoea, pia chama kinachopewa nafasi kubwa ni CCM kutokana na kuwa kikongwe katika kuongoza serikali na kushinda katika chaguzi mbalimbali.

Ni katika kundi hili la wapigakura, wanapokutwa watu ambao hupenda kupigia kura chama chochote, chenye mwelekeo wa kushinda.

Hata hivyo, katika kundi hili vyama vya upinzani vikicheza karata zake vizuri, baadhi vinaweza kutoa ushindani na kujinyakulia wapigakura.

### KUSHTUKIZA

Wapigakura za kushtukiza ni kundi lisilotabirika. Hili linaweza kumwangukia yeyote maana ni aina ya watu ambao hufanya uamuzi ndani ya chumba cha kupigia kura.

Uamuzi wa watu wa aina hii hutegemea masuala yanayoongelewa siku hiyo ya kupiga kura, huwa hawana msimamo na hujihisi hawana cha kupoteza.

Kilichotokea mwaka 2015 hakuna mtu aliye makini katika kufuatilia siasa nchini, ambaye hakushuhudia jinsi vyama vya upinzani kupitia umoja wao uliyofahamika kama Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa), vilivyotoa ushindani wa kutosha kwa CCM katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.

Hali hii ilitokana na vyama hivyo kuteka ajenda ya masuala (kueleza kuhusu dola na utekelezaji wa ahadi, matakwa na matarajio ya wananchi).

Inasadikiwa kuwa chama chochote cha siasa kikiweza kusimamia vyema ajenda hiyo vizuri, huteka wapigakura wengi ikilinganishwa na ajenda zingine.

### ILIKUWAJE CCM KUSHINDA?

Mbinu iliyokinusuru chama hicho ni kuteka wapigakura wa kundi la itikadi na imani ambalo pia linasadikiwa kuwa na mchango mkubwa katika kukipa chama cha siasa ushindi.

Kura za mazoea pia zinatajwa kukiongezea nafasi ya ushindi chama hicho, ikilinganishwa na vyama vya upinzani ambavyo havina nafasi katika makundi hayo ya wapigakura.

Said Nguya ni mchambuzi wa masuala ya Siasa na Maendeleo anapatikana Dodoma



HABARI MBEYA

## Maonyesho ya mazao kutoa elimu kwa wakulima

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

ZAIDI ya teknolojia 30 za mazao mbalimbali ya kilimo, zinatarajiwa kuonyeshwa na Kituo cha Utafiti wa Mazao ya Kilimo (Tari) Uyole kilichopo jijini hapa kwa lengo la kutoa elimu kwa wakulima na kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao ya nafaka na mboga.

Mkurugenzi wa Kituo hicho, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maonyesho hayo ambayo alisema yamefikia asilimia 85.

Dk. Bucheyeki alisema maonyesho hayo yanalenga kuwasaidia wakulima kuwapa mbinu na teknolojia za kisasa kwenye kilimo cha mazao ya nafaka na mboga.

Alisema teknolojia 30 ambazo walibuni zitaleta tija kwa wakulima kwa kuwa kupitia mashamba darasa yao yamekuwa kivutio kwa wengi wakihitaji kufundishwa.

"Miongoni mwa mazao ambayo tumebuni teknolojia mpya kuanzia kwenye kupanda hadi kuvuna ni mahindi, maharage, ufuta, karanga na upande wa mboga ni spinachi, vitunguu, hoho, nyanya na karoti na teknolojia hizo zinamsaidia mkulima kupata mavuno mengi," alisema.

Alisema maonyesho ya teknolojia hiyo ambayo yanalenga kwenye kilimo biashara, yalianza tangu Desemba 20 mwaka 2019 na yanatarajiwa kumalizika Mei 9, mwaka huu na imani yake kila mkulima atakayetembelea maonyesho hayo ambayo yanafanyika katika ofisi za kituo hicho watazalisha kwa tija na kuongeza mavuno.

Ofisa Kilimo Mtafiti wa Tari Uyole, Boniphace Minja, alisema bado wanaendelea kufanya utafiti na kugundua aina mbalimbali za teknolojia na mbegu bora ambazo zinaendana na mabadiliko ya tabia nchi.

Alisema kituo hicho kina lengo la kuwasaidia wakulima kupata mbegu bora ambazo zinaendana na aina ya udongo kwenye maeneo husika na kuwashauri wakulima kuzingatia maelekezo wanayopewa na watafiti hao kabla na baada ya kupanda ili kuepuka hasara.

Baadhi ya kampuni zinazoshiriki maonyesho hayo zimetoa ushauri kwa wakulima kuendelea kujitokeza ili waweze kuzifahamu mbegu kinzani na magonjwa yanayoyoshambuliwa mazao yao.

# Costech yashauriwa kutambua wabunifu vyuoni

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

TUME ya Sayansi na Teknolojia (Costech), imeshauriwa kutenga fungu maalumu la fedha litakalotumika kutambua, kuzifikia na kuziendeleza kazi zote za ubunifu zinazobuniwa na wanafunzi wa vyuo vikuu na wananchi wengine ili kuleta tija na kusaidia kufikia uchumi wa viwanda.

Ushauri huo ulitolewa jana na Kaimu Rasi, Ndaki ya Sayansi na Elimu ya Ufundi Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya Must, Dk. John John, wakati wa ufunguzi wa maonyesho ya ubunifu yanayofanyika Chuo cha Sayansi na Teknolojia (Must), yakiwashirikisha watu kutoka viwandani, wanafunzi na wafanyakazi kutoka vyuo mbalimbali mkoani humo.

Dk. John alisema miongoni mwa vikwazo vinavyosababisha ubunifu kushindwa kuleta tija ni Costech kutokuwa na fungu maalumu la fedha ambalo litasimamia na kuziendeleza kazi bunifu zinazofanywa na vijana.

Aliishauri Costech kuandaa sera ambazo zitalinda haki ya mbunifu, taasisi aliyotoka na taifa ili kuepuka wizi wa kazi ambao unafanywa na baadhi ya watu wakidai wao ndiyo wabunifu.

"Vyuo vikuu vina kazi kuu tatu ambazo ni kufanya utafiti, kufundisha na kutoa ushauri wa kitaalamu, ni muda sasa Costech kuandaa sera maalumu ambayo italinda kazi ya mbunifu pamoja na kuendeleza kuliko ilivyo sasa ndoto za vijana wengi zinaishia njiani kwa sababu ya kutoungwa mkono, lakini nashauri kuwawezesha kifedha wabunifu wote wanabuni vitu vyenye tija kwa maendeleo ya nchi," alisema Dk. John.

Rais wa Chuo cha Must, Hassan Masanja, aliwashauri wanafunzi wenzake kujikita kwenye ujuzi wa kijiditaji ambao unaangalia na kutafuta matatizo ya vitu mbalimbali vinavyotokea ndani ya jamii.

Alisema Wiki ya Ubunifu itumike vyema na wanachuo kuongeza maarifa ambayo yatakwenda kutatua vikwazo kwa wananchi ikiwamo mazingira.

Naye Naibu Makamu Mkuu wa Chuo cha Mipango, Fedha na Mipango Must, Dk. Justinian Anatory, alisema chuo hicho kimekuwa na msaada mkubwa kwa jamii kuwasaidia katika nyanja za sayansi na teknolojia.

Alisema chuo hicho ni miongoni mwa wanufaika wa fedha kutoka mfuko wa ubunifu unaofadhiliwa na watu wa Uingereza, HDIF, kwa ajili ya kuendeleza ubunifu ikiwamo matumizi ya simu na mazingira.

Mkurugenzi wa Fedha na Utawala kupitia mfuko wa ubunifu unaofadhiliwa na HDIF nchini Tanzania, Revocatus Vedasto, alisema mfuko huo ulianza kufanya kazi tangu mwaka 2013 na kwamba wanafunzi na wabunifu mbalimbali wamenufaika.

Aliwahamasisha wadau kupeleka ubunifu wao kwenye mfuko huo ili wawezeshwe fedha na kuleta matokeo huku akikipongeza Must kuandika wazo lenye tija.



Wanafunzi wabunifu wa Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya Must, pamoja na wananchi wengine wakifuatilia kwa karibu mdahalo wa wiki ya ubunifu, chuoni hapo, jijini Mbeya juzi, unaolenga kuzitambua na kuziendeleza kazi zao ili zilete tija kwa Taifa, kuelekea uchumi wa viwanda. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# RC atoa miezi 2 wadaiwa sugu kurejesha mikopo

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ametoa muda wa siku 60 kwa wadaiwa sugu wa deni la Sh. bilioni 1.09 ambalo ni mikopo kutoka kwa wanachama wa Chama cha Ushirika wa Akiba na mikopo Lulu, kilichopo jijini hapa kurejesha fedha hizo haraka.

Chalamila alitoa agizo hilo juzi wakati wa sherehe za maadhimisho ya sita tangu kuanzishwa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo Lulu, na kusisitiza ambao hawatazirejesha kwa muda alioutoa atachukua hatua kali za kisheria.

Alisema chama hicho ni miongoni mwa vyama vinavyofanya vizuri katika uwezeshaji wa wanachama wake kiuchumi pamoja na akiba kubwa ya pesa ikilinganishwa na vingine.

Aliwataka waliokopa na kushindwa kurejesha fedha kwa wakati warudishe ili wasikitie doa chama hicho ambacho kinaaminika na wakazi mbalimbali wa Jiji la Mbeya.

"Yeyote anayejiona ni mdaiwa sugu kwenye chama hiki nimetoa muda wa miezi miwili kurejesha fedha ili na wengine waanze kukopa, nawahakikishia ambaye hataweza kutoa anakamatwa na kupelewa polisi," alisema Chalamila.

Meneja wa chama hicho, Emmy Ntale, alieleza vikwazo mbalimbali vinavyorudisha nyuma maendeleo kuwa ni baadhi ya wanachama kushindwa kurejesha mikopo yao kwa wakati.

Alisema chama kimekuwa na utaratibu wa kutoa mikopo kwa wanachama wake kwa awamu, lakini baadhi yao wanalazimisha kukopeshwa bila kufuata utaratibu na sheria ikisimamiwa wanadai kuna upendeleo. Mwenyekiti wa Bodi ya chama hicho, Byalugaba Chengule, aliahidi kupeleka majina yote ya wadaiwa sugu kwa Mkuu wa Mkoa, Albert Chalamila ili hatua zichukuliwe.

Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo mkoani humo, Angela Maganga, aliwashauri wadaiwa wote kurejesha fedha hizo kwa wakati kabla hawajafikishwa kwenye vyombo vya sheria.





# Kongwa yakaribisha wawekezaji

**Na Ibrahim Joseph, KONGWA**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kongwa imetoa wito kwa wawekezaji mbalimbali kuchangamkia fursa ya uwekezaji wilayani humo kutokana na miundombinu kuboreshwa.

Wito huo ulitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Dk. Omari Mkulo, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye wilaya hiyo.

Alisema kutokana na kukamilika kwa baadhi ya miundombinu ya barabara kwa kiwango cha lami kuingia Kongwa mjini na maeneo mengine kwa kiwango cha changarawe wawekezaji wanakaribishwa kuchangamkia fursa ya kuwekeza.

Dk. Mkulo alisema halmashauri hiyo inakaribia kukamilisha ujenzi wa barabara kutoka Mbande hadi Kongwa mjini kwa kiwango cha lami ambayo itarahisisha kuingia na kutoka kwa urahisi ndani ya mji huo.

Alibainisha kuwa utekelezaji wa ujenzi wa barabara hiyo unajengwa kwa thamani ya Sh. bilioni 11 na unatarajiwa kukamilika mwezi ujao.

Mkurugenzi huyo alisema halmashauri imekamilisha ujenzi wa mtandao wa barabara kwa kiwango cha lami za ndani ya mji zenye zaidi ya kilometa nane kwa kutumia mapato ya ndani na fedha kutoka serikalini.

Aliongeza kuwa ujenzi wa barabara huo umeenda sambamba na uwekaji wa taa za barabarani ambazo zitawawezesha wananchi na watumiaji wengine wa barabara kutumia wakati wa usiku bila ya kuwa na mashaka ya kuvamiwa na vibaka.

"Utakuwa na uwezo wa kutembea kwa miguu au kutumia baiskeli wakati wa usiku kutoka Mbande hadi Kongwa Mjini bila mashaka yoyote ya kuvamiwa na vibaka au utaweza kuendesha gari bila kuwasha taa wakati huo wa usiku kwa sababu ya taa hizo zitakuwa na nguvu," alisema.

Aidha, alisema wawekezaji wanaweza kuwekeza katika wilaya hiyo kutokana na kuwa na utajiri wa mazao ya kilimo kama karanga, alizeti, mahindi, mtama na ufuta.

Aliutaja utajiri mwingine uliopo kwenye wilaya hiyo kuwa ni uwepo wa mifugo ya ng'ombe, mbuzi na kondoo inayofungwa na wananchi na Ranchi ya Taifa ya Kongwa.

Aliishukuru serikali kwa kuendelea kutoa fedha za ujenzi wa miradi mbalimbali katika wilaya hiyo ikiwamo afya, elimu na maji.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Zuberi White, alisema katika msimu wa mwaka huu watakuwa na uhakika wa kuvuna mazao ya kutosha kutokana na wingi wa mvua.

Aliwataka wananchi kutunza akiba ya kutosha ya chakula wasidanganyike kutokana na soko zuri la mazao hayo litakalokuwapo.



Muuguzi wa Hospitali ya Benjamin Mkapa mkoani Dodoma, Pascal Mathewsela (katikati), akitoa elimu kwa wananchi namna ya kutumia dawa ya Sanitizer ya kuua vijidudu vya magonjwa, ikiwa ni juhudi za kujikinga na virusi vya corona, wakati wa maonyesho ya mashindano ya kitaifa ya sayansi na teknolojia na ubunifu, katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Machinga Nyerere Square waonywa

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma, imetoa onyo kwa wafanyabiashara wadogo (Machinga) kuacha kupanga bidhaa zao kabla ya muda uliopangwa kwenye barabara ya Nyerere Square ili kutozuia watumiaji wengine wa barabara.

Katika barabara hiyo, wafanyabiashara hao wanapaswa kupanga bidhaa zao kuanzia saa 10:00 jioni baada ya muda wa kazi kuisha, lakini wameonekana kukiuka utaratibu huo na kuanza kupanga kabla ya muda huo.

Onyo hilo lilitolewa jana na Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, alipokuwa akizungumza na wafanyabiashara hao wanaofanya biashara katika eneo hilo.

Alisema hivi sasa wamekuwa wakipanga bidhaa muda wa asubuhi hali inayoleta usumbufu kwa watumiaji wengine wa barabara.

"Wafanyabiashara mnapaswa kufuata sheria, kanuni na maagizo yaliyoelekezwa na jiji ya kufanya biashara zao kwa muda waliopangiwa ili barabara hii itumike kwa shughuli nyingine," alisema.

Aliongeza: "Jiji halitakuwa tayari kuwaona baadhi yenu mkikiuka maelekezo mliyopewa ya kufanya biashara zenu kwa muda mlioambiwa wa kuanzia saa kumi hadi saa tatu usiku, vinginevyo tutawaondoa bila nyinyi kupenda suala ambalo halina tija kwa pande zote hivyo ninawataka mzingatie maelekezo sivyo vinginevyo."

Sambamba na hilo, aliwataka kuzingatia usafi kwenye maeneo ambayo wamekuwa wakifanya biashara zao.

"Hii ni pamoja na kutokiuka maelekezo ya maeneo mnayotakiwa kufanya shughuli zenu ili kuepukana kuondolewa kwa nguvu na kusababisha hasara ya bidhaa zenu," alisema.

Kadhalika, ofisa huyo alisema kuwa bado kuna tatizo kwa baadhi ya machinga ya kuvamia maeneo yasiyo rasmi ikiwamo kando kando ya barabara na kwenye mitaro ya kupitisha maji na kusababisha adha kwa watumiaji wengine.

Alisema halmashauri imetenga barabara zinazotumika kama soko la muda lakini si barabara zote.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara hao kushirikiana na halmashauri ya jiji pale wanaogundua kuna baadhi yao wamekuwa wakikiuka maagizo ili wachukuliwe hatua.

"Pia kuna utapeli kwa baadhi ya wafanyabiashara wanaowalaghai wenzao kwa kuwauzia maeneo ambayo yapo wazi huku wakidai kuwa wana vibali halali toka halmashauri ya jiji jambo ambalo si la kweli," alisema.

# Jafo ataka kasi ya ujenzi Hospitali Uhuru

**Na Augusta Njoji, CHAMWINO**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amemwagiza Mkandarasi wa Suma JKT anayejenga Hospitali ya Uhuru Wilaya ya Chamwino kuongeza nguvu kazi ili ujenzi huo ukamilike kwa wakati.

Hospitali ya Uhuru inayojengwa wilayani Chamwino inajengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 3.5 ikiwa ni fedha ambazo zilitokana na Rais John Magufuli kuzuia maadhimisho ya sherehe za Uhuru mwaka 2018 na fedha za gawio zilizotolewa na kampuni ya Airtel.

Jafo alitoa agizo hilo juzi alipotembelea eneo linalojengwa hospitali hiyo.

Alisema kasi ya ujenzi wa hospitali hiyo bado hairidhishi licha ya kuchelewa kutokana na mvua.

Jafo alisema wanatakiwa kuongeza kasi ya ujenzi kwa kuongeza vijana wengi wa JKT ili kazi hiyo imalizike kwa wakati Mei, mwaka huu.

Naye, Mhandisi wa ujenzi kutoka Suma JKT, Omary Kabalagu, alisema pamoja na kuwa nyuma kwa takribani wiki tisa, taasisi yake imebadili namna ya kujenga, utaratibu ambao utaokoa muda uliopotea na pia jengo litakuwa imara.


"Hapa tumeona tukiweka jamvi itatulazimu kusubiri siku 21 ndio tuendelee kupandisha tofali, kinachofanyika kwa sasa tunapandisha tofali huku tukiwa tumeweka nondo kwa ajili ya nguzo ambazo zitakuja kuwekewa zege baadaye," alisema.

Katika hatua nyingine, Jafo alikagua maandalizi ya ujenzi wa barabara za Mji wa Serikali Mtumba, na kumtaka Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA) kuhakikisha anamsimamia kwa karibu mkandarasi aliyepewa kazi ya kujenga barabara za mji wa serikali inayogharimu takribani Sh. bilioni 88.1 ili kazi hiyo ikamilike ndani ya miezi 18 iliyopangwa.

Kufuatia maelekezo hayo, Mtendaji Mkuu wa Tarura, Victor Seff, alisema maandalizi ya ujenzi wa mtandao wa barabara hizo utakaokuwa na urefu wa kilomita 51.2 yameanza tangu Februari mosi mwaka huu.

Alieleza kuwa barabara hizo itahusisha uwekaji wa taa za kuongoza magari, taa za barabarani, mifereji mikubwa na barabara za watembea kwa miguu.

## HABARI ZANZIBAR



# Corona yapandisha bei maski, sabuni

**Na Rahma Suleiman, UNGUJA**

SIKU moja baada ya kugundulika kwa mgonjwa wa corona nchini, bei ya maski na sabuni maalum ya kuoshea mikono (hand sanitizer) zinazotumika kujikinga na virusi hivyo zimepanda.

Akizungumza na Nipashe jana, mfanyabiashara wa dawa za binadamu eneo la Darajani mjini Unguja, Khamis Omar, alisema kuwa muda mfupi baada ya kugundulika kwa mgonjwa wa corona nchini, wateja walimiminika dukani kununua maski na sanitizer.

Alisema tayari vifaa hivyo vimepanda bei na vimeanza kuadimika Zanzibar.

Alibainisha kuwa awali maski moja ilikuwa ikiuzwa Sh. 500 na sasa inauzwa Sh. 1,500, wakati boksi moja lenye maksi 50 hivi sasa linauzwa Sh. 60,000 wakati awali ilikuwa Sh. 7,500.

Alisema chupa moja ya sanitizer yenye ujazo wa nusu lita ilikuwa ikiuzwa Sh. 9,000 na sasa inauzwa Sh. 12,000 na chupa ndogo iliyokuwa inauzwa Sh. 2,500, sasa inauzwa Sh. 3,500.

"Kidumu cha lita tano cha sanitizer kinauzwa Sh. 75,000 na hivi sasa imeshaanza kuadimika, watu wengi wanakuja kununua hasa wenye kampuni," alisema.

Baadhi ya wananchi wameishauri serikali na mashirika mbalimbali kutoa bure vifaa hivyo kwa wananchi kwa kuwa baadhi yao hawana uwezo kumudu gharama zake.

Abeda Suleiman, mkazi wa Kisauni Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, alisema ni vyema serikali ikatoa vifaa hivyo kwa wananchi bila malipo ili wajikinge na corona.

"Kama serikali ilivyotupatia vyandarua bure na kutupigia dawa majumbani kwa ajili ya kujikinga na malaria, tunaiomba pia itusaidie na hili," alisema.

Aliongeza kuwa ni vigumu kwa mwananchi mwenye kipato cha chini kwenda kununua maksi ya 1,500 wakati nyumbani hana hata chakula.

Waziri wa Afya, Hamad Rashid Muhamed, alisema tayari serikali imeshasambaza maski katika hospitali zote za wilaya na vifaa vingine vya kutoa huduma kwa wananchi ambao watagundulika kuwa na maambukizo ya virusi vya corona.

Aliwataka wananchi kuwa na utamaduni wa kuosha mikono yao mara kwa mara kwa kutumia maji na sabauni ili kujikinga na ugonjwa huo.

"Kama mtu hana uwezo wa kununua sanitizer, atumie maji yalio safi na sabuni, aoshe mikono yake maana kinga ni bora kuliko tiba," alisema.



Mwanafunzi wa Sekondari Shule ya Mikindani mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Khamis Shehe (kulia), akitoa maelezo kwa waandishi wa habari wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Ubunifu mjini Zanzibar jana, ambapo mwanafunzi huyo, amebuni kifaa cha kupata umeme.
**PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Zeco yajivunia mafanikio usambazaji wa umeme

**Na Rahma Suleiman, UNGUJA**

SHIRIKA la Umeme la Zanzibar (Zeco) limesema limevuka malengo ya usambazaji wa umeme vijijini na kufikisha huduma hiyo katika visiwa vidogo vya Unguja na Pemba kwa asilimia 100.

Akizungumza na waandishi wa habari, Meneja Mkuu wa Zeco, Hassan Ali Mbarouk, alisema shirika limevuka malengo kwa kusambaza umeme vijijini kwa asilimia 113.

Alisema shirika limesambaza umeme katika vijiji 520 kwa kutumia miradi tofauti ya usambazaji umeme vijijini kupitia Shirika la Misaada la Norwad (Norad) na sasa limebaki na vijiji vichache ambavyo havijapata huduma hiyo.

Alisema Zeco imevuka malengo na kusambaza umeme katika visiwa vidogo vipatavyo 10 vya Unguja na Pemba huku vikibakia visiwa viwili ambavyo bado wananchi wake hawajapata nishati hiyo.

"Shirika la Umeme la Zanzibar limevuka malengo ya utekelezaji wa ilani kwa wastani wa asilimia 100 katika majukumu na kazi lilizotakiwa kuzifanya na Serikali Kuu... tulitakiwa kufikisha umeme vijijini na tumefanya na katika visiwa vidogo vinavyoishi, watu tumepata mafanikio hayo," alisema.

Alisema kwa sasa ni visiwa viwili tu vinavyoishi wananchi ambapo huduma ya umeme haijafikishwa, ambavyo ni Kisiwa cha Njau na Kokota, vyote vipo Pemba.

Mbarouk alisema wananchi wengi kwa sasa wanatumia nishati ya umeme hadi vijijini, hivyo matumizi kuongezeka kutoka MW 40 mwaka 2008 hadi kufiki ya MW 90.

Alisema huo ni ushahidi tosha kwamba wananchi wamehamasika katika kutumia nishati ya umeme na kuachana na matumizi ya kuni na kuchoma mkaa ambayo ni sehemu ya uharibifu wa mazingira.

"Katika ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2015-2020, tunatakiwa tuwahamasishe wananchi kutumia nishati ya umeme kikamilifu ili waache kutumia kuni na mkaa ambavyo ni vyanzo vya uharibifu wa mazingira," alisema.

# Maonyesho ubunifu yaanza rasmi Z'bar

**Na Mwandishi Wetu, UNGUJA**

KWA mara ya kwanza Zanzibar inaadhimisha Wiki ya Ubunifu itakayokuwa na maonyesho mbalimbali ya ubunifu na ujasiriamali.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Cube Zanzibar, ambao ndiyo waandaji wa wiki ya ubunifu, Said Suleiman, aliyasema hayo alipozungumza na waandishi wa habari mjini Zanzibar.

Alisema katika wiki hiyo ya ubunifu iliyoanza jana, kutakuwa na maonyesho ya wajasiriamali na ubunifu ili kuona ubunifu unaofanywa na vijana.

Alisema vijana wengi wanatumia teknolojia, lakini hawajui kujilinda hivyo wiki ya ubunifu itatoa elimu kwao kuhusu kujilinda na teknolojia.

Mkurugenzi huyo alisema matumizi ya teknolojia ni rahisi, hivyo watatoa elimu jinsi ya kuzitumia taka kwa maendeleo ili kuhifadhi mazingira.

Ofisa Tehama wa Kampuni ya D-Tree International, Haji Masoud Ibrahim, alisema lengo la wiki ya ubunifu ni kuwawezesha vijana kuitumia mitandao ya kijamii kwa maendeleo yao na taifa.

Vijana waliojitokeza kuonyesha kazi zao za ubunifu zikiwamo za masuala ya kuunganisha umeme, walisema masomo wanayofundishwa shuleni yamewasaidia kuwa wabunifu.

"Hapa tumetengeneza kifaa hiki ambacho kinaleta umeme ambao unaweza kutumika kwa matumizi madogo. Kupitia somo la Fizikia, tumeweza kutengeneza kifaa hiki," alisema Khamis Shehe, Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Mikindani Wilaya ya Magharibi A Unguja.

Kauli mbiu ya wiki hiyo ya ubunifu ni 'kuvumbua kwa maendeleo ya jamii'.

# Zungu: Miradi SGR, Kinyerezi ni salama

**Na Robert Hokororo**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, amesema miradi ya reli ya kisasa (SGR) na uzalishaji wa umeme kwa gesi wa Kinyerezi, imezingatia vigezo vya mazingira.

Zungu aliyasema hayo jana wakati akiwasilisha taarifa mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, inayoongozwa na Mwenyekiti, Sadiq Murad, ilipotembelea na kukagua miradi hiyo jijini Dar es Salaam.

Alipongeza utekelezaji wa miradi hiyo na kubainisha kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais imeshirikishwa katika hatua zote za utekelezaji wa miradi hiyo.

"Tumekuja hapa na tumejiridhisha mradi huu umefuata taratibu zote za mazingira na vibali vyote vilitolewa pamoja na mapendekezo ya maeneo ya kufanyia maboresho, NEMC (Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira) walikuja hapa Kinyerezi mara tano kuthibitisha, taka ngumu na za sumu zinadhibitiwa na pia misitu yetu ipo salama," alisema.

Kamati hiyo ya Bunge ilipongeza serikali kwa utekelezaji wa miradi hiyo, Murad akisema kuwa mradi wa SGR unaotekelezwa na serikali kupitia Shirika la Reli (TRC) unakwenda kwa kasi na umekidhi vigezo vyote vya mazingira.

Mwenyekiti huyo aliagiza NEMC kuendelea kusimamia kwa karibu masuala yote yanayohusu mazingira katika miradi hiyo ili kuepuka athari zinazoweza kujitokeza kwa jamii na mazingira hapo baadaye.

"Niwapongeze Mkurugenzi wa TRC na timu yake, kwa kweli wamejitahidi sana kwa ujenzi huu na unakwenda kwa spidi nzuri, lakini NEMC wana kazi ya ziada ya kuendelea kuwa karibu nao waje kuwashauri kwani ushauri wao utakuwa na faida kubwa kwa nchi yetu hapo baadaye," alisema.

Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alisema katika miradi hiyo, Shirika la Umeme (Tanesco) kila mwaka wanatenga Sh. milioni 50 kwa ajili ya utunzaji wa mazingira.



Mamalishe akisonga ugali kwa ajili ya mlo wa mchana kwa wateja wake, kando ya Barabara ya Kijenge, eneo la Sayansi Miti Mirefu, Kijitonyama jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

## ZRB yasaidia ujenzi ofisi wenye ulemavu

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

BODI ya Mapato Zanzibar (ZRB), imekabidhi vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. milioni 10 kwa jumuiya ya watu wenye ulemavu Wilaya ya Micheweni kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya jumuiya hiyo.

Vitu vilivyotolewa ni saruji mifuko 100, nondo 40, mchanga magari matatu, kokoto magari manne, matofali 4,000 na fedha taslimu Sh. 2,500,000.

Akizungumza na wananchi na wanachama wa jumuiya hiyo baada ya kukabidhi vifaa hivyo, Kamishna wa ZRB, Joseph Abdalla Meza, alisema wamefanya hivyo ili kusaidia jengo hilo liweze kutumika.

Meza alieleza kuwa ZRB ni taasisi ya serikali ambayo inajishughulisha na ukusanyaji wa mapato Zanzibar, na kuwa imefanya hivyo kutokana na maelekezo wanayoyapata kutoka kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohammed Shein, kuwa kila mahali ambapo panahitajika msaada wahakikishe wanasaidia.

Kamishna huyo pia alieleza kuwa watafarijika sana kuona mchango huo walioutoa utatumika kama ilivyokusudiwa katika kukamilisha ujenzi wa ofisi hiyo hadi kufikia hatua ya uwezekaji.

Katibu Tawala Wilaya ya Micheweni, Hassan Abdalla Rashid, alieleza kuwa jumuiya ya watu wenye ulemavu katika wilaya hiyo walikuwa wakikabiliwa na changamoto kubwa kutokana na kutokuwa na ofisi ya kufanyia shughuli zao za kila siku.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Micheweni Shamata Shaame Khamis, aliipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na taasisi mbalimbali kwa michango yao mbalimbali wanayoitoa ndani ya jimbo hilo katika kufanikisha shughuli za maendeleo.

**Meza alieleza kuwa ZRB ni taasisi ya serikali ambayo inajishughulisha na ukusanyaji wa mapato Zanzibar, na kuwa imefanya hivyo kutokana na maelekezo wanayoyapata kutoka kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohammed Shein, kuwa kila mahali ambapo panahitajika msaada wahakikishe wanasaidia.**

# NIT yaomba TBS kutoongeza mikataba ukaguzi magari nje

**Na Prosper Makene**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), kimeliomba Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kutokuongeza mikataba na kampuni ya ukaguzi wa magari nje ya nchi.

Lengo ni kuwezesha magari yote yakaguliwe nchini kulisaidia taifa kuongeza mapato na siyo kupeleka mabilioni ya pesa Japan, Uingereza, Dubai na Marekani.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkuu wa NIT, Prof. Zacharia Mganilwa, alisema kuwa chuo hicho kina vifaa vya kisasa vya ukaguzi wa magari yaliyotumika, hivyo hakuna haja tena ya TBS kuendelea kupeleka mabilioni ya fedha nje ya nchi kwa ajili ya ukaguzi.

"TBS imekuwa ikitumia mawakala wa ukaguzi wa magari nje ya nchi, na gari moja limekuwa likikaguliwa kwa kiasi cha Dola za kimarekani 150, sasa kwa kuwa vifaa vyote vya kisasa tunavyo hapa nchini katika chuo chetu cha taifa cha usafirishaji hakuna haja tena kwa Shirika la Viwango kuendelea kupeleka pesa hizo nje ya nchi," alisema.

Prof. Mganilwa aliongezea: "Nawaomba mara wamalizapo mikataba na kampuni hizo zilizopo nje ya nchi basi wasiweze kusaini tena mikataba mipya ili kutoa wigo kwa Chuo chetu cha Taifa cha Usafirishaji kuweza kufanya kazi hiyo ambayo itaongeza pato kwa Taifa na hivyo kusaidia katika harakati za Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli, ambaye amejikita katika kuleta maendeleo kwa Watanzania."

Mganilwa alisema kuwa kama gari moja lina kaguliwa kwa dola 150 nchini Japan, Dubai, Uingereza na kwingineko nje ya nchi, magari yakiwa mengi ambayo yatakaguliwa nchi, basi NIT itaweza kuangalia upunguzwaji wa gharama hizo ikiwa ni sababu mahusisi kuweza kufanya pesa hizo kubaki nchini.

"Badala ya kutoza dola 150 kama wanavyotozwa nje ya nchi sisi tutaona uwezekano wa kupunguza gharama hii. Tunataka kuona ni jinsi gani mabilioni hayo ya pesa yataweza kubaki nchini, tunakila sababu ya kuwaomba TBS wasitishe kusaini mikataba mipya, tunauwezo mkubwa wa kukagua magari yote yanayoingia kutoka nje ya nchi," alisema.

Alitanabaisha kuwa kwa siku moja NIT inayo uwezo wa kukagua magari zaidi ya elfu moja katika kituo chao cha ukaguzi wa magari kilichopo kampasi yao kuu ya Mabibo jijini Dar es Salaam.

"Chuo kimewekeza teknolojia ya hali ya juu kabisa katika kituo cha ukaguzi wa magari, ikiwa ni mahususi katika kulinda usalama katika sekta ya usafirishaji. Tunaamini teknolojia yetu ni sawa na ambazo zinatumika katika mataifa yaliyoendelea kama Japan, Uingereza, Dubai na Marekani," alisema.

## Tshisekedi, Kabila wazungumzia mageuzi tume ya uchaguzi

**KINSHASA,** Congo

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi na mtangulizi wake Joseph Kabila wametathmini makubaliano yao ya kugawana madaraka, kufuatia kuibuka kwa tofauti nyingi baina yao.

Wiki za hivi karibuni hali ya kutoaminia ilijitokeza baina ya maofisa wa serikali na idara za kiusalama kutokana na vuguvugu la FCC la Kabila na lile la CACH la Rais Tshisekedi.

Taarifa ya pamoja iliyotolewa baada ya mazungumzo baina ya viongozi hao iliyosomwa na Vital Kamerhe kiongozi wa ofisi ya Rais Felix Tshisekedi, inaelezea kuwa mazungumzo baina ya Tshisekedi na Kabila yalifanyika katika hali ya utulivu.

Kamarhe alisema miongoni mwa masuala waliozungumzia ni pamoja na mageuzi ya mfumo wa uchaguzi na pia tume ya uchaguzi.

Viongozi hao wawili waliamua kuwapo na mazungumzo ya mara kwa mara kwa ajili ya mwenendo bora wa mkataba wao wa uongozi wa pamoja, na wamekubaliana kuanzisha mazungumzo kwa ajili ya mageuzi ya mfumo wa uchaguzi nchini. **DW**

## Marekani yawawekea vikwazo viongozi wawili

**HARARE,** Zimbabwe

MAREKANI imewawekea vikwazo viongozi wawili wa Zimbabwe kwa ukiukaji wa haki za binadamu.

Viongozi hao ni Waziri wa Usalama, Owen Ncube na Balozi wa Zimbabwe nchini Tanzania, Anselem Sanyatwe kwa kuhusika na mashambulizi dhidi ya wapinzani.

Wizara ya Fedha ya Marekani imeeleza kuwa viongozi hao walihusika na mashambulizi dhidi ya waandamanaji nchini humo.

Hatua hiyo imekuja wiki moja baada ya Marekani kuongeza vikwazo vya kiuchumi dhidi ya Zimbabwe kwa kipindi cha mwaka mmoja zaidi.

Taarifa ya Wizara ya Fedha ya Marekani imeeleza kuwa Waziri wa Usalama wa Zimbabwe, Owen Ncube amewekwa katika orodha ya watu waliowekewa vikwazo na Marekani kufuatia tuhuma kwamba aliwaamuru maofisa wa usalama wa nchi hiyo kuwavamia na kuwatesa wanachama wa upinzani.

Kwa mujibu wa wizara hiyo, pia imemwekea vikwazo Anselem Sanyatwe, Balozi wa Zimbabwe nchini Tanzania, ikimtuhumu kuongoza mashambulizi ya maofisa wa usalama dhidi ya wapinzani baada ya uchaguzi wa mwaka 2018. **DW**

# Akubali kuchomwa sindano yenye virusi vya corona

**WASHINGTON,** Marekani

WAKATI dunia ikihaha kupambana na ugonjwa hatari wa virusi vya corona sambamba na kupata tiba yake, nchini Marekani mtu mmoja amejitokeza ili kufanyiwa jaribio la chanjo ya kinga ya ugonjwa huo.

Mtu huyo kujitolea kupata dozi ya kwanza ya utafiti huo siku ya Jumatatu ni mama wa watoto wawili, Jennifer Haller mwenye umri wa miaka 43 mkazi wa Seattle Washington.

Shirika la habari la Associated Press la nchini humo limeeleza kuwa wagonjwa wanne walidungwa sindano yenye virusi vya ugonjwa wa corona katika kituo cha utafiti kiitwacho Kaiser Permanente kilichopo mjini Seattle, Washington.

Hata hivyo, chanjo hiyo haiwezi kusababisha Covid-19, lakini ina jeni la virusi ambavyo vinaweza kusababisha ugonjwa.Wataalamu wanasema itachukua miezi mingi kujua ikiwa chanjo hiyo au utafiti mwingine utafanikiwa.

"Hii ni fursa ya kufurahisha kwangu mimi kuweza kufanya kitu fulani," alisema mama huyo.

> **Badala yake, inajumuisha kipande kifupi cha aina ya jeni iliyonakiliwa kutoka kwa virusi ambavyo wanasayansi wameweza kuvitengeneza katika maabara.**

Wanasayansi kote duniani wanaharakisha utafiti wao kujaribu kupata chanjo au tiba ya virusi vya corona.

Na jaribio hili la kwanza kwa binadamu, lililodhaminiwa na Taasisi ya Kitaifa ya Afya nchini Marekani umefanyika kando ili kuangalia kile ambacho kwa kawaida kingekuwa kikifanyika kuhakikisha chanjo inaweza kusababisha kuchochewa kwa kinga ya mwili katika wanyama.

Lakini kampuni ya teknolojia ya masuala ya vimelea wa magonjwa ambayo ndiyo inayoendesha utafiti huo, Moderna Therapeutics, inasema kuwa chanjo imeshatengenezwa kwa kutumia mchakato uliojaribiwa na kupimwa. Dk. John Tregoning, mtaalamu katika magonjwa yanayoambukiza katika Taasisi ya Imperial College mjini London, Uingereza amesema chanjo hiyo imetumia teknolojia iliyokuwapo awali.

"Imefanyika kwa kiwango cha hali ya juu, kwa kutumia vitu ambavyo tunavyofahamu ni salama kuvitumia katika watu na wale wanaoshiriki katika jaribio hili watakuwa wakifuatiliwa kwa karibu sana.

"Ndio, hili limefanyika haraka sana, lakini ni mbio dhidi ya virusi, siyo dhidi ya kati ya mwanasayansi na mwanasayansi na inafanyika kwa manufaa ya binadamu," alisema Dk. Tregoing.

Dk. Tregoing alisema chanjo halisi ya virusi kama vile vinavyosababisha magonjwa kama surua hutengenezwa kutokana na virusi vilivyodhoofishwa au vilivyokufa.

Alisema lakini chanjo ya mRNA-1273 haijatengenezwa kutokana na virusi vinavyosababisha ugonjwa wa virusi vya corona.

"Badala yake, inajumuisha kipande kifupi cha aina ya jeni iliyonakiliwa kutoka kwa virusi ambavyo wanasayansi wameweza kuvitengeneza katika maabara. Chanjo hii huenda ikasaidia mwili kujitengenezea mfumo wake wa kinga wa kupigana na ugonjwa halisi," alisema na kuongeza:

"Waliojitolea kufanyiwa jaribio la chanjo walipewa dozi tofauti za jaribio la chanjo. Kila mmoja atadungwa sindano mbili za virusi kwa ujumla, baada ya siku 28, kwenye mshipa wa sehemu ya juu ya mkono."

Alisema hata kama vipimo vya awali vimefanikiwa, bado inaweza kuchukua hadi miezi 18 kuweza kuwa na uwezekano wowote wa chanjo kuweza kupatikana kwa umma. **BBC**




Makamu wa Rais wa zamani wa Marekani, Joe Biden (kushoto) na Seneta wa Jimbo la Vermont, Bernie Sanders, wakati wa mdahalo uliofanyika mjini Washington DC. **PICHA: AP**

# Watu 19 wakamatwa kwa kueneza umbea

**ANKARA,** Uturuki

UTURUKI imesema imewabaini watuhumiwa 93 wanaochapisha taarifa zisizokuwa na msingi kwenye mitandao ya kijamii kuhusu mlipuko wa virusi vya corona ambazo ni za uchochezi na zinalenga kueneza hofu miongoni mwa watu.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Uturuki imesema kati ya watuhumiwa hao 19 wamekamatwa na wanashikiliwa na kwamba msako unaendelea kuwatafuta waliobaki.

Jumatano iliyopita, Uturuki moja kati ya nchi zenye uchumi mkubwa ilirripoti kuzuka nchini humo virusi vya ugonjwa wa corona na Waziri wa Afya, Fahrettin Koca alitangaza maambukizi mapya 29 kuthibitisha kuwa idadi ya watu ilongezeka na kufikia 47.

Wakati huo huo, Ofisi ya Gavana wa Istanbul imesema kwamba raia wa Uturuki ambao wanaotaka kurudi kutoka kwenye nchi tisa za Ulaya watarejeshwa usiku wa leo kwa sharti kwamba watawekwa karantini kwa muda wa siku 14. **DW**

# Wenye mita mbovu za maji kufungiwa mpya

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Vipimo Nchini (WMA), imewataka wananchi wenye malalamiko ya kufungiwa mita za maji mbovu kufika kwenye ofisi zake mapema ili waweze kufungiwa mita mpya.

Kwa mwaka mmoja sasa WMA kupitia kituo chake cha Misugusugu Mkoa wa Pwani imefanya ukaguzi wa mita 83,257 za maji na kubaini 530 hazifai.

Hayo yalisemwa jana na Ofisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Ludovick Manege, wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Mazingira kwenye kituo chake cha Misugusugu kinachopita dira za maji na matangi ya kusafirishia mafuta.

"Mtu akiona mita yake ni mbovu asikae kimya tuna ofisi kila mkoa afike awaone maofisa wa WMA wataiondoa na kumwekea mpya, hatutaki kuona mwananchi analipa bili ya maji isiyo sahihi," alisema Manege.

Manege pia aliwaonya wazabuni wanaoagiza mita za maji nje ya nchi kuhakikisha wanaziwasilisha WMA kwa ajili ya ukaguzi ili kuona kama zinafaa kabla ya kusambazwa kwa watumiaji wa mwisho.

Alisema hivi sasa serikali inatekeleza miradi mingi mikubwa ya maji hivyo wazabuni wa mita za maji wanapaswa kuwa makini kuagiza zitakazowatendea haki wananchi na kuondoa malalamiko.

"Kumekuwa na malalamiko mengi ya mita za maji sasa sisi WMA tutaendelea kuwabana wazabuni kwa kuhakikisha wanazileta hapa zipimwe kabla ya kuwafungia wananchi hivyo mzabuni akiagiza mita mbovu ajue atapata hasara yeye maana hazitafungwa," alisema Manege.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Mazingira, Suleiman Sadiq Muradi, alipongeza WMA kwa kufanya kazi kisasa zaidi hasa kwenye kituo hicho cha Misugusugu.

Alisema WMA imefanikiwa kuzifanyia kazi changamoto ambazo wabunge walizitoa wakati kamati hiyo ilipokutana na maofisa wa wakala mwaka jana mkoani Dodoma.

Alisema wabunge wamejionea namna mita na matangi ya kusafirishia mafuta yanavyofanyiwa ukaguzi ili kupata vipimo sahihi kwa watumiaji wa mwisho na ameahidi kufanyia kazi changamoto walizoona.



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Mazingira, wakishangaa kisima kirefu cha kuhifadhia maji yaliyochanganyika na mafuta cha Wakala wa Vipimo (WMA), katika eneo la Misugusugu, wilayani Kibaha, mkoani Pwani walipotembelea kituo hicho cha ukaguzi wa mita za maji na matangi ya kusafirishia mafuta. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Auawa kwa kuchomwa moto tuhuma wizi mahindi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MTU ambaye hajafahamika jina wala makazi, anayekadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 25-30, amekutwa akiwa amekufa kwa kuchomwa moto, baada ya kutuhumiwa kuiba mahindi shambani wilayani Kahama mkoani Shinyanga.

Tukio hilo lilitokea Jumapili majira ya jioni eneo la Mwime, ambapo wananchi wanaodaiwa kuwa na hasira kali walimpiga mtu huyo kisha kumchoma moto.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Deborah Magiligimba, baada ya mtu huyo kukamatwa na mahindi hayo, wananchi walimpiga kisha kumchoma moto pamoja na baiskeli aliyokuwa amebebea mahindi hayo.

"Katika eneo la tukio la kuchomwa moto, kulikuwa na mahindi pamoja na baiskeli karibu na mwili wa mtuhumiwa kama kiashiria kwamba alitumia baiskeli hiyo kubebea mahindi hayo," alisema Magiligimba.

Alisema mwili wa mtu huyo umehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Kahama," aliongeza kamanda huyo.

Alisema Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi wa tukio hilo na kuwabaini watu waliohusika kujichukulia sheria mikononi.

## Tigo, Samsung wazindua simu janja 3

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Tigo, kwa kushirikiana na Samsung Electronics, wamezindua simu janja aina ya Samsung Galacy S20, Galacy S20+ na Galaxy S20 Ultra.

Meneja wa bidhaa za intaneti wa Tigo, Mkumbo Muyonga, akizungumza jana jijini Dar es Salaam, wakati wa uzinduzi wa simu hiyo alisema ushirikiano huo ni sehemu ya mkakati wa Tigo wa kuongeza matumizi ya mtandao wa 4G na kuchangia ukuaji wa teknolojia ya kidijitali nchini.

"Ni jambo la kubwa kwetu kuchaguliwa na Samsung kuwa wa kwanza kuzihifadhi na kuuza simu za Samsung S20 kwenye soko la Tanzania. Hii inaonyesha imani yao kwetu juu ya chaneli kubwa za usambazaji tulizonazo na pia kupitia timu yetu ya huduma kwa wateja inayotoa huduma zenye ubora wa hali ya juu," alisema Muyonga.

Alisema lengo la Tigo ni kuchochea mageuzi ya kidijitali katika maisha ya watu nchini na ndio maana wameungana na Samsung ili kuongeza idadi ya umiliki wa simu janja pamoja na matumizi ya data katika kuhakikisha watu wengi zaidi wanafikiwa na teknolojia hiyo.

"Tunalenga kuongeza uenezaji wa simu janja nchini huku tukihakikisha wateja wetu wanafurahia huduma za kidigitali kupitia mtandao mkubwa wa 4G nchini. Na ndio maana tunatoa 78 Gb za intaneti kwa mwaka mzima kwa wateja wote watakaonununa Samsung S20," alisema.

Meneja wa Samsung Tanzania, Suleiman Mohamed, alisema kampuni yao imezindua simu ya Samsung Galaxy S20 toleo jipya ulimwenguni ambayo itabadilisha maisha ya watu na kuufurahia ulimwengu.

"Tukiwa tunaingia kwenye muongo mwingine, kuna mabadiliko makubwa kwenye sekta ya mawasiliano na namna watu wanavyoujua na kuufurahia ulimwengu. Samsung inahakikisha inatoa teknolojia na vifaa vya kisasa zaidi ili kuendana na mabadiliko hayo. Kwa kutumia camera yenye mfumo wa AI unaweza kupata kila tukio na kuungana na uwapendao bila mipaka," alisema Mohamed.

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**VIWANJA VINAUZWA,** Headline block ya viwanja vine inauzwa, Viko mbweni mpiji karibu na Shule ya Sekondari Mpiji . Eneo zaidi ya heka moja ) 4220 Sq mt . Viwanja Surveyed. Simu: 0711 506758 0787 445506, 0679 041220


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI (SUMMONS)**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI KAHAMA WILAYA YA KAHAMA**

**SHAURI LA JINAI/MADAI/MIRATHI/TALAKA/PINGAMIZI 2/2020**

**KWA ALEX WILLIAM KISHIMBA DAR ES SALAAM, 0712 800767**
**K.K HAKIMU MKAZI MFAWIDHI KAWE –DAR ES SALAAM**

**Kwa kuwa imelazimika uhudhurie ili KUJA KUJIBU KESI YA PINGAMIZI YA MIRATHI MAHAKAMA YA MWANZO MJINI KAHAMA.**

Unaamuriwa na JAMHURI uhudhurie mbele ya Mahakama hii siku ya **JUMANNE tarehe 24/03/2020** saa 2:00 asubuhi/Mchana na ukifika usioondoke bila ruhusa ya mahakama.

Unaonywa kwamba ikiwa utakataa kupokea wito huu au kupuuza bila udhuru kwa maana hati itatolewa kukulazimisha uhudhuria na utashtakiwa kwa kosa hilo.

Hati hii imetolewa kwa AMRI yangu na MUHURI wa Mahakama hii leo JUMATATU Tarehe 2/03/2020.

PRINCIPAL ... COURT MAGISTRATE
URBAN COURT KAHAMA

Nimepokea nakala ya kuitwa shauri hii nakubali nitafika
Sahihi ya mtu anaepelekewa wito

115671302

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ELIAS FRANSIS KALIKOWELE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 957 BYQ** aina ya **DAF-CF.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/235650/2020.**

115671702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA KINONDONI**
**SHAURI LA MIRATHI NA.13 YA 2020**

RWEBUGISA RWABYO MUTAHABA......MWOMBAJI
DHIDI YA
RUGEMALIRA MBEIKYA MUTAHABA.........MAREHEMU

Kwa,
Yeyote anayehusika au mwenye maslahi
Kwa kuwa mdai ameleta ambayo maelekezo ya maombi yameelezwa katika nakala za maombi amabzo zinawezaa kupatikana katika mahakama hii. Kwa hiyo mtu yeyote mwenye maslahi katika maombi ya mirathi tajwa hapo juu anapaswa kuweka pingamizi na kuhudhuria katika mahakama hii wilaya hapo juu anapaswa kuweka pingamizi na kuhudhuria katika mahakama hii ya wilaya binafsi au wakili au mwakilishi ambaye anayeruhusiwa kabla au siku ya tarehe 30 Mwezi 3,2020 saa mbili (2:00) kamili asubuhi . Kwa kuwa siku hiyo ni kutajwa kwa shauri unatakiwa kuja na vielelezo vyote vinavyohusiana na maombi ya mirathi hii.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama leo tarehe 28 mwezi wa 02,2020

MAHAKAMA YA WILAYA KINONDONI

HAKIMU MKAZI

156718

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DAVID MWANGOLE MOSHY** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T.148 AGX aina ya Toyota Corolla. Chassis namba 6083540, Engine namba 4K5904922.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.
Taarifa ya polisi
**IR/TR/RB/57/2020.**

156715

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YA MIZIGO

**EMILY PHILLEMON LEO**
Anatangaza kupotelewa na Kadi ya Pikipiki ya mizigo aina ya SKYMARK CARGO yenye namba ya usajili MC 738 ATK Chassis namba B21NEF11K14X00345 Engine namba B21N1631MLE0000345

Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo cha Polisi.

Taarifa ya Polisi:
**MWA/NY/RB/570738/2019**

156716


***Uza, Chenye Thamani Kubwa***

***Kwa Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Khamisi Kigwangalla, akipokea maji kutoka kwa Meneja Mawasiliano wa Kampuni ya Tanga Cement, Mtanga Noor, wakati wa mbio za Kili Marathon zilizofanyika Machi Mosi mjini Moshi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kili Marathon inavyodunda na Tanga Cement miaka 17

**Na Mwandishi Wetu**

KWA mara nyingine tena historia imeandikwa katika mbio kongwe nchini za Kilimanjaro Marathon, zilipofanyika mjini Moshi mkoani Kilimanjaro Machi Mosi, mwaka huu na kuhudhuriwa na maelfu ya wakimbiaji kutoka nje na ndani ya nchini.

Katika mbio hizo ambazo mwaka huu zilisherehekewa kutimiza miaka 17 tangu kuanzishwa kwake, zilikuwa za aina yake kutokana na wanariadha walioshiriki kuonyesha viwango vya juu na wale wa Kitanzania kukataa kuwa wateja kwa kufanya vizuri isivyo kawaida.

Mbali na rekodi zilizowekwa, kwa upande wa Kampuni ya Tanga Cement ambayo ilikuwa moja ya wadhamini waliokuwa na jukumu ya kutoa huduma ndogondogo kama maji katika vituo vilivyotumika kwa mbio hizo, nayo imejivunia miaka 17 ya kuwapo katika mbio hizo.

Tangu kuanzishwa kwa mbio hizo, Tanga Cement imekuwa ikishiriki Kili Marathon katika maeneo mbalimbali kwa kutoa wafanyakazi wake kushiriki katika mbio, huku pia ikiwa mstari wa mbele katika kutoa huduma kwa wanariadha.

> Mbio za Kili Marathon zimekuwa zikikua kila uchao kwa kuwa washiriki kutoka mataifa mengine nao wanaongezeka.

Kwa mwaka huu pekee, zaidi ya wafanyakazi 22 kutoka Tanga Cement walijitokeza kushiriki mbio hizo na miongoni mwao, akiwamo mshiriki wa 'Full Marathon' (Km 42), Meneja Mipango, Fanuel Petro.

Wengine 21 walikimbia mbio za Nusu Marathon (Km 21) na wote waliweza kuibuka na medali kwa kukamilisha mbio hizo bila matatizo yoyote tofauti na washiriki wengine ambao waliishia njiani.

Ikumbukwe jumla ya wanariadha 11,300 kutoka mataifa mbalimbali ya Afrika na Ulaya, walijitokeza katika mbio hizo ambazo zimejizolea umaarufu mkubwa ndani na nje ya nchi kutokana na kuteka hisia za watu wengi pamoja na kuwavutia kushiriki.

Aidha, ni vigumu kutaja mafanikio ya Kili Marathon pasipo kuwashukuru wadhamini wa mbio za Km 42, Kilimanjaro Lager, Tigo wanaodhamini Nusu Marathon (Km 21) na wadhamini wa 'Fun run' (Km 5), Grand Malt.

Kwa mwaka huu, jumla ya wanariadha 800 walikimbia mbio za Km 42, huku Nusu Marathon ikiwa na washiriki 5,500 na zile za Km 5 walijitokeza wanariadha 5,000, hapo unaweza kuona ni namna gani zilivyowavutia watu wengi.

Akizungumzia sababu ya uwapo wa Tanga Cement katika mbio hizo kwa miaka yote hiyo, Meneja Biashara wa kampuni hiyo, Peet Brits, amesema ushiriki wao kwa miaka 17 unatokana na kila mwaka kuzidi kuvutiwa na ubora wake na tukio lenyewe na jinsi zinavyoboreshwa mwaka hadi mwaka huku zikivutia watu wengi duniani.

Amesema kampuni yao ilitoa wafanyakazi 22 katika mbio hizo, huku wakikimbia katika mbio tofauti tofauti kulingana na uwezo wa kila mmoja.

"Tanga Cement PLC kupitia bidhaa chapa ya Simba Cement, imekuwa ikidhamini Kilimanjaro Marathon tangu mbio hizo zilivyoanzishwa, hizi ni miongoni mwa matukio makubwa ya michezo ambayo yamekuwa kivutio kikubwa kwa wafanyakazi wetu," anasema.

Anasema mbali na kujitolea kushiriki katika mbio zote na kutoa maji katika vituo, pia wametoa fursa ya kukutana na wateja wao na kuwasikiliza.

"Mbio za Kili Marathon zimekuwa zikikua kila uchao kwa kuwa washiriki kutoka mataifa mengine nao wanaongezeka," anasema Brits.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Kili Marathon, John Bayo, ameitaja Tanga Cement kuwa sehemu muhimu katika mbio hizo.

Anasema ukikosa wadhamini wenza kama hao haitakuwa rahisi kufanikisha mbio hizo ambazo zimefanyika kwa miaka 17.

Katika mbio hizo za mwaka huu, Watanzania Joseph Panga na Magdalena Shauri waliibuka washindi wa Tigo Nusu Marathon na hivyo kufanya wanariadha wa Tanzania kung'ara huku nafasi pili imeshikwa na Mtanzania mwingine Josephat Joshua ambaye alitumia muda wa saa 1:04:28 akifuatiwa na Mkenya Vincent Towett aliyeshika nafasi ya tatu akitumia muda wa saa 1:04:32.

Panga alivunja mwiko kwa mbio hizo ambazo kwa miaka mingi zimekuwa zikitawaliwa na raia wa kigeni husasan Wakenya ambao kwa kipindi kirefu wamekuwa wakiibuka washindi.

Kwa upande wa wanawake, mwanariadha Magdalena aliibuka na ushindi wa kishindo kwa kutumia muda wa saa 1:09:54 baada ya kumbwaga Mkenya Susy Chebet aliyeshika nafasi ya pili kwa kutumia muda wa saa 1:16:18, akifuatiwa na Valentina Jepkorir kutoka Kenya.

Mbio hizo za Kilimanjaro Marathon hufanyika mjini Moshi kila mwaka huku idadi ya washiriki ikiongezeka. Kwa mujibu wa waandaaji idadi hiyo imeongezeka kutoka wakimbiaji 750 hadi kufikia washiriki 11,000 kwa sasa.

## Uefa yajadili kuipeleka Euro mwaka 2021

**LONDON,** England

SHIRIKISHO la vyama vya soka Ulaya, Uefa, linatarajia kuahirisha michuano ya mataifa ya Ulaya, Euro 2020, hadi mwaka 2021 katika kikao chao cha jana Jumanne kujadili hatima ya mashindano hayo kutokana na ligi kusimamishwa kwa mlipuko wa virusi vya corona.

Kusogezwa mbele kwa michuano hiyo inamaana kuaathiri pia mashindano ya Ligi za Mataifa ya Uefa na mashindano ya Ulaya kwa umri chini ya miama 21 na yale ya wanawake yanayotarajiwa kufanyika mwaka 2022.

UEFA pia inatarajia kuhakikisha mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na ile ya Europa Ligi kumalizika msimu huu, hata kama yatachelewa.

Kwa sasa Uefa inadadili pia uwezekano wa michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya robo fainali kuchezwa mchezo mmoja badala ya kuwa na marudiano ili kupata muda wa kumalizika haraka.

Mapendekezo hayo yalitarajiwa kujadiliwa jana Jumanne yakiwa yamependekezwa na rais wa Uefa, Aleksander Ceferin.







## MAN UNITED YAJITOSA KUMWANIA UMTITI

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imeripotiwa kwamba inajitosa kumsajili mlinzi wa kati wa Barcelona, Samuel Umtiti kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 yupo katikati ya msimu wake wa nne pale Nou Camp, lakini hajaweza kujiimarisha yeye mwenyewe kwenye kikosi cha kwanza.

United na Arsenal zote zimeonesha nia ya kumsajili beki huyo, lakini mashetani wekundu sasa wanataka kuongeza nguvu ili kumsajili beki huyo, kwa mujibu wa Daily Sport.

United awali waliripotiwa kutaka kumsajili beki wa kushoto, lakini sasa wanamtaka Umtiti ambaye kocha wake, Quique Setien anaweza kuruhusu aondoke.

Mlinzi wa kati wa Napoli, Kalidou Kouliably kwa muda mrefu pia amekuwa akiwaniwa na Man United, lakini sasa Umtiti anaonekana kuwa chaguo la kwanza.

Raia huyo wa Ufaransa ameanza katika mechi tisa tu za Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, msimu huu na amekuwa kama msaidizi wa Clément Lenglet tangu alipojiunga hapo Barca kipindi cha majira ya joto mwaka 2018.

## *Liverpool ina kikosi cha thamani zaidi Ulaya*

**LONDON** England

LIVERPOOL imetajwa kuwa yenye kikosi cha gharama zaidi katika ligi tano kubwa barani Ulaya, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na kampuni ya CIES uliochapishwa kwenye gazeti la Daily Mail la jana.

Kikosi hicho cha kocha, Jurgen Klopp ndio chenye thamani kubwa zaidi kwenye soka la usajili katika ligi hizo tano kubwa Ulaya kikiwa na thamani ya pauni bilioni 1.27, ikifuatiwa na Manchester City yenye thamani ya bilioni 1.24.

Kushinda kwao taji la Ligi ya Mabingwa msimu uliopita kumewafanya vijana hao wa pale kwenye dimba la Anfield kukizidi kikosi cha Pep Guardiola pamoja na Barcelona na Real Madrid.

Miamba wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Barca na Real Madrid wametofautiana kwa jumla ya pauni milioni 63.

Barcelona wapo nafasi ya tatu ambapo thamani ya kikosi chake ni pauni bilioni 1.06, huku Real Madrid wakiwa nafasi ya nne kwa thamani ya pauni bilioni 1.00.

Nafasi ya tano inashikwa na Chelsea yenye kikosi chenye thamani ya pauni milioni 917, huku Manchester United wakiwa nafasi ya sita ambapo thamani yake ni pauni milioni 917.

Klabu cha Paris Saint-Germain inashika nafasi ya saba kikiwa na thamani ya pauni milioni 890, Atletico Madrid ikiwa nafasi ya nane kwa thamani ya pauni milioni 760, huku Tottenham ikiwa nafasi ya tisa kwa thamani ya pauni milioni 715, huku nafasi ya 10 inashikwa na Juventus ambayo kikosi chake kina thamani ya pauni milioni 712.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# KANE AGOMBEWA NA JUVENTUS, MADRID

Zote zinajipanga kumsajili kipindi cha majira ya joto, wakati mwenyewe anapambana...

**MADRID,** Hispania

JUVENTUS na Real Madrid zote zipo kwenye mbio moja za kuwania kumsajili mshambuliaji wa Tottenham Hotspur, Harry Kane kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

Kwa mujibu wa gazeti la AS la nchini Hispania, klabu hizo zinataka kumsajili Kane, huku kila moja ikiwa na nia ya kupanua kikosi chake wakati wa dirisha hilo kubwa la usajili wa majira ya joto.

Kane hajacheza mchezo wowote tangu mwaka mpya 2020 kwa sababu ya kuumia misuli, lakini ameanza kufanya mazoezi ya peke yake wiki iliyopita, wakati akiwa anapambana kurudi dimbani.

**Nyota huyo wa timu ya taifa ya England mwenye umri wa miaka 26 mara kadhaa amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka pale Tottenham, ambako mkataba wake wa sasa unamalizika kipindi cha majira ya mwaka 2024.**

Kabla ya kuingia kwenye majeruhi hayo, Kane tayari alikuwa ameshafunga mabao 17 katika mechi 25 alizoichezea Tottenham katika mashindano yote msimu huu.

Kwa ujumla Kane amefunga mabao 181 katika mechi 278 alizoichezea Tottenham, huku akiwapita Jimmy Greaves (mabao 266) na Bobby Smith (mabao 208) wakiwa ndio wachezaji walioifungia timu hiyo mabao mengi zaidi.

Licha ya kutambulika kama mmoja wa washambuliaji bora duniani, Kane bado hajashinda taji lolote akiwa na Tottenham na pengine anaweza kushawishika kuondoka kabuni hapo kwa ajili ya kutafuta sehemu atakayoweza kutwaa taji.

## ZISIKUPITE

### MAN CITY KUTOMZUIA MAHREZ

KLABU ya Manchester City haitazuia uhamisho wa winga wa Algeria, Riyad Mahrez mwenye umri wa miaka 29, kwenda kujiunga na Paris St-Germain kipindi cha majira ya joto. ***(Goal)***

### MAN UNITED KUMSAJILI UMTITI

MIAMBA wa Ligi Kuu ya England, Manchester United, itajaribu kwa bidii kubwa kumsajili mlinzi wa kati wa Barcelona na timu ya taifa ya Ufaransa, Samuel Umtiti mwenye umri wa miaka 26, kipindi cha majira ya joto. ***(Sport)***

### YAJIPANGA KWA DEMBELE

TIMU ya Chelsea kipaumbele chake ni kumsajili mshambuliaji wa Lyon na Ufaransa, Moussa Dembele mwenye umri wa miaka 23, wakati dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto litakapofunguliwa. ***(Daily Mail)***

### NYOTA ATAKIWA STAMFORD

KLABU ya Chelsea imeripotiwa kufanya mawasiliano na Porto kwa ajili ya uwezekano wa kumsajili mlinzi wa kushoto wa Brazil, Alex Telles mwenye umri wa miaka 27. ***(A Bola)***

### WAJITOSA KWA MARTINEZ

KLABU za Manchester City na Chelsea zipo kwenye mbio moja ya kuwania kumsajili mshambuliaji wa Inter Milan na timu ya taifa ya Argentina, Lautaro Martinez. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 22 amekuwa akihusishwa na mpango wa kusajili Barcelona. ***(Sport)***

### AZIGONGANISHA ARSENAL, SPURS

MLINZI wa kati wa Liverpool na timu ya taifa ya Croatia, Dejan Lovren mwenye umri wa miaka 30, anawaniwa na klabu za Arsenal na Tottenham. ***(Mirror)***

### BAINES ATAKA MWAKA MMOJA

BEKI wa kushoto wa timu ya taifa ya England, Leighton Baines mwenye umri wa miaka 35, anataka kuongeza mkataba wa mwaka mmoja na Everton licha ya uvumi kuzagaa kwamba anataka kwenda LA Galaxy. ***(Daily Mail)***

### ZAMWANIA PELLEGRINI

KLABU ya Inter Milan imeungana na Everton kwenye mbio za kumsajili kiungo wa AS Roma na Italia, Lorenzo Pellegrini mwenye umri wa miaka 23. ***(Calciomercato)***

### KLOPP KUPIGA PANGA NYOTA 6

KOCHA Jurgen Klopp anataka kukifanyia mabadiliko makubwa kikosi chake cha Liverpool na inaweza kushuhudia wachezaji sita wakiondoka. ***(Mirror)***

### DALOT AMPA TANO FERNANDES

BEKI wa Manchester United, Diogo Dalot mwenye umri wa miaka 20 raia wa Ureno amesema mchezaji mwenzake, Bruno Fernandes atakuwa "gwiji" wa klabu hiyo. ***(Sky Sports)***

### SPURS YAMWINDA DOGO WA QPR

KLABU ya Tottenham Hotspur inamfuatilia kwa karibu, kiungo wa Queens Park Rangers, Eberechi Eze mwenye umri wa miaka 21 na wanaweza kumsajili kipindi cha majira ya joto kijacho. ***(Sun)***

HABARI MICHEZO

## Corona kuahirisha Mwalimu Cup

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

TIMU za soka 24 zilizopo katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha zimejitokeza kushiriki katika mashindano ya Kombe la Mwalimu (Mwalimu CUP) yaliyoanza kutimua vumbi jana katika viwanja vya Mwendapole.

Hata hivyo, jana jioni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa, alipiga marufuku shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu kwa kipindi cha mwezi mmoja, ikiwamo michezo.

Awali kabla ya agizo hilo la Waziri Mkuu, Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano hayo, Saimon Mbelwa akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa jana alisema, mashindano hayo yatafanyika katika viwanja vinne tofauti.

Mbelwa alisema kuwa mashindano hayo ambayo yamedhaminiwa na Mwalimu Aboubakary Alawi, yana lengo la kuibua vipaji kwa vijana, kuimarisha michezo na kujenga urafiki.

Alisema mashindano hayo yanasimamiwa na Chama cha Mpira wa Miguu Kibaha (Kibafa) na yatafanyika katika viwanja vya Mwendapole, Visiga, Mailimoja na Kongowe.

Mbelwa alisema katika mashindano hayo mshindi wa kwanza atanyakua kitita cha Sh. 500,000, kombe na medali na mshindi wa pili ataondoka na Sh.300,000 na medali huku mshindi wa tatu akijinyakulia kiasi Sh.200,000.

Katibu wa Kibafa Daudi Mhina 'Mourinho' alisema ni muda mrefu Kibaha haijapata mtu wa kudhamini michezo, lakini kwa sasa chama kimefarijika kumpata Mwalimu Alawi na kudhamini michezo hiyo.

## CAVB yazuia wavu Tanzania

**Na Saada Akida**

MWENYEKITI wa Chama cha Mpira wa Wavu, Patrick Mlowezi, amethibitisha kutokuwapo kwa mashindano ya Afrika ya mchezo wa ufukweni hatua ya pili ya kutafuta nafasi ya kushiriki michezo ya olimpiki kwa wanaume.

Michuano hiyo ya awamu ya pili ilikuwa ishirikishe nchini nchi tano ambazo ni Afrika Kusini, Sudan, Ghana, Niger pamoja na Tanzania ambao ni wenyeji.

Mlowezi ametoa sababu kubwa ya kuahirishwa kwa shindano hilo lililotarajiwa kuanza Machi 27, mwaka huu katika fukwe za Coco, jijini Dar es Salaam, kuwa ni kutokana na kuwapo baada ya kupokea barua kutoka Shirikisho la Mpira wa Wavu Afrika, CAVB.

Alisema wameahirisha shindano hilo baada ya barua hiyo ya CAVB, wakihofia juu ya maambukizi ya virusi vya corana (COVID-19) ikiwataka kuiahirishwa kwa matukio yote ya kimichezo barani Afrika kwa kipindi cha Machi 16 hadi Aprili 30, mwaka huu.

"Kwa taarifa hiyo shindano la Afrika tulilokuwa tumeandaa la mpira wa wavu wa ufukweni halitakuwapo na badala yake tunasubiri ratiba mpya kutoka CAVB, kuhusu timu yetu iliyopo kambini itaendelea kuandaliwa hadi Machi 30, 2020 ambapo kambi itaahirishwa rasmi," alisema Mlowezi.

Hata hivyo, jana Waziri Mkuu wa Tanzania, Kassim Majaliwa alipiga marufuku shughuli zote za mikusanyiko ikiwamo michezo kwa kipindi cha mwezi mmoja kutokana na tishio la kusambaa kwa virusi vya corona.

# NDAYIRAGIJE AFURAHIA STARS KUJINOA KWA GPS

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, Etienne Ndayiragije, amesema teknolojia mpya ya vifaa vya kutambua utimamu wa mwili wa mchezaji (GPS) inayotumika ndani ya timu hiyo kwa sasa itamrahisishia kazi ya kutambua muda na uwezo wa wachezaji wake wakiwa mazoezini.

**Ndayiragije alisema kwa sasa wachezaji wanatumia vifaa maalumu ambavyo wanavivaa (GPS) ambavyo anaamini vitamrahisishia kutambua utimamu wa mwili kwa wachezaji.**

"Vifaa wanavyovaa wachezaji wakiwa mazoezini vinasaidia kutambua utimamu wa mwili, pamoja na uwezo wao na muda ambao wamefanya mazoezi hiyo inarahisha katika kutambua ubora wao.

"Hivi pia vimekuwa vikitumiwa na wachezaji wakubwa katika kufanya mazoezi, ni kitu kizuri na nina imani kitakuwa na matokeo chanya," alisema Ndayiragije.

Alisema vifaa hivyo pia vitasaidia makocha wa klabu wanazotoka wachezaji hao kujua kiwango cha mazoezi kama kimepanda au kushuka.

Akizungumzia kuhusu kuwapo kwa fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) baada ya mlipuko wa virusi vya corona kuikumba duniani, kocha huyo alisema bado hajapata taarifa ya kuwapo ama kutokuwapo kwa michuano hiyo.

Alisema kwa sasa wanasubiri taarifa kutoka Shirikisho la Soka Afrika (Caf) juu ya kuwapo au kutokuwapo kwa michuano hiyo inayotarajiwa kufanyika nchini Cameroon kuanzia Aprili 4-25, mwaka huu.

"Kwa sasa hali imekuwa si nzuri juu ya ugonjwa huu, pia hadi sasa hatujajua kama CHAN itakuwapo kati ya siku hizi mbili, tunatarajia kupata taarifa juu ya michuano hiyo," alisema Ndairagije.

Aidha, alisema hana taarifa yoyote juu kutokuripoti kambini kwa kiungo wa Simba Jonas Mkude licha ya wachezaji wenzake wote kufika kwa muda na kuendelea na mazoezi.

Alisema, haelewi sababu za mchezaji huyo kutokuripoti kambini na kudai kama leo (jana) hataripoti kambini atatoa tamko rasmi kama ataendelea kumhitaji ndani ya kikosi hicho au ataamua kuachana naye.

"Ni kweli Mkude hajaripoti kambini na taarifa zake mpaka sasa sina licha ya wachezaji wenzake wa Simba kuripoti, nashangaa ila nina imani meneja anaweza kunipa taarifa juu ya sababu ya kutoripoti kwa mchezaji huyo," alisema.

Stars imepangwa Kundi D pamoja na Zambia, Guinea na Namibia kwenye michuano hiyo ya CHAN.

VIFAA...




Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa, Tarimba Abbas (wa pili kulia), akikabidhi vifaa vya michezo kwa timu ya KISA Academy iliyopo chini ya Abdallah 'King' Kibadeni (kulia), katika hafla fupi ya makabidhiano hayo yaliyofanyika Kisarawe ikiwa ni Kampeni ya SportPesa ijulikanayo kama KITS FOR AFRICA wilayani Kisarawe. **PICHA: SPORTPESA**

# Eymael aitwa kumwaga 'upupu' Yanga

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya timu ya Yanga kurejea jijini Dar es Salaam juzi ikitokea Ruangwa mkoani Lindi, ilipolazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Namungo FC, uongozi wa timu hiyo unatarajia kukutana na Kocha wao Mkuu, Luc Eymael muda wowote kuanzia sasa, ili kutoa dukuduku zake kuhusu kikosi hicho.

Akizungumza na Nipashe jana, Makamu Mwenyekiti wa klabu hiyo, Fredrick Mwakalebela alisema baada ya kikosi kurejea watakaa kikao kizito na kocha wao ili aweze kuwaeleza yale yote ambayo yalimkwaza kuelekea katika mchezo huo, ambao alisikika akiwalaumu baadhi ya wachezaji kuwa wanachagua mechi, kwa kumpa sababu ambazo hazielewi.

"Tutakutana na kocha wetu siku za hivi karibuni ili atueleze kiundani yale yote ambayo hajaridhishwa nayo kabla na baada ya kuelekea katika mchezo huo ambao tulipata matokeo ya sare, tulikuwa hatuhitaji matokeo hayo," alisema Mwakalebela.

Makamu Mwenyekiti huyo alisema baada ya kukutana na kocha huyo na kumsikiliza dukuduku zake uongozi utatoa tamko na kudai kwa sasa hawawezi kulitolea ufafanuzi suala hilo mpaka hapo kikao hicho kitakapomalizika.

"Ni kweli hata sisi haturidhishwi kuona wachezaji wanakwenda kinyume cha matakwa ya kocha, tutamsikiliza kocha kwa sababu wachezaji wote wapo chini yake, halafu ndipo tuchukua hatua kwa yale ambayo atakuwa atueleza," alisema.

Katika hatua nyingine, alisema kikosi hicho kitaendelea na mazoezi leo baada ya kuwapa mapumziko ya siku moja wachezaji wao, wakati kwa upande wa wachezaji walioitwa kwenye kikosi cha timu ya Taifa waliwaruhusu jana asu-

# Michezo

Jumatano Machi 18, 2020

Nipashe



Kane agombewa na Juve, Madrid

UKURASA 30



Beki wa Highlands Park ya Sauzi na Taifa Stars, Abdi Banda, anayehofiwa kuwa na maambukizi ya virusi vya corona. **PICHA: MTANDAO**

# CORONA YATIBUA UBINGWA SIMBA

## ● ● ● Serikali yaizuia kuutangaza mapema, benchi la ufundi kukutana leo kujadili...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba walikuwa wakipiga hesabu kali za kushinda michezo yao mitano tu kati ya 10 waliobakiza ili kutwaa ubingwa msimu huu, mipango hiyo imetibuliwa rasmi kutokana na hofu ya maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19) vinavyoitikisa dunia kwa sasa.

**Kutibuliwa huko kunatokana na hatua muhimu iliyochuliwa na serikali kwa kusimamisha kwa kipindi cha mwezi mmoja kuanzia jana, shughuli zote za kijamii na kisiasa ikiwamo michezo, zinazosababisha mikusanyiko ya watu wengi, hivyo kuikumba Ligi Kuu na Ligi Daraja la Kwanza, kutokana na hofu ya kusambaa kwa virusi hivyo.**

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, juzi alitangaza rasmi mwanamke mmoja wa Kitanzania kubainika kuwa na maambukizo ya virusi vya corona ambaye alitua nchini katika Uwanja wa Ndege wa KIA akitokea Ubelgiji na kisha kulazwa katika Hospitali ya Mt. Meru jijini Arusha. Hatua hiyo, imeifanya serikali kupitia kwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano, Kassim Majaliwa, jana kutangaza rasmi kuzuia kwa kipindi cha mwezi mmoja shughuli zote za mikusanyiko zikiwamo za michezo, kufunga shule kuanzia za awali hadi kidato cha sita kwa kipindi cha mwezi mmoja.

"Kutokana na kusambaa kwa virusi vya corona, kuanzia leo tunapiga marufuku kufanyika shughuli zote za kijamii zinazosababisha mikusanyiko ya watu zikiwamo za kisiasa, michezo ikiwamo Ligi Kuu, kufunga shule za awali, za msingi na kidato cha kwanza hadi cha sita kwa kipindi cha mwezi mmoja kuanzia sasa," alisema Majaliwa.

Na kwa mujibu wa ratiba ya Ligi Kuu, Simba ilikuwa ikiendelea kujifua kwa kasi katika viwanja vyake vya Mo Simba Arena vililivyopo Bunju, nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam kwa lengo la kusaka ushindi katika mechi zake tano zijazo, lakini sasa imepigwa na butwaa ghafla baada ya ligi hiyo kusimamishwa.

Kwanza ilikuwa ikijiwinda katika mechi hizo ambazo zilikuwa hazijapangiwa tarehe kutokana na wachezaji wake wengi kuwa katika kambi ya Taifa Stars wakijiandaa na michuano ya Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani, CHAN iliyokuwa ikitarajiwa kufanyika nchini Cameroon kuanzia Aprili 4-25, mwaka huu.

Mechi hizo zilikuwa dhidi ya Ruvu Shooting katika Uwanja wa Taifa, kisha Mwadui FC (Taifa), Mbeya City (Sokoine), Tanzania Prisons (Sokoine) na kuhitimisha na Ndanda FC kwenye dimba la Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara, ambazo ilikuwa ikihitaji pointi 14 tu ili kufikisha alama 85 ambazo haziwezi kufikia na timu yoyote katika ligi hiyo.

Akizungumza na Nipashe baada ya taarifa hiyo ya serikali kusitisha Ligi Kuu kwa kipindi cha mwezi mmoja, Meneja wa timu ya Simba, Patrick Rweyemamu, alisema bado hawajajua nini cha kufanya hadi kapo watakapokutana mazoezini leo.

"Benchi la ufundi tutakutana kesho [leo] kujua ama tuendelee na mazoezi au tusitishe, uamuzi huo tutautoa katika mazoezi kesho [leo]," alisema meneja huyo ambaye kitaaluma ni kocha.

Rweyemamu alisema kwa kipindi chote ambacho baadhi ya wachezaji wao walikuwa kambini na Taifa Stars, wengine waliobaki walikuwa wakifanya mazoezi wakitokea nyumbani ispokuwa Sharaf Shiboub ambaye aliwahi kuondoka kwenda kwao Sudan kujiunga na timu ya taifa kabla ya Caf kuahirisha mechi za kufuzu Afcon 2021.

Mbali na mechi hizo, pia Simba inayoongoza ligi hiyo ikiwa na alama 71 hadi sasa wakati huu ikiwa imeshuka dimbani mara 28, imebakiza mechi dhidi ya Namungo FC katika Uwanja wa Majaliwa, Mbao FC (Taifa), Alliance (Taifa), Coastal Union (Mkwakwani) na Polisi Tanzania kwenye dimba la Ushirika mjini Moshi.

Azam FC inayoshika nafasi ya pili baada ya mechi 28, ina pointi 54 huku Yanga ilishuka dimbani mara 27 ikifuatia na alama zake 51.

## Beki Stars azuiwa Sauzi kwa corona

**Na Saada Akida**

Beki wa kimataifa wa Tanzania na Klabu ya Highlands Park ya Afrika Kusini, Abdi Banda, amesimamishwa kufanya mazoezi na wenzake kutokana na kuhofiwa kuwa na maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19) na leo anatarajiwa kupewa majibu rasmi baada ya kuchukuliwa vipimo.

Banda ambaye aliitwa katika kikosi cha Taifa Stars kujiandaa na mechi ya kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2021 dhidi ya Tunisia kabla ya Shirikisho la Soka Afrika (Caf) kuahirisha mechi zote za kuwania kufuzu kutokana na tishio la kusambaa kwa virusi vya corona, alizuiwa kufanya mazoezi baada ya kubainika kuwa na mafua makali, homa na kukohoa.

Akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya simu kutoka Afrika Kusini, beki huyo wa zamani wa Simba na Coastal Union, alisema alihisi baridi kali na homa alipokuwa uwanjani katika mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Supersport United Jumapili ya Machi 8, mwaka huu. Baada ya hali hiyo, alisema alilazimika kuondolewa uwanjani kwenda kuchukuliwa vipimo vya virusi vya corona, na leo ndio anatarajia kupata majibu ya vipimo hivyo.

"Nilijisikia baridi sana na hali ya homa, baada ya kutoa taarifa kwa viongozi wangu waliweka tahadhari kwa kunipima, wakihofia ugonjwa huo na kunieleza natakiwa niwe makini na kukaa ndani.

"Wanahofia kwamba nimepata maambukizi ya virusi hivyo, kwa hiyo nimeambiwa nikae ndani, na kutoshiriki mazoezi hadi hapo majibu ya vipimo yatakapotoka," alisema Banda ambaye katika mechi hiyo timu yake ilikubali kipigo cha mabao 2-0.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042